# Nipashe

Ijumaa Oktoba 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581112

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT
TZS.1,044,303,118
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




## Vikao vya juu CCM vyachuja wagombea wa nafasi nyeti

UKURASA 3



Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

BUFE

Wanahabari tuache uchawa kwa wanasiasa

Wazazi wenye kichwa kikubwa, mgongo wazi wanolewa ujasiriamali wajikimu

Ijue Faida Fund; mtaa mpya wa uwekezaji kwa wasio nacho

Samaki Pweza; bidhaa mpya ya mageuzi kwa vijana wa Tanga

UKURASA 13

# Mgawo maji watikisa

• **Rukhsa** wenye visima kufanya biashara... *Endelea ukurasa 2*



Mwonekano wa Daraja jipya la Mto Wami mkoani Pwani baada ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (hayupo pichani), kulikagua jana na kuruhusu magari kuanza kupita kutokana na kukamilika kwa asilimia 96. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

## Wauawa wakipora fedha za VICOBA

UKURASA 25




Ofisa Mkuu Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (katikati) na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Fedha la IFC, Frank Ajilore (wa pili kulia), wakionyesha hati ya kutambulika ya uimara wa kiuchumi na usawa wa kijinsia iliyotolewa kwa NMB na Taasisi ya The EDGE Certified Foundation jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Masuala ya Jinsia wa IFC Afrika, Anne Kabugi (kulia), Ofisa Mkuu Huduma Shirikishi wa NMB, Nenyuata Menjooli (kushoto) na Ofisa Mkuu wa Udhibiti NMB, Doreen Joseph. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CHADEMA yatoa neno maridhiano na Rais Samia



UK. 2

**MICHEZO** NABI AANDAA SILAHA KUWAVAA WATUNISIA UK.32

**KABWELA** UK.25



Wanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Mdote wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakipanga foleni ili kupata chakula cha mchana baada ya kufanya mtihani wa taifa wa darasa la nne ulioanza juzi na kumalizika jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mgawo wa maji watikisa

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kutofanya upendeleo katika ratiba ya mgawo wa maji ulioanza kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani.

Kadhalika, ameitaka DAWASA kushirikiana na wafanyabishara na wadau wenye visima vikubwa vya maji kusambaza maji kwa wananchi na kuhakikisha wanauza maji kwa bei elekezi.

Aweso alitoa agizo hilo wakati alipotembelea kuona kazi inayofanywa na mafundi wa DAWASA ya kuhamisha maji kutoka kwenye bomba la inchi 72 kwenda kwenye bomba la inchi 24 eneo la Wazo kwa lengo la kutoa huduma kwa wakazi wa maeneo ya Bahari Beach, Kunduchi, Kilongawima, Mbezi Beach, Tegeta kwa Ndevu, Kunduchi Mtongani, Africana ambao hawapati huduma hiyo kutokana na kupasuka kwa bomba la inchi 54 eneo la Mbezi Jogoo.

"DAWASA wametoa utaratibu wa jinsi ya watu watakavyopata maji, kwa maana ya ratiba ya mgawo, elekezo la kwanza kwa DAWASA, ratiba ile ambayo imetolewa isitokee upendeleo kwamba hawa wanapata leo, wengine hawapati, kwahiyo ratiba ifuatwe ili kuhakikisha hiki kidogo (maji) kilichoko watu wote wanapata," alisema Aweso.

"Naomba sana watoa huduma (wauza maji kwa boza) kipindi hiki sio kipindi cha kujinufaisha, yaani kufa kufaana...tupo tayari kushirikiana nanyi katika kutoa huduma hii kuhakikisha tunavuka katika kipindi hiki," alisema Aweso.

Aweso alipongeza jitihada za DAWASA katika mradi wa visima wa Kigamboni wenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 70 za maji yatakayosaidia kupunguza makali ya mgawo kwa wakazi wa Dar es Salaam.

Alisema zipo jitihada zinazofanywa na serikali kuhakikisha inamaliza upungufu huo katika Mto Ruvu hasa katika kipindi cha ukosefu wa mvua za vuli kwa kujenga wa Bwawa la Kidunda.

"Huu ni mkakati wa muda mrefu, ni zaidi ya miaka 50 sasa, lakini tunashukuru sana jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika wizara yetu na support (jitihada) yake ya karibu tumeshampata mkandarasi ambaye anakwenda kujenga bwawa lile la kihistoria ambapo mnafahamu, badala ya mvua kuwa maafa katika nchi yetu basi iwe fursa kwa maana gani, mvua inaponyesha maji yanapotea tu baharini lakini ujenzi wa bwawa hili la Kidunda utakusanya maji mengi katika kipindi kama hiki cha kiangazi maji hayo yanaweze kutumika.

Alisema mwezi Novemba mwaka huu Rais Samia atashuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa bwawa hilo na mkandarasi ambaye tayari ameshapatikana.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema matengenezo yanayofanyika eneo la Wazo ni kwa ajili ya kukarabati bomba kubwa la inchi 54 lililopasuka na kusababisha wananchi wa maeneo ya Mbezi Beach, Tegeta, Africana, Makonde na Kawe kukosa huduma.

Kazi inayoendelea ni kwa ajili ya kuhamisha maji kutoka kwenye bomba kubwa la inchi 72 kwenda la inchi 24 ili wananchi waendelee kupata huduma.

Juzi DAWASA ilitoa ratiba ya mgawo wa maji katika Jiji la Dar es Salaam kuanzia jana Oktoba 27 hadi 30, 2022 na kueleza kuwa itakuwa inatolewa kila wiki.

Kwa wakazi wanaohudumiwa na mtambo wa Ruvu Chini, leo maeneo yatakayopata maji kwa saa 24 ni Mwenge, Kijitonyama, Mwananyamala, Makumbusho, Kinondoni, Masaki, Mikocheni, City Center, Kariakoo, Mlalakua, Mlimani City, Chuo Kikuu, Keko na Temeke. Maeneo mengine ni Kigamboni, Magomeni, Tandale, Kigogo Kilongawima, Kunduchi, Meko, Mtongani, Kisanga A&B na Mbezi Beach A&B.

Jumamosi yatakayopata maji saa 24 ni Boko, Tegeta, Kunduchi, Salasala, Mbezi Beach, Ununio, Wazo, Bagamoyo Mjini, Sunguvuni, Zinga, Viwandani, Kiharaka Kerege Mapinga, Mikocheni, Kawe, Mbezi Juu, Goba, Kijitonyama, Mabwepande, Bunju Mkoani na Bunju B&A, Malolo, Mabwepande, Kinondoni, Kibesa, Teta, Mpiji, Maputo, JKT na Mbweni Masaiti, Bunju Beach, Mivumoni, Kilimahewa na Kinzudi.

Jumapili ni Mwenge, Kijitonyama, Mwananyamala, Makumbusho, Kinondoni, Masaki, Mikocheni, City Center, Kariakoo, Mlalakua, Mlimani City, Chuo Kikuu, Keko, Temeke, Kigamboni, Magomeni, Tandale na Kigogo.

Kwa wakazi wanaohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu Ijumaa Oktoba 28,2022 watakaopata maji kwa saa 24 ni Ubungo, Sinza, Magomeni, Mabibo, Manzese, Mlimani City, Tandale na Mburahati Takukuru, Lapaz, Rising Star, Dampo, Brazil, Kanisa la KKKT, Royal hostel na kwa Mama Mary, kwa Fabiani, Hekima, Machimbo, Uzaramuni, Ngorongoro na Kwa Mwanajeshi.

Jumamosi Oktoba 29, 2022 watakaopata maji kwa saa 12 Mtambo wa Ruvu Juu ni Buguruni-Madenge, Mwananchi, TAZARA, Tabata Matumbi, Tabata-Reli, Tabata-Shule, Tabata-Barakuda, Tabata- Bima, Aroma, Kibangu, Kajima na Novo Liwiti, Maruzuku, Myamani na Ubaya Ubaya).

Maeneo mengine ni Unyamwezini, Tabata/Segerea, Kilungule, Kisukuru, Kwa mkua, Kibangu, Makoka, Gide, Bucha, Baruti, Korogwe na Vinane, Tabata Msimbazi, Butiama, Kipawa, Stakishari, viwandani (nyerere road), Kinyerezi Mbuyuni na Kinyerezi Kanga.

Jumapili Oktoba 30,2022 maeneo yatakayopata maji kwa saa 12 Mtambo wa Ruvu Juu ni Ubungo, Sinza, Magomeni, Mabibo, Manzese, Mlimani City, Tandale na Mburahati Takukuru, Lapaz, Rising Star, Dampo, Brazil, Kanisa la KKKT, Royal Hostel na kwa Mama Mary, kwa Fabiani, Hekima, Machimbo, Uzaramuni, Ngorongoro na Kwa Mwanajeshi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
28.10.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe **01-11-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili:
**T 807 DYL / T 416 AYQ T 468 DYG / T 887 DJB T 464 DYG / T 837 DJB**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 24.00** |
| **Upana** | - | **mita 4.60** |
| **Kimo** | - | **mita 5.20** |

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji** kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

27121102

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# CHADEMA yatoa neno maridhiano na Samia

**Na Romana Mallya**

WENYEVITI wa Majimbo Mkoa wa Dar es Salaam wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamesema maridhiano yanayofanywa baina ya chama chao na Rais Samia Suluhu Hassan, yatakuwa na matokeo chanya kwa mustakabali wa taifa.

Hayo yalisemwa jana kwa niaba yao na Mwenyekiti wa chama hicho Jimbo la Kawe, Leonard Manyama, wakati wakijibu hoja zilizotolewa na vyama 14 vya upinzani baada ya CHADEMA kutoa msimamo wa ripoti ya kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia na vyama vingi.

Baada ya CHADEMA kukosoa ripoti hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili wa Baraza la Vyama vya Siasa, Doyo Hassan, alikishangaa chama hicho kuwa kinapingaje ilhali hawajui kilichoandikwa ndani kwa kuwa bado haijawekwa hadharani.

Akijibu vyama hivyo, Manyama alisema, "Vimesubiri CHADEMA itoe maoni ndipo vijitokeze. Vyama vya namna hii ni vya kuvitazama, kujaribu kuviona havina afya kwa mustakabali wa demokrasia ya nchi."

Alisema wao wanasimamia alichokisema Katibu Mkuu wao, John Mnyika, na wanaamini maridhiano yanayofanywa na CHADEMA na Rais Samia yatazaa matokeo chanya kwa ajili ya mustakabali wa taifa.

"Katika majimbo yetu tunawaambia wanachama wawe watulivu tukisikia na kusubiri msimamo wa chama chetu katika maridhiano na tutakuwa tayari kutekeleza kile viongozi wetu watatuongoza tufanye. "Kwa sasa tunasimama na kauli ya chama kwamba taarifa ya kikosi kazi ina mapungufu, ilipaswa kurekebishwa."

Mwenyekiti Jimbo la Ukonga wa chama hicho, Sweya Rajabu, alisema vyama hivyo vinajitokeza vikiona kuna mshike mshike wa CCM na upinzani.

## HABARI KITAIFA

# TICTS yawasilisha mpango wa kuwekeza tril. 1.15/- bandarini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI inayohusika na kitengo cha makasha katika Bandari ya Dar es Salaam (TICTS), imewasilisha serikalini mpango madhubuti wa kuwekeza Sh. trilioni 1.15 kwenye mifumo ya upakuaji na upakiaji makasha bandarini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana, kampuni hiyo imefurahishwa na kuboreka kwa uhusiano wake na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), hatua iliyofanikisha kuimarika kwa utendaji mwaka uliopita.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa mwaka 2021, muda wa meli kusubiria kuingia bandarini ulikuwa mrefu, hali iliyosababisha mrundikano wa meli kwenye bahari kuu.

"Kampuni yetu kupitia kwa kampuni mama ya Hutchison Ports ya China, ilifanikiwa kuwekeza zaidi ya Sh. bilioni 12.5 katika vifaa, mifumo, kuongeza ufanisi, kulitatua na kulimaliza kabisa tatizo hilo sasa hali ni shwari," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

Kutokana na uwekezaji huo mpya, TICTS iliongeza idadi ya makasha yanayopitia kwao kutoka 50,000 kwa mwezi na sasa yanakaribia 70,000.

"TICTS tunaamini kuwa hii ni habari njema kwa wafanyabiashara wa kimataifa nchini na majirani zake wanaotegemea Dar es Salaam kama mlango wao mkuu wa biashara pamoja na bandari kama chaguo lao," ilibainisha taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kuwa pamoja na mafanikio hayo ya mwaka 2022, kumekuwapo na vikwazo kadhaa ikiwamo vifaa vya kazi kuharibiwa katika mazingira ya kutatanisha, mambo yaliyosababisha kuvirekebisha vifaa hivyo kwa gharama kubwa pamoja na kutoa ripoti polisi kwa waharibifu hao.

"Wakati wote huo kampuni yetu pia imefanya kazi kwa karibu sana na mamlaka ya bandari na hilo limesaidia sana kupata msaada wa kiufundi na ushauri, pale tunapouhitaji kutoka kwa mamlaka hiyo ambayo ni mmiliki wa eneo zima la bandari," ilifafanua.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa TICTS, Matthew Clifft alisema: "TICTS inazishukuru Mamlaka ya Bandari na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ushirikiano mzuri kutoka kwa serikali ya Tanzania, pia kutoka kwa wadau mbalimbali wa bandari kwa ushirikiano wao pamoja na wafanyakazi wa kampuni kwa kufanya kazi kwa makini," alisema.

TICTS ni kampuni tanzu ya Hutchison Ports Hongkong ya China ikiwa inaendesha bandari 52 katika nchi 26 za Asia, Mashariki ya Kati, Afrika, Ulaya, Amerika Kusini na Australia.

# CCM yawachuja wagombea nafasi nyeti

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) leo kinaanza vikao vyake vya ngazi ya juu kwa ajili ya mchujo cha wanachama walioomba kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama na jumuiya zake.

Jumuiya za chama hicho ni Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) na Jumuiya ya Wazazi.

Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka katika taarifa aliyotoa jana, alibainisha vikao hivyo ni vya kawaida vya uongozi ngazi ya taifa.

"Kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2022 Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (CC) na tarehe 29 Oktoba 2022 Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa (NEC), pamoja na mambo mengine, vikao hivi vitakuwa na kazi ya kupokea mapendekezo, kujadili, kupitisha na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama walioomba uongozi katika ngazi ya mikoa na taifa kwa upande wa jumuiya pamoja na chama," alisema.

Shaka alisema vikao hivyo pia vimetanguliwa na kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kilichofanyika Oktoba 24 na 25 jijini Dodoma.

Taarifa ya Katibu wa NEC Organaizesheni, Dk. Maudline Castico kwa Makatibu Wakuu wa Jumuiya na Makatibu wa CCM Mikoa iliyotolewa Oktoba 10, mwaka huu, ilibainisha nafasi hizo ni wenyeviti wa jumuiya za CCM ngazi ya taifa, Makamu Wenyeviti na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa wanaotokana na jumuiya za CCM.

Pia wenyeviti wa jumuiya za CCM ngazi ya mkoa, wajumbe wa Baraza Kuu la kila Jumuiya ya CCM, ngazi ya taifa na wanachama wanaoomba nafasi za uongozi za jumuiya zisizokuwa za uwakilishi katika vikao vya CCM.

Ratiba inaonyesha kuanzia Oktoba 24 hadi Novemba 2, mwaka huu, vitafanyika vikao vya ngazi ya taifa kwa ajili ya kuchambua, kupendekeza na kuteua majina ya wagombea watakaowania nafasi hizo.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA MBAO NA PLYWOOD**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-00010**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ugavi na Ujenzi wa Gati na Kituo Kupakia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Kampuni zenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Ugavi wa Mbao na Plywood.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa kilomita 2 kutoka ufukweni kutika eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Kutoa mbao na plywoods za vipimo tofauti.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Wafanyakazi waliohitimu na kufanya shughuli za kuthibitisha ubora / kudhibiti ubora (QA/QC)
- Muda wa udhamana (Warranty Period) wa miezi 24 na miaka 5 ya kasoro fiche (Latent Defects) baada ya kumalizika kwa muda wa udhamana;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa kusimaia kandarasi husika.
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi / rekodi husika inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma sawa kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linaloshabihiana,
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipango ya Afya na Usalama eneo la Kazi na vyeti vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) au vyeti sawa;
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Hati zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **11 novemba 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

21719801

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UGAVI WA VIFAA VYA AFYA, MAZINGIRA NA USALAMA ENEO LA KAZI (HSE) PAMOJA NA VIFAA KINGA BINAFSI (PPE)**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0009**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni wataalamu wenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Ugavi wa Vifaa vya Afya, Mazingira na Usalama Eneo la Kazi (HSE) pamoja na Vifaa Kinga Binafsi (PPE)**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Vifaa vya Afya, Mazingira na Usalama Eneo la Kazi (HSE) pamoja na Vifaa Kinga Binafsi PPE)

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Wafanyakazi waliohitimu Kuthibitisha Ubora na Kudhibiti Ubora (QA/QC);
- Muda wa dhamana (Warranty Period) wa miezi 24 na miaka 5 ya kasoro fiche (Latent Defects) baada ya kumalizika kwa muda wa dhamana;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi / rekodi ya kufuatilia inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa,
- Alama za ubora za CE, EN kiwango na vyeti
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi umekataliwa sana .

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Upeo wa Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **11 Novemba 2022, Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka** : Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

21719801

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UGAVI WA BIDHAA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0008**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni wataalamu wenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Ugavi wa Bidhaa kwa matumizi ya kawaida**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Spesa za Plastiki kwa ajili ya zege,
- Nyavu za chuma na mihimili au nguzo,
- Sealant za zege na maungio ya zege,
- Dawa za kuchanganyia zege,
- Geotextile,
- Karatasi ya polyethilini ,
- Release oil,
- Thermocoupler,

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Wafanyakazi waliohitimu na Kuthibitisha Ubora / Kudhibiti Ubora;
- Muda wa dhamana (warranty Period) wa miezi 24 na miaka 5 juu ya kasoro fiche (Latent Defects) baada ya kumalizika kwa muda wa dhamana;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi / rekodi ya kufuatilia inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linaloshabihiana,
- Sera ua Ubora ya Kampuni na mipango ya Afya, mazingira na Usalama eneo la Kazi na vyeti vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) au vyeti sawa ;
- Alama ya Ubora ya CE na Hati / vyeti vyote vya ubora wa vifaa;
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Upeo wa Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & Hati zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **11 Novemba 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

21719801

RIPOTI MAALUM -2

# Simulizi wanawake wa Longido waliogeukia mkaa kuikabili njaa

## ■Wachemsha magome ya miti kupata chai

Na Elizabeth Zaya, LONGIDO

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na ushuhuda wa madhila yanayoikumba jamii ya wafugaji wilayani Longido kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi, wanawake na watoto wakiathiriwa zaidi. Endelea kupata undani wa kinachojiri.**



Sehemu inayotumiwa kuchomea mkaa.

### MAGOME YA MITI

MKAZI wa Kijiji cha Longaiki, Marya Oreteiti anasema wakati mwingine wanapokosa kabisa chakula, hulazimika kutumia magome ya miti kama majani ya chai na kuchemsha chai ya rangi na kuwapatia watoto wanywe ili kufanikisha alichokiita kupasha tumbo.

"Yaani tunatumia kila njia kunusuru watoto, ukikosa hata uji inakubidi utafute magome uyatumie kama majani ya chai, unachemsha na kuwapatia watoto wanywe. Kama una sukari unashukuru na kama huna unawapatia hivyo hivyo, mradi wapashe tumbo," anasema.

Katika hili, Kiongozi wa Mila wilayani Longido, Mutel Laizer, anaiomba serikali kuangalia upya utaratibu wa kuuza chakula wilayani hapo.

"Kama serikali imeleta chakula kwa ajili ya kumsaidia mwananchi, tunaiomba iruhusu mtu anunue hata kama ni kilo moja ya mahindi. Na ikiwezekana iangalie zile familia zenye njaa zaidi izipatie chakula bila malipo halafu hizi zenye angalau fedha kidogo waziuzie kwa bei ya chini zaidi, hii ndio itasaidia kunusuru hali iliyopo sasa.

"Tunachojivunia ni kwamba pamoja na baa hili la njaa kwenye familia nyingi, wanafunzi hawajaathirika sana kwa sababu wenyewe wanapata uji shuleni. Kwa hiyo, wengi wanaona ni bora waende shuleni kwa sababu wanapata chochote kitu cha kuweka tumboni," anafafanua.

Katibu Mkuu wa Viongozi wa Wamaasai Tanzania, Amani Lukumai, anatoa rai kwa mashirika na taasisi mbalimbali kujitokeza kusaidia maeneo hayo yaliyokumbwa na baa la njaa.

"Familia nyingi kuupata mlo mmoja ni muujiza kwao, hata ukipatikana ni kama unawaonjesha watoto, mlo mkubwa unaopatikana angalau ni uji.

"Tunaomba taasisi na wadau mbalimbali wenye moyo, wanyooshe mkono wao watusaidie chakula huku na Mungu atawabariki. Serikali pia iangalie uwezekano wa kupunguza zaidi hiyo bei ya chakula, tunajua inauza bei ya chini kidogo kulinganisha na wafanyabiashara, lakini tunaendelea kuomba ipunguze tena na iruhusu wananchi wanunue hata kilo moja," anawasilisha hoja yake.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Longido, Genofefa Jumanne, anakiri ugumu wa kupata chakula kwa kaya nyingi katika eneo lake la kazi kutokana na ukame uliosababisha hali ngumu kiuchumi.

"Kama ambavyo umejionea, kaya nyingi zimekumbwa na njaa, wanawake ndio wamebeba mzigo mkubwa kulea familia kwa sababu waume zao wamekwenda mbali kuhangaikia mifugo yao. Kwa hiyo, kila kitu kwa sasa ni juu ya kinamama katika eneo letu hili," anasema.

Ofisa Mtendaji huyo pia anakiri kaya nyingi zimeshindwa kumudu kununua chakula kinachouzwa na serikali kutokana na masharti ya kutakiwa kununua kuanzia gunia moja.

"Tunaishukuru sana serikali imetuletea chakula, lakini utaratibu wa kutakiwa kununua kuanzia gunia moja la kilo 80 au kilo 50 ni kikwazo, kaya nyingi zimeshindwa kununua kwani hazina fedha," anasema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Longido, Lunda Kapande, anasema kata hiyo imeathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na ukame na kwa muda mrefu mvua haijanyesha katika eneo hilo.

"Kwa sasa mahindi hapa yanauzwa Sh. 22,000 kwa debe moja katika maduka ya wafanyabiashara. Kilio cha wananchi wengi ni kuomba bei ya chakula hiki kinacholetwa na serikali iendelee kupunguzwa, ili kuwasaidia wale ambao wanashindwa kumudu kabisa bei hii ya sasa," anasema Kapande na kubainisha kuwa kata hiyo imepokea chakula cha bei nafuu tani 15 kutoka serikalini.

Ofisa Mtendaji huyo pia anafafanua utaratibu wa kutoa chakula hicho kwa wananchi, akitamka: "Ni lazima wajiandikishe na kulipia fedha halafu wanasubiri ndani ya siku moja au mbili chakula kinaletwa."KAULI YA DED

Nestory Dakaro, Ofisa Mifugo Wilaya ya Monduli, akitoa ufafanuzi kwa Nipashe kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, anasema hali ya njaa Longido ni mbaya na ndio maana serikali imepeleka chakula hicho cha bei nafuu.

Kuhusu masharti kwa wananchi kutakiwa kununua kuanzia gunia moja, Dakaro anasema ni utaratibu ambao umeelekezwa kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na wananchi wasiomudu kununua huwa wanajichanga kununua kilo hizo kisha wanagawana.

Anabainisha kuwa kiwango cha chakula kilichopokewa katika halmashauri hiyo ni tani 736.3, huku akikiri uhitaji ni mkubwa kuliko kiwango kilichopokewa.

Kuhusu wanawake kuchoma mkaa, Dakaro anasema wananchi wanafanya shughuli hiyo bila kibali na wamekuwa wakiingia kwenye shida na maofisa wa serikali kwa kuwa halmashauri inakataza uchomaji mkaa kwa kuwa unaathiri mazingira.

Ofisa Mifugo huyo anasema hali ya mazingira wilayani hapa ni mbaya kwa kuwa uoto wa asili umepotea kutokana na ukame ulioikumba Longido kwa miaka mitatu mfululizo na kusababisha vyanzo vya maji kukauka.

"Upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani sio tatizo kubwa huku kwa sababu yapo yanayotiririka kutoka Mto Simba," anafafanua.

### MKAKATI NFRA

Mkurugenzi wa NFRA, Milton Lupa anasema mpaka sasa wamegawa chakula katika mikoa ambayo imekuwa na mfumuko mkubwa wa bei ya chakula, ili kupunguza makali huku ikimaarisha akiba zaidi ya chakula kutoka tani 58,000 hadi kufikia tani 110,000 kwa mwaka 2021/22 na ununuzi wa chakula kwa mwaka 2022/23 unaendelea.

Anasema tayari timu zimetawanyika kupeleka mahindi ya bei nafuu katika maeneo yenye uhitaji na bei zao zinaanzia Sh. 1,000 hadi 1,600 kwa kilo.

Abainisha kuwa halmashauri zilizopelekewa chakula ni Longido, Sengerema, Geita, Nzega, Liwale, Nachingwea, Loliondo na Monduli, zaidi ya tani 3,000 zikipelekwa katika maeneo hayo.

"Tunaendelea na kazi hiyo ya kusambaza na kuna maeneo mengine tena ambayo tumeletewa yenye uhitaji wa haraka wa chakula, tunafanya tathmini na tunatarajia ikikamilika tutapeleka chakula huko. Wakala una chakula cha kutosha, hivyo wananchi wasiwe na wasiwasi," Lupa anatamba.

### ANGALIZO LA TMA

Septemba mwaka jana, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitoa taarifa kuhusu kuwapo ukame na joto kali nchini kutokana na mvua za vuli (Oktoba hadi Novemba) kuwa chini ya wastani, Mkoa wa Arusha ukiwa miongoni mwa iliyotarajiwa kukumbwa na hali hiyo.

Vilevile, Aprili mwaka huu, TMA ilitoa taarifa nyingine ya kuendelea kuwapo upungufu wa mvua hizo za vuli kati ya Oktoba hadi Desemba mwaka huu, ikitahadharisha kuwa hali hiyo itapunguza unyevunyevu katika udongo, hivyo kusababisha athari mbalimbali, ikiwamo vipindi virefu vya ukame.

Ni athari ambazo Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, anaitaja imetokana na mabadiliko ya tabianchi na kadhia ya ukataji miti katika maeneo mengi nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akiwa katika kikao cha wadau wa mazingira kilichofanyika Oktoba 3, mwaka huu, alisema serikali imepanga kutumia dola za Marekani bilioni 19.2 kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.09.2022

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Sep-22 | Robo Mwaka ya 31/06/2022 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,864 | 4,416 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,425 | 8,455 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 34,437 | 38,063 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 48,690 | 7,962 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 0 | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | 12,145 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 70,953 | 73,915 |
| 12 | Mali Nyingine | 10,385 | 30,379 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,299 | 2,483 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **181,052** | **177,817** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 26,923 | 34,756 |
| 18 | Amana za Wateja | 113,857 | 103,858 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 4,517 | 4,121 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 20 | 20 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,666 | 1,401 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 3,332 | 4,012 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,859 | 4,029 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **154,174** | **152,197** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **26,878** | **25,620** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (36,526) | (36,526) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,880 | 1,622 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **26,878** | **25,620** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 709,786 | 960,602 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,744 | 6,102 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 572 | 493 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15% | 14% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4% | 4% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 60% | 69% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39% | 42% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 58% | 70% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 10% | -12% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2% | 3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-22 | Robo ya Mwaka linganishi 31/06/2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,208 | 3,592 | 10,368 | 9,056 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,059) | (1,157) | (3,279) | (3,027) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,149** | **2,435** | **7,089** | **6,029** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **3,302** | **2,806** | **8,626** | **9,242** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 507 | 450 | 1,372 | 981 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 2,787 | 2,350 | 7,217 | 8,147 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 7 | 6 | 37 | 113 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(4,027)** | **(4,205)** | **(12,519)** | **(10,912)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,918) | (1,792) | (5,679) | (4,975) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (452) | (383) | (1,227) | (987) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,657) | (2,030) | (5,613) | (4,951) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,423** | **1,036** | **3,196** | **4,359** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (166) | (113) | 457 | (175) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,258** | **923** | **3,653** | **4,184** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,258** | **923** | **3,653** | **4,184** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 128 | 127 | 128 | 124 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 200 | 147 | 458 | 666 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 7 | 7 | 7 | 7 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.80% | 2.10% | 2.14% | 2.37% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 19.17% | 14.53% | 14.63% | 15.28% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 61.86% | 65.73% | 65.91% | 59.64% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.49% | 8.24% | 8.24% | 4.60% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Sep-22 | Robo ya Mwaka linganishi 31/06/2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **1,258** | **923** | **2,880** | **4,184** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 754 | 384 | 1,138 | 456 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 2,962 | 2,921 | 5,883 | 5,298 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,562 | 4,382 | 6,944 | (238) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 3,626 | 5,751 | 9,377 | 8,887 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (170) | 1,761 | 1,591 | 167 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 13,294 | (12,311) | 983 | (713) |
| - Kodi Iliyolipwa | (37) | - | (37) | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **24,248** | **3,811** | **28,758** | **18,041** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (149) | (1,869) | (2,017) | (372) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(149)** | **(1,869)** | **(2,017)** | **(372)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Taslimu | **24,099** | **1,942** | **24,099** | **14,033** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 49,627 | 47,685 | 49,627 | 104,214 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **73,726** | **49,627** | **73,726** | **118,247** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (36,039) | 487 | (487) | - | 24,485 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 2,880 | - | - | - | 2,880 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(33,159)** | **487** | **(487)** | **-** | **27,365** |
| **Mwaka uliopita 2021** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,015 | - | - | - | 1,015 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | 487 | - | - | 487 |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | (487) | - | (487) |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(36,039)** | **487** | **(487)** | **-** | **24,485** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | Gbenga Makinde **Mkurugenzi Mtendaji** | Imesainiwa | 26th October 2022 |
| 3 | Benson Msangi **Afisa Mkuu wa Fedha** | Imesainiwa | 26th October 2022 |
| | Joseph Ringa **Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | Imesainiwa | 26th October 2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | Amb.Tuvako Manongi **Mwenyekiti wa Bodi** | Imesainiwa | 26th October 2022 |
| | Ebele Ogbue **Mkurugenzi** | Imesainiwa | 26th October 2022 |





217119202

United bank of Africa (T) Ltds is a subsidiary of United Bank of Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa, USA, Europe & UAE.

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana
- Benin
- Burkina Faso
- Cote D'Ivore (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

**United Arab Emirates**
- Dubai

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa TMA uzingatiwe

**KATIKA** taarifa yake iliyotoka juzi, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema kutakuwa na upungufu wa mvua nchini na kutaka watu kuchukua tahadhari mapema.

Mvua za vuli zilizotarajiwa kuanza kunyesha kwa mujibu wa utabiri zitakuwa na uhaba kwenye mikoa 14.

Mikoa hiyo imetajwa kuwa ni Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa, Njombe, Katavi, Dodoma, Tabora, Mtwara, Lindi, Songwe na Kigoma huku maeneo ya Kusini mwa Mkoa wa Morogoro inatarajiwa kupata mvua chache katika kipindi cha msimu huu kitakachoanza Novemba na kumalizika Aprili, mwakani.

Taarifa hiyo iliyotolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri wa Mamlaka hiyo, Dk. Hamza Kabelwa, inatoa tahadhari ya kukosekana kwa mvua hizo ambayo italeta athari katika sekta mbalimbali zikiwamo za kilimo, mifugo na nishati.

Athari za kukosekana kwa mvua zimeshaanza kujitokeza katika maeneo mengi nchini, hivi sasa mgawo wa maji umeanza katika baadhi ya mikoa na sehemu nyingine umeme kukatika mara kwa mara.

Taarifa hiyo ya mkurugenzi imefafanua upungufu huo wa mvua utasababisha kuathiri ukuaji wa mazao na chakula kupungua.

Upungufu huo hauathiri sekta ya kilimo pekee, bali pia kwenye sekta ya nishati ambako mabwawa na mito itapungua maji na kuathiri uzalishaji.

Viumbe pia vitaathirika ikiwamo mifugo ambayo inategemea majani kama chakula na maji kutokana na ukame.

Ukame husababisha hata kutokea kwa migogoro kati ya wafugaji na wakulima katika matumizi ya maji, lakini migogoro ya wanyama na binadamu inaweza kutokea wakati wa kutafuta maji.

Mamlaka hiyo imeshauri watu kuzingatia uvunaji na utunzaji wa maji ili kukabiliana na tatizo hilo.

Pia mamlaka hiyo imesema nusu ya kwanza ya msimu huu kuanzia Novemba 2022 mpaka Januari 2023 kunatarajiwa vipindi virefu vya ukavu lakini kunatarajiwa nusu ya pili ya msimu ambao ni kuanzia mwezi Februari mpaka Aprili 2023 kuwapo ongezeko la mvua zitakazoisha wiki ya nne ya mwezi Aprili.

Mamlaka imefafanua katika kipindi cha Novemba na Desemba upungufu mkubwa wa unyevunyevu kwenye udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi ya mikoa hiyo.

"TMA tunashauri sekta husika kutoa elimu kwa wakulima kulima mazao yanayohimili mvua ndogo na utunzaji wa chakula."

Katika maeneo mengi ya mikoa hiyo 14, mvua zitaanza wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba.

Tahadhari hiyo ilitolewa na TMA lazima ichukuliwe kwa umuhimu ili nchi iweze kuepuka janga la njaa kwa kukosa chakula cha kutosha.

Athari za mabadiliko ya tabianchi zimekumba mataifa mengi duniani na tumeshuhudia jinsi watu wanavyohangaika kwa kukosa chakula na maji. Hata mifugo imeathirika na kufa kwa kukosa malisho na maji.

Nchi yetu imejaliwa kuwa na mito, maziwa yenye maji mengi ambayo kama wataalamu watawezesha kutumika kwa matumizi ya nyumbani na umwagiliaji mashamba kutaokoa janga hili linalotaka kutupata.

Ni muhimu pia kumuomba Mwenyezi Mungu, atuepushe na janga hili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Vyoo vichafu sokoni chanzo cha magonjwa

Na Adam Fungamwango

**UKIPATA** bahati ya kuingia kwenye vyoo katika vituo cha mabasi ya daladala na hata vya kusafiri mikoani na nje ya nchi, halafu ukaenda kuingia kwenye vyoo vya masoko utakutana na vitu viwili tofauti.

Cha ajabu ni kwamba vyoo hivyo vyote vinamilikiwa na Manispaa. Yenyewe hutoa tenda kwa kampuni za usafi kwa ajili ya kutunza na kusafisha.

Hata hivyo, utakachokiona kwenye vyoo vya masoko mengi nchini, si kile utakachokiona kwenye vyoo vya kwenye vituo vya mabasi.

Tukianza kwenye vituo vya mabasi, kwanza utakuta hata viwango vya utengenezaji ni tofauti. Ukiingia mara nyingi ni visafi na eneo karibuni lote ni kavu.

Utakutana na maji yakitiririka kwenye mabomba na hata kama siku hiyo hakuna maji utaona majaba yakiwa yamejazwa maji.

Ukiingia unapokewa na harufu ya dawa za kusafisha vyoo si harufu zisizoeleweka, ili mradi tu hata ukitoa pesa yako unaona kabisa kutokana na huduma iliyotolewa pesa zinakwenda kihalali. Unatoka chooni hata kama ulikuwa unataka kwenda hotelini kula chakula, wala hupati shida kwa sababu mtu anakuwa hajachefukwa kutokana na mazingira aliyoyakuta ndani.

Ni kwa sababu mtu anaweza kukutana na mwezake anayefahamiana naye wakasimama na kupiga stori hata dakika mbili tatu humo humo chooni kabla ya kutoka nje.

Shughuli ipo kwenye vyoo vya masoko. Hapa ndipo kwenye matatizo. Vyote vinamilikiwa na Manispaa, lakini huku ni kama vile wanaopewa tenda ya kuvilinda, kuvitunza kuvisafisha na kuviendesha, hawana utaalamu huo, na wanaviendesha kienyeji ili mradi tu.

Vyoo vya masoko mengi nchini ni vichafu na vimekuwa ni vyanzo vya magonjwa mengi ya kuambukiza. Magonjwa ya tumbo, kuhara na kipindupindu ukiangalia mara nyingi huanzia masokoni na hii inatokana na ubora hafifu wa vyoo.

Mara nyingi vyoo vya masoko mara zote utakuta vina unyevunyevu, ambao unatokana na uchafu wenyewe wa choo na hata wanaoviendesha na waliowaweka kusimamia kutojua wakati gani wa kusafisha na wakati gani wa kuwaacha watu wavitumie kwanza.

Usafi siyo kusafisha muda wa watu kuvitumia. Muda huo watumiaji wanatakiwa kuvikuta vyoo vikiwa vikavu, kinachotakiwa ni maelekezo tu kwa watumiaji jinsi ya kutumia kwenye haja kubwa, ndogo na jinsi ya kunawa baada ya kutumia.

Kwenye vyoo vya masoko hata miundombinu yake inakuwa ni tatizo. Unaweza kukuta hata koki zote hazifanyi kazi, badala yake kuna makopo mawili au matatu tu ambayo watu wote wanalazimika kuyatumia kitu ambacho ni hatari sana kiafya.

Sehemu ambayo wanaume wanapanda kwa ajili ya haja ndogo unakuta marumaru zimechoka mpaka zimebadilika rangi.

Pembeni ambako haja ndogo inamwagika, marumaru za ukutani zimebadilika rangi kiasi cha kutia mtu kichefuchefu.

Huko kwenye vyoo vya kinamama ndiyo kabisa, kiasi cha kuwafanya kuwapa magonjwa ya maambukizi ya mkojo au UTI. Unashangaa ni kwa nini vyoo vinakuwa vichafu wakati watu wanalipia?

Watu wote waliokusanyika kwenye soko hilo, ambao ni wafanyabiashara na wateja wao wanalipia huduma na hata wapita njia nao wanatumia, lakini unakuta watu waliopewa dhamana hiyo wanashindwa kufanya vyoo vya masoko kuwa salama kwa afya ya binadamu.

Ninavyojua miundombinu au vifaa vya vyoo havinunuliwi kila siku. Marumaru, koki za maji, taa, fagio, mabomba na vifaa vingine vinavyofanana na hivyo vikishanunuliwa huweza kukaa muda mrefu bila kununua, labda dawa za kuua wadudu na kukata harufu mbaya ndiyo zinawaza kununuliwa labda kila baada ya siku tatu, nne tano au wiki.

Kwa hili nawashauri baadhi ya Mwenyeviti wa Serikali za Mitaa, viongozi wa masoko kubadilisha mitazamo yao na kujali sana usafi wa vyoo kwani ndiko sehemu ambazo watu kutoka sehemu mbalimbali wanakutana.

TANGAZO

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED

KCBL Together, Transforming Lives

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30/09/2022
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| A. | MALI | Robo mwaka kwa sasa 30.09.2022 | Robo mwaka iliyopita 30.06.2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Fedha Taslimu | 30,743 | 37,096 |
| 2 | Salio katika benki kuu ya Tanzania | 309,002 | 346,446 |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 1,625,557 | 2,328,889 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 6,630,890 | 5,327,846 |
| 12 | Mali nyingine | 426,510 | 289,884 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 222,999 | 229,744 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **9,245,701** | **8,559,905** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 4,233,178 | 4,843,541 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | 19,051 | 20,069 |
| 23 | limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | 44,871 | 29,966 |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Fedha za washirika(MIVARF Grant) | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa baadaye | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 231,066 | 230,873 |
| 28 | Madeni | 1,000,000 | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **5,528,166** | **5,124,449** |
| 30 | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **3,717,535** | **3,435,456** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 14,849,819 | 14,623,323 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 40,429 | 41,388 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (11,300,591) | (11,301,550) |
| 34 | Faida(hasara)ya kipindi husika | 127,878 | 72,295 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| 37 | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **3,717,535** | **3,435,456** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | 479,053 | 970,715 |
| 39 | Mikopo chechefu | 155,006 | 177,142 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 65,571 | 65,649 |
| 41 | Jumla ya mikopo ghafi na amana | 6,727,539 | 5,424,453 |
| 42 | Mali nyingine chechefu | | |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 40.21% | 40.13% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 2.30% | 3.27% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 158.92% | 111.99% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 71.72% | 62.24% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 72.25% | 62.89% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -12.60% | -0.69% |
| (vii) | Ongezeko la mali | 8.01% | 2.26% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO INAYOISHIA 30/09/2022
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 30/09/2022 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2022 | Limbikizo la mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato yariba | 241,616 | 148,144 | 665,297 | 390,131 |
| 2 | Gharama za riba | 23,733 | 12,500 | 59,424 | 38,913 |
| 3 | **Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2)** | **217,883** | **135,644** | **605,873** | **351,218** |
| 4 | Madeni viza yaliyopitwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | 78 | 17,918 | 9,160 | 17,918 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya riba** | **110,852** | **74,091** | **253,909** | **217,047** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | | - | | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 27,369 | 33,547 | 81,474 | 114,452 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | 83,483 | 40,544 | 172,435 | 102,595 |
| 7 | **Gharama zisizo na riba** | **273,204** | **245,018** | **741,064** | **568,341** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 130,409 | 123,420 | 380,580 | 309,838 |
| | 7.2 Ada na kamishani | 1,553 | 12,179 | 2,189 | 12,179 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 141,242 | 109,419 | 358,295 | 246,324 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **55,609** | **(17,365)** | **127,878** | **17,842** |
| 9 | **Tengo la kodi ya mapato** | | **-** | | **5,353** |
| 10 | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **55,609** | **- 17,365** | **127,878** | **12,489** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | | | |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **55,609** | **(17,365)** | **127,878** | **12,489** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 22 | 24 | 22 | 24 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 1.99 | -0.63 | 4.61 | 0.45 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.60% | -0.23% | 1.38% | 0.50% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4.49% | -1.90% | 10.32% | 1.37% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 77.51% | 110.25% | 80.62% | 93.60% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.52% | -2.06% | 5.79% | 1.48% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 30/09/2022

| Robo Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Upunguzaji wa jumla wa matengo | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa** | 14,623,323 | 0 | -11,229,255 | 41,388 | 0 | 0 | 3,435,456 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 127,878 | | | | 127,878 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 226,496 | | (59,717) | | | | 166,779 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | (11,619) | (959) | | | -12,578 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | | | | | 0 |
| Mengineyo | | | | | | | 0 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | **14,849,819** | **-** | **(11,172,713)** | **40,429** | **-** | **-** | **3,717,535** |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | **14,448,518** | **-** | **(11,274,967)** | **29,769** | **-** | **-** | **3,203,320** |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 72,295 | | | | **72,295** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | | | | | | **0** |
| Miamala na wanahisa | 174,805 | | (14,964) | | | | **159,841** |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | **0** |
| Tengo la ziada ya jumla | | | (11,619) | 11,619 | | | **0** |
| Ziada ya kisheria | | | | | | | **0** |
| Mengineyo | | | | | | | **0** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | **14,623,323** | **-** | **(11,229,255)** | **41,388** | **-** | **-** | **3,435,456** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30/09/2022
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka kwa sasa 30.09.2022 | Robo mwaka iliyopita 30.09.2022 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 55,609 | 57,330 |
| | **Marekebisho Kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Badiliko katika mali isiyoshikika | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 6,745 | 6,118 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | (1,303,044) | (380,166) |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika amana | (610,363) | (33,846) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 193 | (33,364) |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | (136,626) | (14,381) |
| | - Kodi iliyolipwa | 14,905 | 9,517 |
| | - Mengineyo(bainisha) | (1,018) | 14,517 |
| | - Maslahi ya wachache | (26) | |
| | - Madeni na benki nyingine | | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji*** | **(1,973,625)** | **(374,275)** |
| II: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji*** | - | - |
| III: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | 226,496 | 174,805 |
| | Gawio lilololipwa kwa fedha taslilmu | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | 1,000,000 | - |
| | Mengnineyo | - | |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha*** | **1,226,496** | **174,805** |
| IV: | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu:** | | |
| | **Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali** | **(747,129)** | **(199,470)** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo ya mwaka.** | **2,712,431** | **2,911,901** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo ya mwaka.** | **1,965,302** | **2,712,431** |

| *JINA NA CHEO* | *SAINI* | *TAREHE* |
|---|---|---|
| CPA. KINYAKI O. KINYAKI<br>**MKUU WA FEDHA NA UTAWALA** | | 27th October 2022 |
| GODFREY J. NG'URAH<br>**MANEJA MKUU** | | 27th October 2022 |
| CPA. APOLINARY S. KITYAMWI<br>**MKUU WA UKAGUZI WA NDANI** | | 27th October 2022 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini ,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu ,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

| *JINA NA CHEO* | *SAINI* | *TAREHE* |
|---|---|---|
| **1. Dr GERVAS M. MACHIMU, MWENYEKITI WA BODI** | | 27/10/2022 |
| **2. CPA. MWAMINI J. MUSSA, MKURUGENZI** | | 27/10/2022 |

## MINIMUM DISLOSURES OF CHARGES AND FEES

| TRANSACTION | DESCRIPTION | 2022 VAT exclusive | 2022 VAT inclusive |
|---|---|---|---|
| **MAINTENANCE FEE: CURRENT ACCOUNT** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Normal Business Current account | Per month | 15,000 | 17,700 |
| Personal Customers | Per month | 15,000 | 17,700 |
| Umoja Account | Per month | 13,000 | 15,340 |
| Jasiri Account | Per month | 5000 | 5,900 |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| Normal Saving Account | Per Month | 2,000 | 2,360 |
| Salary Account | Per Month | 2,000 | 2,360 |
| Msomi Account | Per Month | 1,000 | 1,180 |
| Mtoto Account | Per Month | Free | n/a |
| Mama Afrika Account | Per Month | Free | n/a |
| Mafao Account | Per Month | Free | n/a |
| Wekeza Account | Per Month | Free | n/a |
| Kilimo Tija Account | Per Month | 1,500 | 1,170 |
| **CASH WITHDRAW OVER THE COUNTER** | Per transaction | 2022 VAT exclusive | VAT inclusive |
| **UMOJA ACCOUNT** | Per transaction | 5,000 | 5,900 |
| **All savings account (Except those exempted from charges)** | 1,000 -499,999 | 5,000 | 5,900 |
| | 500,000 - 999,999 | 6,000 | 7,080 |
| | 1,000,000 -2,999,999 | 7,000 | 8,260 |
| | 3,000,000 -4,999,999 | 8,000 | 9,940 |
| | 5,000,000 & above | 0.25% | 0.295% |
| **Current Account** | Below 3,000,000 | 5000 | 5,900 |
| | 3,000,000 - 4,999,999 | 7000 | 8,260 |
| | 5,000,000 – above | 0.2% | 0.236% |
| **ATM** | **BAND** | 2022 VAT exclusive | VAT inclusive |
| KCBL and CRDB ATMs | 5,000-150,000 | 1,300 | 1,534 |
| | 155,000-400,000 | 2000 | 2,360 |
| | 405,000-600,000 | 2500 | 2,950 |
| Other Local Banks ATM's | Per Transaction | 4,000 | 4,720 |
| Other Banks ATM outside the Country | Per Transaction | 6,780 | 8,000.40 |
| Transaction Decline at ATM Outside the country due to PIN Error | Per decline | 1,000 | 1,180 |
| ATM withdrawal (Customer of other Banks) | Per transaction | 4,000 | 4,720 |

**WAKALA**

| Per Transaction | VAT exclusive | VAT inclusive | Per Transaction | VAT exclusive | VAT inclusive |
|---|---|---|---|---|---|
| <1,999 | 254.00 | 299.72 | 300,000-399,999 | 5,900 | 6,962 |
| 2,000-2,999 | 350.00 | 413 | 400,000-599,000 | 6500 | 7,670 |
| 3,000-4,999 | 400 | 472 | 600,000-999,999 | 7000 | 8,260 |
| 5,000-6,999 | 750 | 885 | 1,000,000-1,999,999 | 7500 | 8,850 |
| 7,000-19,999 | 800 | 944 | 2,000,000-2,999,999 | 8000 | 9,440 |
| 20,000-29,999 | 2650 | 1947 | 3,000,000-3,999,999 | 9000 | 10,620 |
| 30,000-49,999 | 1800 | 2,124 | 4,000,000-6,000,000 | 9900 | 11,682 |
| 50,000 -99,000 | 2550 | 3,009 | 6,000,001-7,999,999 | 11000 | 12,980 |
| 100,000-199,999 | 3,500 | 4,130 | 8,000,000-9,999,999 | 13,000 | 15,340 |
| 200,000-299,999 | 4,900 | 5,782 | 10,000,000-19,999,999 | 15,000 | 17,700 |

| TRANSACTION | DESCRIPTION | 2022 VAT exclusive | 2022 VAT inclusive |
|---|---|---|---|
| **CHEQUE BOOK** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Cheque Book order | Per Leaf (Tzs.100 Stamp duty inclusive | 700 | 826 |
| Stop Payment Order | Per cheque | 1.0% of the amount Min. 50,000 Max 300,000 | 1.18% |
| Stop/unblock cheque leaf | Per leaf | 20,000 Max 40,000 | |
| Stop/unblock cheque book | Per cheque book | 50,000 | 59,000 |
| Encashment of third-party cheque without checklist | Per cheque | 5,000 | 5,900 |
| Unpaid cheque for reason "refer to drawer or effects not cleared | Per page | 1% min. 150,000 max 300,000 | |
| "Uncollected cheque Book (After collection notification has been sent to a customer to collect the cheque Book)" | Per cheque book per month | 6,000 | 7,080 |
| **INTERBANK** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Inward cheques for clearance | Per cheque | 1,000 | 1,180 |
| **BANKERS CHEQUE** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Sale of Bankers Cheque | Per leaf | 30,000 | 35,400 |
| Cancellation/Repurchase | Per leaf | 25,000 | 29,500 |
| **TRANSACTION** | **DESCRIPTION** | VAT exclusive | VAT inclusive |
| **BALANCE ENQUIRY** | | | |
| Over the Counter (OTC) | Per Enquiry | 1000 | 1,180 |
| At our ATM- KCBL Customer | Per Enquiry | 350 | 413 |
| Other Local Bank Customers | Per Enquiry | 1,000 | 1,180 |
| At the other banks ATMs within the country | Per Enquiry | 500 | 590 |
| At other Banks ATMs Outside the Country | Per Enquiry | 1,000 | 1,180 |
| Kili Mobile | Per Enquiry | 500 | 590 |
| At CRDB Wakala | Per Enquiry | 500 | 590 |
| **BREAKING OF ACCOUNT CONTRACTS** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Uplifting of Fixed Deposit(FDR) | Per transaction | 50% of interest paid" | 50% of interest paid"+18% |
| Uplifting of Mama Afrika Account | Per transaction | 50% of interest paid min 10,000 | 50% of interest paid"+18% |
| Uplifting of Wekeza Account | Per transaction | 50% of interest paid" | 50% of interest paid"+18% |
| Mtoto Account Cash withdrawal exceeding 4th transaction per annum | Per transaction | 12,000 | 14,160 |
| **ACTIVATION OF DORMANT ACCOUNT** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| CURRENT ACCOUNT | Per activation | 20,000 | 23,600 |
| Savings Account except Mtoto A/c | Per activation | Free | n/a |
| Accrued Monthly/Maintenance Fee on dormant accounts with zero balance | Per activation | Free | n/a |
| **CLOSING ACCOUNT** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Current Account | Per account | 23,000 | 27,140 |
| Savings Account | Per account | 10,000 | 11,800 |
| **FUND TRANSFER** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Between KCBL Customers | | | |
| Over the counter | Own account | Free | n/a |
| Mobile banking | 3rd party account | 2,000 | 2,360 |
| Mobile banking | Transfer to MNOs (Mpesa, TigoPesa, Airtel Money and Halopesa) | | |
| | 5,000-10,000 | 1,500 | 1,770 |
| | 10,001-30,000 | 2,600 | 3,068 |
| | 30,001-100,000 | 3,500 | 4,130 |
| | 100,001-200,000 | 4,500 | 5,310 |
| | 200,001-500,000 | 4,600 | 5,428 |
| | 500,001-1,000,000 | 6,000 | 7,080 |
| | Per Transaction | 1% | 1.18% |

| | | 2022 VAT exclusive | 2022 VAT inclusive |
|---|---|---|---|
| **INTER BANK (OUTWARD FUND TRANSFER** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| TISS | Per Transaction | 10,000 | 11,800 |
| EFT | Per Transaction | 10,000 | 11,800 |
| **INTER BANK (INWARD TRANSFER)** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| TISS | Per transaction | Free | |
| EFT | Per transaction | 4,000 | 4,720 |
| **INTERNATIONAL/FOREIGN FUNDS TRANSFER** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Within East Africa Community Countries (TISS) | Per Transaction | 10,000 | 11,800 |
| Outward transfers to other countries | Per Transaction | Equiv. USD 50 | Equiv. USD 59 |
| Inward Foreign Funds transfer | Per Transaction | 5,000 | 5,900 |
| **KCBL VISA CARD** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| VISA card | Per card | free | |
| Annual Card fee | Per card | 15,000 | 17,700 |
| **RENEWAL OF CARD ON EXPIRY** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| VISA card | Per card | 10,000 | 11,800 |
| **REPLACEMENT OF CARD** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| VISA card | Per card | 15,000 | 17,700 |
| PIN creation | Per creation | 3,500 | 4,130 |
| **ACCOUNT STATEMENTS** | **DESCRIPTION** | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Mini statement over the counter (10 transactions) | Per Statement | 3,000 | 3,540 |
| Monthly statement for current Account | Per Page | 1,500 | 1,770 |
| All statement-All Accounts | | 1,500 | 1,770 |
| **SALARY PAYMENTS** | | | |
| Manual Salary Processing | Per Entry | 3,000 | 3,540 |
| Bulk Salary Processing Automated | Per transaction | 1,500 | 1,770 |
| **CASH COUNTING/DEPOSIT OF SMALL DENOMINATIONS** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| 1,000 Notes | Above 1,000,000 | 0.2% min 2,000 | 0.236% |
| Coins | Above 100,000 | 0.2% min 2,000 | 0.236% |
| **INFORMATION SEARCH** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| For Information Up to 12 Past Months | Per Document | 50,000 | 59,000 |
| For Information of 1 to 5 Past Year | Per Document | 80,000 | 94,400 |
| For Information of Above 5 Past years | Per Document | 100,000 | 118,000 |
| CCTV image retrieve for ATM per transaction | Per Document | 100,000 | 118,000 |
| Loan Processing Fee | Personal loans | 2.1% | 2.48% |
| | Cooperatives | 2.5% | 2.95% |
| | MSME up to 100 Mn | 2.0 % min 200,000 No Max | 2.36% |
| | SME 101mn-1Bn | 2.0% Min 1,000,000 no maxi | 2.36% |
| Lending interest rates | Co-operative Union loans | 17% P.a | |
| | MSME Loans with Traditional Security | 18% P.a | |
| | MSME Loans with Non-Traditional Security | 23% P.a | |
| | Mama Afrika Loans | 14% P.a | |
| | Personal Loan | 15% P.a | |
| | Jasiri Group Loan | 48% P.a | |
| Restructuring fees | MSME | 1% | 1.18% |
| Documents and Legal Charges | Per Document | 100k@, Max 600,000 | 118K@, max 708,000 |
| Loan Take Over by Other Banks | Personal Loan, SME& Co-operatives | 3% of take Over balance | |
| Commitment fees | Unutilized Overdraft amount | 1% | 1.18% |
| **STANDING ORDER** | | | |
| Within KCBL Accounts | Per Transaction | Free | n/a |
| **INTRODUCTION LETTER AND CERTIFICATE OF BALANCE** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Certificate of Balance | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| Status Report | Per Report | 50,000 | 59,000 |
| Visa Recommendation | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| Any other introduction | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| Confirmation of customer's Bank statement requested by other banks (born by Customer) | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| **POSTAGE AND COURIER CHARGES** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Local Postage | Per Item | | |
| International Postage | Per Item | Equivalent USD | |
| IMPORT L/Cs | Opening- Issuance commission | 1% per quarter | 1.18% per quarter |
| | Acceptance | 0.5% PQ | 0.59% |
| | Discrepancy fee | USD 100 | USD 118 |
| | Document Processing Fee | USD 100 | USD 118 |
| Amendments | General Amendments | USD 100 | USD 118 |
| | Extension Validity | 0.25% per Month | 0.295% per month |
| **TIME DEPOSITS** | | VAT exclusive | VAT inclusive |
| Interest on FDR | | 3-5% | 3.54%-5.9% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information. NB:All charges are VAT exclusive.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | CPA. Kinyaki O. Kinyaki | HEAD OF FINANCE AND ADMINISTRATION | | 27th October 2022 |
| 2 | Godfrey J. Ng'urah | GENERAL MANAGER | | 27th October 2022 |
| 3 | CPA. Apolinary S. Kityamwi | HEAD OF INTERNAL AUDIT | | 27th October 2022 |
| | *Name* | | *Signature* | 27th October 2022 |
| 1. | **Dr GERVAS M. MACHIMU,** | CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS | | 27th October 2022 |
| 2. | **CPA. MWAMINI J. MUSSA,** | DIRECTOR | | 27th October 2022 |

217120502

MuCoBa Bank PLC

"Kwa Maendeleo Yako"

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30-09-2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 30/09/2022 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 30/06/2022 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 895 | 462 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 115 | 181 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 2,522 | 2,534 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 15,294 | 15,726 |
| 12 | Mali nyingine | 4,492 | 4,401 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 565 | 532 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **23,884** | **23,837** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 14,716 | 14,940 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 117 | 117 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 152 | 124 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 584 | 680 |
| 28 | Madeni | 3,526 | 3,426 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **19,099** | **19,290** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **4,785** | **4,547** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 8,789 | 8,789 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (4,536) | (4,558) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 425 | 203 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 107 | 113 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| **37** | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **4,785** | **4,547** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,470 | 1,451 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 140 | 160 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 20.03% | 19.08% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 9.61% | 9.90% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 107.99% | 109.25% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 64.04% | 65.97% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 87.20% | 87.69% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.49% | 7.78% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.19% | 9.95% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-09-2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/09/2022 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/06/2022 | Limbikizo lamwaka sasa 30/09/2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/09/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 829 | 1,020 | 2,358 | 3,075 |
| 2 | Gharama za Riba | (185) | (200) | (508) | (661) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 644 | **819** | 1,850 | 6 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 20 | (53) | (193) | (235) |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 250 | 224 | 706 | 610 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 250 | **180** | 688 | 553 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | 45 | 19 | 57 |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | (672) | **(687)** | (1,939) | (2,120) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (371) | (352) | (1,083) | (1,026) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (35) | (53) | (98) | (156) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (266) | (283) | (758) | (938) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | 222 | 304 | 425 | 668 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (30) | (30) | (60) | (90) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | 192 | 274 | 365 | 578 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | 192 | **274** | 365 | 578 |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 50 | 56 | 49 | 60 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 5.88 | 8.39 | 11 | 18 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 0.93% | 1.34% | 1.78% | 2.95% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 4.76% | 7.28% | 2.28% | 2.95% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 62.27% | 55.25% | 63.27% | 16.02% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 3.41% | 4.53% | 4.50% | 57.55% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30-09-2022

(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,345** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | **-** | **425** | **-** | **425** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | **-** | **21** | **-** | **21** |
| Miamala na Wanahisa | **(6)** | **-** | **-** | **(6)** |
| Gawio lililolipwa | **-** | **-** | **-** | **-** |
| Ziada ya Kisheria | **-** | **-** | **-** | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | **-** | **-** | **-** | **-** |
| Mengineyo | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(4,111)** | **107** | **4,785** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2021** | 8,886 | (5,280) | 87 | 3,693 |
| Salio la mwanzo wa mwaka | - | 743 | - | 743 |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | (91) | - | - | (91) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | (20) | 20 | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,345** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-09-2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/09/2022 | Robo ya Mwaka iliyopita 30/06/2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/09/2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/09/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 222 | 386 | 425 | 578 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | - |
| | Hasara Katika Mali | 70 | 39 | 374 | 534 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | 432 | (1,042) | (475) | (1,722) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (224) | 1,087 | (1,574) | (605) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (68) | (316) | (271) | (237) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (91) | (312) | 46 | (288) |
| | Kodi Iliyolipwa | (30) | (30) | (90) | (60) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **311** | **(188)** | **(1,565)** | **(1,800)** |
| | | | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (32) | (4) | (41) | (35) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(32)** | **(4)** | **(41)** | **(35)** |
| | | | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (100) | - | (200) | (100) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | 177 | 1,000 | 1,197 | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **77** | **1,000** | **997** | **(100)** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 356 | 807 | (609) | (1,935) |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 3,177 | 2,369 | 4,142 | 4,714 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **3,533** | **3,177** | **3,533** | **2,779** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

Jina Na Cheo Saini Tarehe

Philip Raymond .................................. (Imesainiwa) 28/Oct/2022
Meneja Mkuu

Kelvin Mushi ..................................... (Imesainiwa) 28/Oct/2022
Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala

Saleh S. Abdallah................................. (Imesainiwa) 28/Oct/2022
Mkaguzi Mkuu wa Ndani

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi

Jina Tarehe

1. Arafat A. Ally...................... (Imesainiwa) 28/Oct/2022
Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi

2. Bakar R. Bakar ...................... (Imesainiwa) 28/Oct/2022
Mkurugenzi

## DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2015

## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

### MUCOBA BANK PLC- REVISED CHARGES AND FEES- SEPTEMBER 2021

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 2,000 |
| Credit Interest Rate | 1% pa |
| | |
| **Group Savings Account (GS09)** | |
| Account opening minimum amount | Free |
| Minimum operating balance | Free |
| Minimum Interest-Bearing balance | N/A |
| Cash Withdrawal Fee | Refer cash withdrawal fee below |
| Credit Interest Rate | N/A |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 2,000 |
| Credit Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 10,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 2,000 |
| Interest Rate | |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 1%pa |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest-Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |
| Prematurity withdrawals | 10,000 |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | Rate |
|---|---|
| 3 months | 4% |
| 6 months | 5% |
| 12months | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs**10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 3,000 |
| Cash withdrawal- from Tzs 5,000,000 and above) | 3,000+0.12%, Max Tzs 150,000 |
| Account closure | 10,000 |
| Dormant account reactivation | 5,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,500 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Bank Statement Fee /page | 2,000 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | 15,000 |
| TT Outward local- EFT | 15,000 + Levy |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Inward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balance Inquiry:<br>*Mobile banking<br>*Over the counter<br>*ATM | <br>200<br>500<br>400 |
| Money Transfer | 15,000 |
| ATM card | 15,000 |
| Searching Fee | 10,000 |
| Coins deposit fee | 10% |
| ATM card replacement | 10,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,500 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,500 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alert | 500 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |
| ATM Balance Inquiry | 400 |
| Annual card maintenance fee | 5,000 |
| PIN re-issue | 1,000 |
| Card replacement fee | 15,000 |
| Monthly fee | 2,000 |
| Standing Order | 10,000 |

**LOAN CHARGES AND COMMISION**

| S/NO | LOAN PRODUCTS | CHARGIES |
|---|---|---|
| 1. | 1.Business loan<br>2.Mixed loan<br>3.Agriculture loan<br>4.Housing loan<br>5.Assets acquisition loan | -Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 20,000/=<br>-Delay fines 0.1<br>-Interest rate<br>A. 1-6 Months 13% pa<br>B. 7-12 Months 18% pa<br>C. Above 12Months 20% pa |
| 2. | 1.Group loans | -Application fee 1%<br>-Interest rate 25% pa |
| 3. | 1.Salary loan full guarantee- Government | - Indemnity fund 3% of the approved amount.<br>-Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 10,000/=<br>-Interest rate 13% pa |
| 4. | 1.Salary loan full guarantee- Private sector | - Indemnity fund 3% of the approved amount.<br>-Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 10,000/=<br>-Interest rate 14% pa |
| 5. | 1.MUCOBA staff loan | - Indemnity fund 3% of the approved amount.<br>-Interest rate 5% pa |

HABARI KITAIFA

## TMA yatoa hadhari upungufu wa mvua

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) kutoa tafadhari ya kuwapo kwa upungufu wa mvua kwa mikoa 14 inayopata mvua mara moja kwa mwaka, uongozi wa Mkoa wa Ruvuma umewatoa hofu wananchi kuhusu upungufu wa chakula.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Tawala wa mkoa huo, Mashauri Ndaki, alisema pamoja na tishio la mvua chache, mkoa wake una akiba kubwa ya chakula.

Alisema watakutana na kamati yake ya maafa ya mkoa kuangalia athari nyingine zitakazotokana na kupungua kwa mvua kunakotarajiwa, lakini si suala la chakula.

"Sijapata rasmi taarifa ya TMA, lakini kwa kuwa nyie wanahabari mpo karibu zaidi niseme nitakutana na kamati kuangalia athari zinazoweza kutokea lakini nina uhakika sio suala la chakula, mkoa wa Ruvuma kwa mwaka wa kumi sasa tumeongoza kwa kuzalisha chakula kwa wingi kinachotumika hapa nchini," alisema Ndaki.

Akitoa utabiri wa msimu kwa mikoa hiyo 14 inayopata mvua mara moja kwa mwaka kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk Agnes's Kijazi, Mkurugenzi wa huduma za utabiri wa Mamlaka hiyo, Dk. Hamza Kabelwa, alitaja mikoa hiyo kuwa ni Ruvuma, Mbeya, Rukwa, Njombe, Iringa, Lindi, Mtwara, Songwe, Katavi, Kigoma, Singida, Tabora, Dodoma pamoja na baadhi ya maeneo ya Kusini mwa mkoa wa Morogoro.

"Katika nusu ya kwanza ya msimu huu mwezi Novemba 2022 mpaka Januari 2023 tunatarajia vipindi virefu vya ukavu, lakini tunatarajia nusu ya pili ya msimu ambayo ni mwezi Februari mpaka Aprili 2023 kutakuwa na ongezeko la mvua hizo zitakazoisha wiki ya nne ya mwezi Aprili," alisema Dk. Kabelwa.

Pia, alisema katika kipindi cha Novemba na Desemba upungufu mkubwa wa unyevunyevu kwenye udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi na kuathiri shughuli za kilimo.

Alisema TMA inashauri sekta husika kutoa elimu kwa wakulima kulima mazao yanayohimili mvua ndogo.

"Pia, tunatarajia kina cha maji kwenye mito na mabwawa kitapungua na kuathiri upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali, hali hii inaweza kuathiri pia sekta ya ufugaji na kuleta migogoro ya wafugaji na wakulima na wanyama na binadamu katika kuchangia maji, kwa hapa Mamlaka zinashauriwa kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa pamoja na kuweka miundombinu ya uvunaji wa maji sambamba na kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kuhimiza kilimo himilivu," alisema Dk Kabelwa.

Alisema katika maeneo mengi ya mikoa hiyo 14, mvua zitaanza wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba.

"Pamoja na kutabiri vipindi virefu vya mvua chache, bado kuna uwezekano wa kuwapo kwa vipindi vifupi vya mvua kubwa, wananchi wachukue tahadhari," alisema Dk. Kabelwa.

Utabiri huo wa TMA umeonesha sekta ya usafiri wa ardhini, majini na anga itanufaika kutokana na vipindi vya ukavu vinavyoweza kujitokeza.

# Shughuli za kibinadamu zilivyoharibu mito minne

**Na Christina Haule,** MOROGORO

BODI ya Maji ya Bonde la Wami Ruvu imesema shughuli za kibindamu zimesababisha mito minne mkoani Morogoro kujaa udongo na mchanga, hali iliyosababisha gharama kubwa kwenye kuchimba.

Pia imewataka wananchi kulinda vyanzo vya maji kwa kuepusha visijae tope, hali itakayosababisha kutumika fedha nyingi kuchimba badala ya kuelekeza fedha hizo kwenye miradi mingine ya maendeleo.

Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Elibariki Mmassy, alisema hayo juzi kwenye kikao cha wadau wa maji wakiwamo wa umwagiliaji, viwanda na wavuvi kilichofanyika mjini hapo.

Alisema gharama za uchimbuaji upya kuondoa mchanga na udongo huo kwa kilometa moja pekee ni zaidi ya Sh. milioni 20.

Aliitaja mito hiyo kuwa ni Mngazi, Mlali, Mpiji na Mgeta ambayo inasafishwa kwa awamu, ili kuipa uwezo wa kuhifadhi maji ambayo yatasaidia kukabiliana na kero kama ya ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mmassy aliwataka watumiaji maji wakiwamo wavuvi, wachimbaji madini na wakulima kuacha tabia ya kuzuia maji kwenye eneo moja bila kujali watumiaji wengine.

"Watu wanazuia maji ili wavue samaki au wachimbe madini, wengine wanalima wote hao kwa pamoja wanaharibu vyanzo hivyo, wanatia tope zinazopunguza kina cha vyanzo vya maji na sio sahihi," alisema Mmassy.

Alisema wamefanikiwa kuweka bikoni za kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji mita 60 kutoka kwenye maeneo ya maji katika maeneo ya mijini na vijijini, ili kuzuia uharibifu wa vyanzo hivyo unaofanywa na watu wakati mwingine hadi kwenye kingo za mito licha ya kuwapo kwa malalamiko kwa baadhi ya watu.

Mmassy alisema katika kulinda vyanzo vya maji wamelazimika kusitisha vibali 12 vya watumiaji maji mkoani Morogoro, ili kupunguza matumizi ya maji na kukabiliana na hali ya ukame iliyoko inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mmassy alisema bodi hiyo tangu Mei mwaka huu, ilitoa barua kwa wadau wake juu ya kutokuwapo kwa mvua za kutosha za masika na vuli na kuwataka kutowekeza kutokana na maji kutotosheleza.

Pia aliwataka wadau wa maji kuzingatia vipaumbele vya utoaji wa vibali, ikiwamo utunzaji wa mazingira, matumizi ya majumbani na kulingana na upatikanaji maji.

Alisema ifahamike kwamba hiyo ya ukame huwa inatokea kwenye mzunguko wa maji na ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan aliwekeza kujenga Bwawa la Kidunda ambalo linakaribia kuanza kufanya kazi iliyokusudiwa.

Alisema pia ujenzi wa mabwawa madogo madogo matano kwenye safu za milima ya Uluguru utapunguza shida hiyo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mwaka huu haukuwa na mvua toshelevu na kufanya kupungua kwa kina cha maji kwenye mito mingi.

"Miaka ya kawaida kwa tarehe kama ya leo kunakuwa na ujazo wa mililita 14,000 kwenye mto, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi hali imekuwa tofauti," alisema mkurugenzi huyo.

Mmassy alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuchelewa kwa mvua za vuli, wameitana na wadau wa maji na kuwa na mikakati na makubaliano mbalimbali hasa katika kutunza vyanzo vya maji na kuhakikisha wanakabiliana na kero zote za maji.

Alisema katika kikao hicho wamejadili mambo mengi yenye nia chanya ya kujenga na kuhifadhi vyanzo vya maji kwenye bonde hilo kwa njia ya kushirikiana kwenye kutunza na uwekaji wa mipaka kwenye vyanzo vya maji na kuwekeza kwenye miundombinu ya kutunza maji kipindi cha masika.

Alisema bodi imejenga mabirika sita yanayogharimu Sh. milioni 60 kwa wadau wa wafugaji ambapo matano yamejengwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kama mfano kwa wafugaji kujenga wenyewe hasa kwa wale wenye ng'ombe wengi kuanzia 1,000, hivyo wana uwezo wa kujenga kwa ajili ya kupata maji na malisho yao na kuepuka kuvamia na kuharibu vyanzo vya maji.



Mkurugenzi wa Masuala ya Sheria wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Kapwete John (kushoto), akitoa maelezo kwa wajumbe wapya wa Bodi ya Wakurugenzi ya mamlaka hiyo, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu sheria mbalimbali kabla ya kuanza vikao vyao leo. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Mark Mwandosya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Raia Uganda jela miaka mitatu kwa kuingia nchini bila kibali

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu kulipa faini ya Sh. 500,000 au kifungo cha miaka mitatu jela raia wa Uganda, Hamis Ismail baada ya kukiri kosa la kuwapo nchini bila kibali.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Rhoda Ngimilanga ambaye alisema mahakama hiyo imemtia hatiani kwa kosa la kuwapo nchini bila hati ya kusafiria yenye visa inayomruhusu kuwapo nchini.

"Mahakama inakutia hatiani kwa kosa moja la kuwapo nchini na unahukumiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au kutumia kifungo cha miaka mitatu jela kama utashindwa kulipa faini," alisema.

Awali, Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Hadija Masoud, aliomba mahakama kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na watu wengine, huku akidai kuwa hawana kumbukumbu za nyuma za jinai kwa mshtakiwa huyo.

Katika utetezi wake mshtakiwa huyo aliiomba mahakama kumsamehe kwa madai kuwa hali ngumu ya maisha kipindi cha corona ndiyo ilimfanya aje nchini.

Wakili huyo alidai kuwa mshtakiwa huyo aliingia nchini Oktoba 13, 2020 kupitia mpaka wa Mtukula ambayo iliisha Desemba 12, 2020 lakini aliendelea kuwapo nchini bila kuripoti ofisi yoyote ya uhamiaji.

Alidai kuwa Oktoba 24, 2022 mshtakiwa alipewa wito kwenda ofisi ya uhamiaji Ilala, alihojiwa kwa njia ya onyo na kuelezwa haki zake za msingi alikiri kuwapo nchini bila kibali na baada ya kuulizwa alikiri maelezo hayo.

Hata hivyo, alishindwa kulipa faini hiyo na kwenda jela miaka mitatu.

# EU yaipatia Tanzania bil. 371/- za kuboresha miradi mitatu

**Na Gwamaka Alipipi**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 166 (Sh. bilioni 371) kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi mitatu ukiwamo uboreshaji sekta ya fedha na uchumi wa buluu.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam juzi baada ya kuingia kwa makubaliano, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema miradi hiyo ipo katika mpango wa ushirikiano wa EU na Tanzania.

Alisema EU wamekuwa wadau wakubwa wa maendeleo kwa Tanzania tangu mwaka 1975 katika kuisaidia kufikia maendeleo endelevu.

"Hii imedhihirishwa kwa misaada ya kimaendeleo na mikopo ya masharti nafuu ambayo Tanzania imekuwa ikipokea kutoka EU, hadi sasa Tanzania imepokea misaada kutoka EU Euro milioni 2,394 (Sh. trilioni 5.9) kama msaada, jumla ya Euro milioni 270.9 (Sh. bilioni 706.5) zilipokelewa kama mikopo ya masharti nafuu kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya tangu kipindi hicho," alisema Nchemba.

Alisema EU imekuwa ikiisaidia Tanzania katika sekta mbalimbali ikiwamo uchumi sera za kisekta, usafiri wa barabara, viwanja vya ndege, nishati, kilimo, mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema Tanzania imepiga hatua katika maendeleo ya utendaji wa miradi, hadi sasa miradi mitatu kwa mwaka 2021 mikataba yake imeshasainiwa na utekelezaji umeshaanza.

Waziri Nchemba alisema katika msaada uliotolewa na EU, Euro milioni 110 (Sh. bilioni 246), zitaelekezwa katika uchumi wa buluu kwa miaka minne na kuchochea upatikanaji wa ajira na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mradi wa uboreshaji wa sekta ya fedha umetengewa Euro milioni 66 (Sh. bilioni 148) utatekelezwa kwa miaka minne, Euro milioni 50 zitachangiwa na EU na Euro 16 zitachangiwa na serikali ya Finland na Ofisi ya Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya kigeni.

Waziri Nchemba alisema lengo la mradi huo ni kuchangia katika mazingira wezeshi kwa maendeleo endelevu na ukuaji wa Tanzania.

Alisema pia utalenga uboreshaji wa usimamizi wa uwazi wa fedha za umma, kuboresha mifumo ya soko la fedha na kuongeza upatikanaji wa fedha kwa wanawake na vijana, pia itaimarisha uwajibikaji na mazungumzo jumuishi kuhusu utawala wa fedha.

Alisema programu hiyo pia itajikita kusimamia fedha za umma Tanzania Bara na Zanzibar, pamoja na makusanyo ya ndani, msaada wa bajeti.

Waziri Nchemba alisema mradi wa tatu ni kuboresha msaada wa ushirikiano wa Tanzania na EU na wabia wengine wa maendeleo ambao umetengewa Euro milioni sita (Sh. bilioni 13).

Alisema madhumuni ya mradi huo ni kuchangia utekelezaji wa ahadi za maendeleo ya kimataifa pamoja na malengo ya ushirikishwaji wa Tanzania EU.

Kadhalika, malengo mahususi ni kuimarisha utekelezaji pamoja na miradi yake iliyohusisha timu ya Ulaya, kuimarisha utaratibu mzuri wa miradi yote iliyoidhinishwa na EU pamoja na Tanzania.

Vile vile, kuimarisha ushirikiano wa kisiasa na maendeleo kwa ujumla.

Kamishna wa Ushirikiano wa EU, Jutta Urpilainen, alisema miradi hiyo itaongeza ajira kwa Watanzania pamoja na kukuza ushirikiano baina ya nchi za EU na Tanzania.

Urpilainen alisema, mikataba hiyo imeashiria ushirikiano mzuri kati ya EU na nchi za Afrika ikiwamo Tanzania.

# Wazazi, walezi watoto wa kichwa kikubwa wailalamikia Muhimbili

**Na Sabato Kasika**

BAADHI ya wazazi na walezi wa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, wamelalamikia lugha za baadhi ya madaktari wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kuwa zinakera na kuomba wasipokewe huko.

Walitoa malalamiko hayo juzi wakati kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi yaliyofanyika kimkoa kwenye Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), jijini Dar es Salaam.

Mmoja wa wazazi hao, Bilafa Makalani kutoka mkoani Lindi, akidai kuwa baadhi ya madaktari wanatumia lugha kali kwao, ikiwamo kwamba watoto wao hawawezi kupona na hivyo wasiwasumbue.

"Fikiria mimi kama mzazi ninateseka na ugonjwa wa mwanangu, halafu ninafika Muhimbili ninakutana na lugha kali, hii inaumiza sana, hivyo ninaomba tuwe tunapokelewa MOI," alisema Bilafa.

Alisema mazingira hayo sio rafiki kwao na kuomba utaratibu ubadilishwe, ili wasiwe wanaanza kupokelewa Muhimbili, badala yake wanapopeleka watoto wao kupata huduma za matibabu, wafikishwe MOI moja kwa moja.

Kauli ya mzazi huyo iliungwa mkono na Dorah Didacus kutoka Morogoro, ambaye alidai kukumbana na kadhia hiyo na kushauri kuwapo na mabadiliko, ili wasiendelee kunyanyapaliwa.

"Tunafanyiwa unyanyapaa sana na baadhi ya madaktari wa Muhimbili wanatukatisha tamaa kuwa tusiwasumbue eti watoto wetu hawawezi kupona, lugha hiyo inaumiza sana," alisema Dorah.

Kutokana na malalamiko hayo, Mkurugenzi Rasilimali Watu wa MOI, Orest Mushi, alitoa ufafanuzi kuwa: "Mtoto wa umri wa chini ya mwezi mmoja hawezi kulazwa MOI badala yake anaanzia Muhimbili."

Alisema mtoto wa umri huo anatakiwa kulazwa katika wodi ya watoto Muhimbili kwanza wakati taratibu zingine za kumhamishia MOI zikiendelea, huku akiwataka wazazi na walezi hao kuwa na subira.

"Tumesikia malalamiko yenu na tumeyapokea, tutakwenda kuyafanyia kazi na kuyatafutia ufumbuzi haraka iwezekanavyo, hivyo mtuachie tufuatilie ili kujua undani wa malalamiko haya," alisema Dk. Mchome.

Awali, akizungumza katika mkutano wa kilele cha maadhimisho hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema wameanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa kinamama wanaolazwa wakati wa matibabu ya watoto wao.



Mzazi wa mtoto wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, Bilafa Makalani kutoka mjini Lindi, akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

"Wakati mwingine huduma za matibabu zinachukua muda mrefu, hali inayokwamisha shughuli zao za uzalishaji mali, hivyo tukaona tuanzishe utaratibu wa kuwapa mafunzo ya ujasiriamali, ili hata wanaporudi nyumbani waweze kuyatumia kujiingizia kipato," alisema Dk. Boniface.

Alisema wanaofundishwa ujasiriamali huwa wanapewa mtaji kati ya Sh. 100,000 hadi 150,000 kulingana na fedha wanazopata kutoka kwa wafadhili, ili kuhakikisha kinamama hao wanakijimu kimaisha.

Msemaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Aminieli Aligaesha, aliliambia gazeti hili kuwa hakuwa na taarifa ya malalamiko hayo na kwamba atayafikisha kwa mkurugenzi wake kwa ajili ya hatua zaidi.

"Kifupi ni kwamba, wewe ndio unanipa taarifa za malalamiko hayo, hivyo nimeyapokea, sina uwezo wa kuyazungumzia, ila nitafikisha kwa mkurugenzi wangu," alisema.

## Ripoti yataja kampuni inayoongoza spidi mtandao intaneti

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Halotel Tanzania imeongoza kwa mara ya tatu kwa spidi yenye kasi ya intaneti.

Kwa mujibu wa ripoti ya robo ya tatu ya mwaka inayoishia Septemba iliyolotewa na Ookla, kampuni ya kimataifa inayofanya utafiti wa masoko ya mitandao ya simu na masuala ya uunganishi, Halotel imeongoza kwa kupakua Megabyte (MB) 17.63 kwa sekunde.

Taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo ilisema ripoti hiyo inaonyesha spidi ya kupakua ya Halotel ni kubwa zaidi ya wastani wa kitaifa wa Megabyte (MB)11.86 kwa sekunde kwa mitandao ya simu, na nusu ya uwezo wa kupakua kwa mitandao ambayo sio ya simu za mikononi ya Megabyte (MB) 33.17 kwa sekunde.

"Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu, Halotel pia iliongoza kwa kuwa na spidi ya kasi zaidi ya uwezo wa kupakua Megabyte (MB) 17.84 kwa sekunde, ikifuatiwa na Vodacom iliyokuwa na uwezo wa kupakua Magabyte (MB) 12.09 kwa sekunde na nyingine zikifuata, ilisema taarifa hiyo.

Pia ripoti hiyo inaonyesha, kwenye robo ya pili ya mwaka huu, kampuni hiyo iliongoza kwa kuwa na uwezo wa kasi zaidi wa kupakua Megabyte 17.12 kwa sekunde.

"Kwa kupima uimara wa spidi wa kila mtoa huduma, katika robo ya tatu ya mwaka, uchambuzi wa utafiti wa soko la mitandao umesema kwamba Halotel iko katika kiwango cha juu kwa asilimia 79.9, ikifuatiwa na kampuni zingine za simu zenye uimara wa asilimia kwenye mabano (76.1), (73.2), (48.9) na (42.8).

Kadhalika kwenye robo ya pili, Halotel pia iliongoza kwa kuwa na uimara mkubwa wa kimtandao kwa asilimia 80, ikifuatiwa na kampuni nyingine iliyokuwa na asilimia 72.1. "Hii inamaanisha kwamba uwezo wa kupakua na kuweka taarifa au kitu chochote kwenye mtandao kwa Halotel ni mkubwa zaidi ya watoa huduma wote."

Taarifa ya robo ya tatu iliyotolewa karibuni ya Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA) imeonyesha kwamba idadi ya wateja wa Halotel Tanzania imeongezeka na kufikia milioni 7.2 mwezi Septemba mwaka huu kutoka wateja milioni saba mwezi robo ya pili ya mwaka iliyoishia Juni.

Kampuni hiyo hivi karibuni ilinunua masafa ya 2600MHz toka TCRA yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 30.2 (takribani shilingi bilioni 70) na inatarajia kufikisha wateja milioni 10 hadi kufikia mwaka ujao.

Ripoti ya Ookla imeonyesha kwamba mkoa wa Dar es Salaam ndio unaongoza kwa kuwa na spidi kubwa ya intaneti kwenye mitandao ya simu ukiwa na uwezo wa kupakua Megabyte (MB) 13.90 kwa sekunde, ikifuatiwa na Mwanza ambao una spidi ya kupakua megabyte (MB) 13.45 kwa sekunde.

Mkoa wa Arusha unashika nafasi ya tatu kwa kuwa na mtandao wa simu wenye spidi ya kupakua Megabyte (MB) 11.29 kwa sekunde, ukifuatiwa na Mbeya (MB) 11.13 na Dodoma (MB) 7.28.





# Ofisi ya Kamishna Ardhi yakabidhi hati miliki 229

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

OFISI ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi mkoani Manyara, imekabidhi hati miliki za ardhi 229 kwa wananchi.

Hati hizo zilikabidhiwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere katika kilele cha maonyesho ya Manyara Trade Fair Exhibition.

Pamoja na mambo mengine Makongoro aliipongeza Ofisi ya Kamishna kwa kukabidhi hati hizo kwa wananchi walioomba.

"Watu wengi huwa wanaangaika kupata hati ila leo hawa wanapatiwa hati kwa saa 48 mmefanya kazi nzuri kupitia maonesho haya," alisema Makongoro.

Alikabidhi hati miliki 10 kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Manyara, hati moja kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Manyara.

Wengine aliowakabidhi hati kwa niaba ya wananchi ni Anna Aney, Swalehe Mohamed, Salimu Juma, Herman Raphael na Bashan Kinyunyu.

Akizungumzia utoaji wa hati hizo Kamishna Msaidizi wa Ardhi mkoani Manyara, Leonard Msafiri alisema wananchi 89 waliopatiwa hati waliomba kupia na kumilishwa hati kipindi cha maonesho hayo.

Alisema hati nyingine 140 zilizotolewa zilikuwa tayari katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi ila wananchi walikuwa hawajaenda kuzichukua, hivyo wametumia maonesho hayo kuzichukua kwa kuwa zilikuwa tayari.

Mmoja wa wananchi waliopewa hati hizo, Anna Aney alishukru Ofisi ya Ardhi kuwasaidia kupata hati ili kuwa wamiliki halali wa ardhi.

Alisema upatikanaji wa hati kwao kutawasaidia kuongeza thamani ya ardhi yao na kuepusha migogoro ya ardhi.

Akizungumzia maonesho hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Malt Super Brands Limited, David Mulokozi, aliahidi kuwaleta washiriki kutoka nchi za Afrika Mashariki ili kuongeza ubora.

Alisema kupitia maonyesho hayo wameongeza wigo wa kupata fursa za kibiashara kwa kupata mawakala wapya.

Katibu wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Manyara, Mwanahamisi Hussein, alisema maonyesho hayo yalikuwa na tija na mwaka ujao wataalika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), China, India na Uturuki kuja kushiriki.



Wanawake ambao ni wakulima wa maua, mboga, matunda, mimea itokanayo na mizizi na viungo, waliowezeshwa na Taasisi ya Kilele ya Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda na Viungo (TAHA), wakiosha tangawizi tayari kwa kusafirisha kwenda sokoni jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Kanisa lalamikiwa kupiga vyombo kwa sauti kubwa

**Na Jaliwason Jasson,** ARUSHA

WANANCHI wa Mtaa wa Mlimani wilayani Arusha wamelilalamikia Kanisa la Nguvu ya Utimilifu kupiga vyombo vya sauti kwa nguvu nyakati za usiku hali inayowasababishia kero.

Wakizungumza na Nipashe wakazi hao walieleza kuwa kanisa hilo limekuwa likifanya kitendo hicho kwa muda wa miaka mitatu sasa.

Mkazi wa Mtaa wa Mlimani, Barick Msuya alisema upigaji wa vyombo kwa sauti umekuwa ni janga kwa mtaa huo kwa kuwa kanisa hilo linapiga vyombo kwa sauti kubwa bila mpangilio.

Aliiomba serikali kuwaelimisha viongozi wa kanisa hilo namna ya kutumia vyombo hivyo bila kuathiri wananchi, huku akisema huduma ya kuabudu ni nzuri.

Mkazi mwingine Malijani Mstafa alisema licha ya kukaa nao vikao vinne na uongozi wa mtaa, kata na wilaya bado kanisa hilo limekaidi maelekezo ya Mkuu wa Wilaya.

Alisema upigaji mbovu wa vyombo umesababisha mama mmoja kupata maradhi ya moyo, aliiomba serikali kuwahamisha eneo hilo la makazi na kuwapatia eneo lingine.

Mkazi mwingine Abushiri Madaha alisema walishapeleka malalamiko katika Serikali ya Mtaa hadi ngazi ya Wilaya na Mkuu wa Wilaya akatoa maelekezo kwa Baraza la Uhifadhi wa Mazingira la Taifa (NEMC) Kanda ya kaskazini ili wamalize tatizo hilo lakini hakuna utekelezaji wowote.

"Watu tunashindwa kulala usiku, watoto wanashindwa kujisomea usiku na wagonjwa majumbani wanakosa utulivu kwasababu ya kelele," alisema Madaha.

Mkazi mwingine Hemed Mhando alisema licha ya wananchi kufanya vikao vingi na viongozi wa mtaa na kata ila bado kelele zinaendelea.

Alisema Mkuu wa Wilaya aliwahi kuiagiza NEMC imalize tatizo hilo ila bado wanalifumbia macho, huku wananchi wakiteseka na wengine kutishiwa.

Mhando alisema wao hawana tatizo la kanisa hilo kufanya maombi ila wafanye kwa staha bila kupiga vyombo vya muziki usiku kucha tena kwa sauti.

Aliiomba serikali kuwasaidia kutatua tatizo hilo kwa kuwa kanisa hilo ni tabia yao maana waliwahi kutimuliwa Mtaa wa Check Point kwa Mromboo kwasababu ya kupiga vyombo kwa sauti ya juu.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Muriet, Lucy Sungi, akiongea kwa njia ya simu na Nipashe alikiri kuwapo kwa tatizo hilo ambalo alidai ni la muda mrefu, kwamba alilikuta.

Lucy alisema malalamiko ya wananchi hao yamefikishwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na aliagiza NEMC kusimamia kanisa hilo liache tabia hiyo.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mlimani, Joanina Mkabatunzi, alikiri kuwapo kwa malalamiko hayo ambayo alisema uongozi wa Mtaa uliyashughulikia na kufikisha NEMC ili waendelee na hatua zingine.

Meneja wa NEMC Kanda ya Kaskazini, Lewis Nzali, alisema waliandika barua kwenda kwa kanisa hilo ili lijirekebishe na anadai kila akituma wataalamu hakuti kelele.

Nzali alisema taasisi au mtu binafsi mwenye tabia kama ya kanisa hilo akifikishwa mahakamani sheria inampa adhabu ya kufungwa kifungo cha miaka saba gerezani au kulipa faini Sh. milioni tano.

Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Nguvu ya Utimilifu, Jackson Ibrahim, akiongea na Nipashe alikana kupiga vyombo kwa sauti ya juu na kusema hata NEMC walipofika kanisani hapo hawakukuta kelele.

## Wananchi wawaita maofisa ardhi kutatua mgogoro kata

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

DIWANI wa Kata ya Loiborsoit, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Siria Kiduya, amesema wananchi wake wamewaita maofisa wa idara ya ardhi ya halmashauri hiyo kwenda kutatua mgogoro kati ya kata hiyo na Edonyongijape.

Alisema wananchi wa lLoiborsoit wamesikitishwa na kitendo cha baadhi ya wananchi wa Kata ya Edonyongijape kwenda kulima mazao kwenye maeneo yao.

"Wataalamu wa ardhi wanapaswa kutuonyesha mahali mpaka uliko ili wananchi wetu wafahamu na kufanya shughuli za maendeleo bila kutokea kwa tatizo lolote," alisema Kiduya.

Naye Diwani wa Kata ya Edonyongijape, Jacob Kimeso, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, alisema baadhi ya wataalamu wa idara ya ardhi wamekuwa wakiwachanganya wananchi kwa kuwa wanakuwa na ramani tofauti tofauti.


"Leo unawaambia wananchi mpaka wenu mwisho wake ni hapa, siku nyingine unawaeleza kitu tofauti na walichosema awali hivyo wanawachanganya watu kujua ukweli ni upi," alisema Kimeso.

Ofisa Ardhi wa Halmashauri hiyo, Baltazari Sulle, alisema mpaka unaotambulika hadi sasa hivi ni wa mwaka 1991 wakati wilaya hiyo, ikiwa iko kwenye Wilaya ya Kiteto.

Sulle alisema Wizara ya Ardhi bado inatambua mpaka wa awali wa Loiborsoit na Edonyongijape kwa kuwa huo mwingine wa mwaka 2012 uliofanywa na LAMP hautambuliki wizarani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, aliwataka wataalamu wa ardhi kuweka utaratibu wa kuwashirikisha wananchi na viongozi husika ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija.

Diwani wa Kata ya Ruvu Remit, Yohana Maitei Kadogoo, aliwataka viongozi kukubaliana na suala la mipaka kwa kuwa ni jambo la kuhofia kupoteza wapigakura kwa kuwa haliko chini ya uwezo wao.





## LHRC yaziomba AZAKI kusaidia jamii kuhusu TEHAMA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga ameziomba AZAKI kuhakikisha zinasaidia jamii kuendana na mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuleta matokeo chanya katika ulimwengu.

Alitoa ombi hilo wakati wa mkutano wa AZAKI uliofanyika jijini Arusha na kuwakutanisha wadau mbalimbali .

"Nawaomba AZAKI tubadilike tuendane na mabadiliko ya TEHAMA ili teknolojia hii isituache nje na tunapobadilika tubadilike na watu wote," alisema.

Alisema AZAKI zinafanya kazi kubwa katika jamii za aina mbalimbali na hivyo zinapaswa kuendelea ili kusaidia watu katika upatikanaji wa haki za kiuchumi, kiraia, kusikilizwa na nyingine nyingi.

Alisema haki ya kusikilizwa ni muhimu na ili mtu aweze kupata huduma za kijamii ni lazima asikilizwe.

"Mfano mradi ukiendelea katika jamii yao wananchi wapo tayari kujitolea kwa hali na mali ikiwamo fedha na hata ikitokea mfadhili amejiondoa mradi utaendelea sababu wananchi wameshirikishwa na wameona kile kinachofanyika ni chao,"alisema.

Kadhalika, alihimiza katika utawala bora, umuhimu wa kuandaa vijana kwenye utendaji kazi kwa sababu wao ni wepesi katika mabadiliko ya teknolojia tofauti.

**Alisema haki ya kusikilizwa ni muhimu na ili mtu aweze kupata huduma za kijamii ni lazima asikilizwe.**

# Moto waibuka tena Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MOTO uliozuka wiki iliyopita katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), umeibuka tena eneo lile lile la Karanga Camp kuelekea Baranco baada ya kutokea upepo mkali.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Eliamani Sedoyeka, kutokana na hali hiyo serikali imeongeza askari zaidi ya 400 kwenda kuungana na wenzao kuudhibiti moto huo.

"Huo moto ulizuka tena juzi usiku lakini kutokana na hali ilivyo sasa tumelazimika kuongeza vikosi mbalimbali vya ulinzi kwa kushirikiana na wadau wa utalii kwenda kudhibiti moto huo.

"Hata hivyo, tayari utafiti wa kubaini chanzo cha moto huo zimeanza kufanyika." Alisema Profesa Sedoyeka.

Jumapili iliyopita, serikali ilitangaza kupeleka vikosi vingine vya uokozi kutoka vitengo mbalimbali vyenye watu zaidi ya 500. Alipotafutwa kuzungumzia maendeleo ya uzimaji moto huo, Kaimu Kamishna wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Charo Mangare, alisema kazi hiyo inaendelea kufanywa kwa weledi ili kudhibiti majanga mengine kujitokeza.

Hadi kufikia Jumatatu ya wiki hii moto huo ulikuwa umeteketeza eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2.5, sawa na asilimia 0.4 ya hifadhi hiyo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,712.

Moto huo ulioanza kuwaka mwishoni mwa wiki iliyopita uligunduliwa katika eneo la kupumzikia wageni maarufu 'Karanga Camp' kuelekea Baranco, ukiwa unatembea kwa kasi zaidi ukiteketeza sehemu kubwa ya miti ya asili ya hifadhi hiyo.

Mara ya mwisho moto kama huo ulizuka na kuteketeza sehemu ya hifadhi hiyo, Oktoba 11, 2020 katika eneo la Whona, ambacho ni kituo cha kupumzikia wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo.

Kanzidata ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro inaonyesha kuwa mwaka 2015/16 eneo liliototeketea kwa moto ni hekta 49.13, mwaka 2016/17 hekta 17, mwaka 2017/18 hekta 82, mwaka 2018/19 hekta 72.3, mwaka 2020 hekta 22.05.

Kwa kipindi kisichozidi miaka mitano mpaka kufikia mwaka 2020, jumla ya hekta ambazo ziliteketea kwa moto katika hifadhi hiyo zinatajwa kufikia 242.48, huku sababu kubwa ya kuzuka kwa mioto katika eneo hilo ikielezwa uvunaji mbaya wa asali, ujangili na njia mbaya za kilimo.




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere (wa pili kulia), akimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mati Super Brands Ltd, baada ya kuwa mashindi wa kwanza kwenye maonyesho ya biashara ya Tanzanite Manyara katika uwanja wa Kwaraa, Mjini Babati juzi. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Wanafunzi 200 wanufaika programu elimu kwa vitendo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI zaidi ya 200 wamenufaika na Programu ya Elimu kwa Vitendo (PBL), ambayo inawaandaa kujiajiri na kuondokana na tatizo la ajira pindi wanapohitimu mitihani yao ya taifa.

Programu hiyo inayotolewa na Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Sekondari Tumaini Senior iliyopo Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, imewanufaisha wanafunzi hao kwa kuwawezesha kubuni na kutengeneza vitu mbalimbali kulingana na elimu waliyoipata.

Akizungumzia kuhusiana na programu hiyo katika hafla ya kuonyesha bunifu hizo, Mkurugenzi wa shule hiyo, Modest Bayo, alisema programu hiyo, ilianzishwa shuleni hapo mwaka 2016, kwamba hufanyika nje ya masomo ya darasani kwa wanafunzi kupata muda wa kujifunza kwa vitendo kulingana na uhitaji wao.

"Programu hiyo kwa njia ya vitendo imegawanyika katika ngazi mbalimbali ikiwamo utafiti kwa ajili ya malaria, uandishi wa habari na utafiti juu ya vinasaba (DNA), vyote hivyo tunafanya kwa vitendo, huku kila mwanafunzi akionyesha jinsi alivyojifunza,"alisema.

Aliongeza kuwa, tangu kuanza kwa programu hiyo imewajengea upeo wanafunzi katika uhalisia wa darasani kwamba pia imewasaidia wanafunzi wengi waliohitimu kujiajiri pindi wanapohitimu masomo yao.

Mkuu wa shule hiyo, Sifael Martin alisema kuwa mbali na hilo wameweza kufanya utafiti katika masuala ya Google, kwa kutumia kompyuta huku wakitengeneza Robot inayoweza kuruka juu, ikiendeshwa kwa njia ya programu ya drons.

Alisema kuwa mbali na programu hiyo ya PDL wamekuwa wakitoa programu ya Stemm ambayo inamwezesha mwanafunzi kufundishwa masuala ya sayansi ya kompyuta ambayo hujifunza lugha ya kompyuta katika kutengeneza programu.

Mwenyekiti wa Chama cha Walimu (CWT) Mkoa wa Arusha, Lotha Laizer alisema kuwa, uwapo kwa programu hiyo shuleni ni muhimu kwa wanafunzi kwani inawawezesha kujiajiri, pindi wanapomaliza.

Mmoja wa wanafunzi shuleni hapo, Given Malyango wa kidato cha nne, anayefanya programu ya utafiti wa panya na vyura, wanavyoweza kutumika kwa ajili ya kujifunzia kwa vitendo alisema kuwa walianza kwa kufuga panya wawili hadi sasa wamezaliana hadi kufika 11.




Ukurasa 17

**Wanahabari tuache uchawa kwa wanasiasa**



Ukurasa 16

Wazazi wenye kichwa kikubwa, mgongo wazi wanolewa ujasiriamali wajikimu

BUFE
IJUMAA OKTOBA 28, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 19

**Ijue Faida Fund; mtaa mpya wa uwekezaji kwa wasio nacho**

# Samaki Pweza; bidhaa mpya ya mageuzi kwa vijana wa Tanga

**Na Boniface Gideon,** Tanga




Wavuvi wa samaki pweza wakiwa na bidhaa zao. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

SAMAKI aina ya Pweza amejizolea umaarufu mkubwa nchini, hususani katika ukanda wa Pwani, vijana jioni hukutwa wanasubiria kupimiwa supu yake.

Uvuvi wa Samaki aina ya Pweza katika mkoa wa Tanga unaongozwa na wilaya ya Mkinga, Wilaya hii inaongoza kwa Uvuvi wa Pweza kutokana na kuwa na miamba bahari mingi kuliko sehemu nyingine yoyote hapa Tanga.

Ikumbukwe kuwa pweza anaishi kwenye miamba tu na hana uwezo kuhama kutembea kwenye maji yasiyokuwa na miamba.

Wavuvi hao wa samaki aina ya Pweza kata ya Boma Wilayani Mkinga, wapo kwenye furaha kubwa baada ya Oktoba 12 kuvua Pweza, wengi waliozidi kilo 800 ikiwa ni historia kwenye maisha yao ya uvuvi ambao walifanikiwa kuvua samaki wakubwa wenye uzito wa hadi kilo sita na wa chini alikuwa na gramu 500.

Ismail Kassim, Mwenyekiti wa Wavuvi hao alisema matokeo hayo makubwa yanakuja ikiwa baada ya kupatiwa elimu ya kufunga miamba kwa siku 90, ili samaki pweza wapate fursa za kuzaliana na kukua na baada ya hapo hukua hadi kufikia uzito kilo tano hadi sita, kwa pweza mmoja.

"Tunashukuru sana kwa kupatiwa elimu hii ya kufunga miamba baharini ambao leo hii imeleta neema kubwa, mvuvi mmoja leo hii amerudi na kilo 39,35 kitu ambacho sio cha kawaida.

"Kwani awali mvuvi mmoja alikuwa anavua pweza wa gramu 200-700 , tunaomba serikali itusaidie vifaa kama boti kwa ajili ya kufanyia doria baharini hasa nyakati za usiku ili tuilinde miamba yetu maana kuna wavuvi wanafanya uharibifu nyakati za usiku" alisisitiza Kassim.

**WAWEZESHAJI WAFUNGUKA**

Kwa mujibu wa wataalamu wa pweza kutoka Shirika la Mwambao Coastal Community Network Tanzania linalojihusisha na otoaji wa elimu ya utunzaji rasilimali bahari kwa jamii zishizo ukanda wa pwani, inaelezwa kuwa pweza hukua kwa siku 9.

Pia, hana uwezo wa kuhama zaidi ya eneo alilozaliwa ambapo huishi kwenye miamba bahari na huhitaji utulivu mkubwa ili apate kukua kwa haraka.

Jumanne Sobo, Msimamizi wa Mradi huo wa Uwezeshaji na Utoaji wa Elimu ya utunzaji Rasilimali Bahari kwa Wananchi waishio Mwambao wa Pwani, anawaambia waandishi wa habari wakati wa hafla ya kufunguliwa kwa miamba hiyo kuwa haikuwa kazi rahisi kufanikiwa kutoa elimu hiyo ya ufungaji wa miamba baharini kutokana na mazoea ya wavuvi ambapo kila mmoja alikuwa anajivulia kiholela.

"Awali kabla ya hatujawapatia elimu mvuvi alikuwa anapata pweza mwenye gramu 200 japo pweza wa kiwango cha gramu 200 ni kosa kisheria wakati mwingine gramu 500 na hadi 700 kwa siku. Inategemea na siku husika lakini kwa sasa mvuvi kupata pweza wenye uzito wa kilo mbili hadi tano ni jambo la kawaida sana," anasisitiza Sobo.

**MWEKEZAJI AFUNGUKA**

Msimamizi wa Mauzo wa kiwanda Cha Kusindika Pweza cha Alphakrest Ltd Cha Jijini Tanga, Siraji Juma alisema mahitaji ya kiwanda hicho kwa siku ni tani 5-6 lakini kwa sasa wanapata tani chini ya wastani tani mbili kwa siku.

" Sisi kiwanda chetu kina mahitaji makubwa sana ya pweza ambapo kwa siku moja tunahitaji tani tano hadi sita, lakini tunapata chini ya tani mbili kwa siku.

"Na kwa siku kama ya leo ya ufunguzi wa miamba baharini tutapata mzigo mkubwa angalau utasaidia kuzungusha soko letu " anasisitiza Juma.

Kwa upande wa bei anasema wananunua hadi Sh.8000 kwa kilo na baada ya makato ya kodi mvuvi hupata Sh.6000,

"Hapa bei zinapanda na kushuka lakini licha ya hivyo bado tunanunua kwa Sh.8000 lakini tunatarajia bei itapanda zaidi ya hapa huko mbeleni , hii inatokana na mahitaji ya pweza kuzidi kuongezeka kila siku" alisema Juma.

BIASHARA/UCHUMI

# Wazazi wa watoto vichwa vikubwa, mgongo wazi wanolewa ujasiriamali

**Na Sabato Kasika**

WAZAZI na walezi wa watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, wamekuwa wakitumia muda mwingi kukaa hospitalini kuhudumia watoto hao, huku shughuli zao za kiuchumi zikikwama.

Sehemu kubwa ya watoto wenye ulemavu huo, wamekuwa wakilazwa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), jijini Dar es Salaam. Na kwingineko ambako hukaa hata kwa zaidi ya miezi sita.

Hiyo ni kutokana na wanakaa muda mrefu hospitalini, shughuli zao za kuwaingizia kipato hasa kilimo, huwa zinalala, ambapo sasa umeanzishwa utaratibu ambao utawawezesha kukabiliana na ugumu wa maisha.

Taasisi hiyo imeanzisha utaratibu wa kuwapa ujasiriamali, ili wanapoondoka kurudi kwao, wakautumie kwa kutengeneza vitu mbalimbali na kuviuza ili kujiongezea kipato kwa ajili kuendesha maisha.

Utaratibu huo ni wa kuwapa mafunzo ya kutengeneza vitu mbalimbali umeanzishwa na taasisi hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa changamoto ya ugumu wa maisha kwa akina mama hao ambao wengi wao wanatoka vijijini.



Aziza Kasisiko (kulia) na mwenzake Sane Mashishanga, wakiwa na vifaa walivyotengeneza, baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**MKURUGENZI MOI**

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, anasema hayo kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi yaliyofanyika kimkoa kwenye taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam.

"Tulianza utaratibu huu tangu mwaka 2017 na tumeshatoa mafunzo kwa kinamama 135, Desemba mwaka jana tuliwapa mtaji akina mama 120 ambao walionyesha nia ya kufanya biashara," anasema Dk. Boniface.

Katika ufafanuzi wake, Dk. Boniface anasema, wapo kinamama ambao kila mmoja alikabidhiwa Sh. 100,000 na wengine kila mmoja alipata 150,000 kulingana na biashara anayotaka kuifanya.

"Wale ambao kila mmoja alipewa Sh. 100,000 waalipata pia vifaa vya kutengeneza bidhaa kama shanga au vikapu, wale wa 150,000 kila mmoja, ni wale wanaokwenda kufungua magenge au kununua pembejeo," anasema.

**MTAJI UNAKOTOKA**

Ofisa Ustawi wa Jamii wa MOI, Theresia Jacob, ambaye pia ni mkufunzi wa ujasiriamali, anasema taasisi hiyo ina wafadhili watatu wanaoisaidia, inazidi kuboresha huduma kwa watoto hao.

"Wafadhili hao Tema Traders, Yunis & Naomi na Mr & Mrs Gilbert Mrema ndio ambao pia wanatusaidia kwa kutupa mitaji

> **"Tulianza utaratibu huu tangu mwaka 2017 na tumeshatoa mafunzo kwa kinamama 135, Desemba mwaka jana tuliwapa mtaji akina mama 120 ambao walionyesha nia ya kufanya biashara.**




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Dk. Boniface Rwezimula (katikati). Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Mishipa ya Fahamu, Dk. Lemeri Mchome na Mkurugenzi Rasilimali Watu, Dk. Orest Mushi.

tunayoigawa kwa wanawake wenye watoto wa ulemavu huo, ili ziwawezeshe kuanzisha biashara mbalimbali ili kujikimu kimaisha," anasema.

Theresia anasema, amekuwa akiwafundisha wanawake hao kutengeneza bidhaa kama shanga, vikapu, bangili, hereni na maua ya aina mbalimbali kwa siku mbili kwa wiki ambazo ni Jumanne na Alhamisi.

"Pia watoto wenye ulemavu ambao wanasoma katika shule mbalimbali za msingi na sekondari, huwa wana vipindi vya masomo mara tatu kwa wiki, yaani Jumatatu, Jumatano na Jumamosi," anasema.

Katika ufafanuzi wake, anasema wanafanya hivyo ili isiwepo tofauti ya uelewa wa masomo kati ya watoto hao waliopo hospitalini na wenzao wanaoendelea na masomo shule, na kwamba wanatumia walimu kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

"Wadau wengine wanaotoa walimu ni Chama cha Maisha Mtoto na Foundation inayoitwa 'Life for Give Him', kwani watoto hukaa hospitalini kwa zaidi ya miezi minne na idadi yao hufika 37 kwa mwezi, hivyo tumeona ni vyema wawe na walimu wa kuwafundisha masomo ya darasani," anasema.

**WANUFAIKA WANENA**

Aziza Kasisiko, kutoka kijiji cha Nguruka wilayani ya Uvinza mkoa wa Kigoma ni mkulima ambaye hakuwa na ujuzi wowote, anapata mafunzo ya kutengeneza maua kwa kutumia nyuzi.

"Ninashukuru kupata ujuzi huu kwani umeanza kunisaidia, nimekuwa nikitengeneza maua ya kutembeza mitaani kutafuta wateja ambapo kwa wiki ninaweza kuuza maua nane hadi 10," anasema Aziza.

Anafafanua kuwa bei ya ua moja ni Sh. 15,000 na kwamba mtaji wake ukiongezeka, atapanua biashara yake hiyo na kuisambaza katika vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Uvinza.

"Nilipata ujuzi mwaka jana, hivyo ninaamini kwamba kadri Mungu atakavyonijalia, nitazidi kuboresha biashara yangu, ingawa changamoto ni kutembea na mtoto huyu wa miaka mitatu mgongoni," anasema.

Hata hivyo, anaongeza kuwa kufanya biashara hiyo akiwa na mtoto kuna unafuu kuliko kwenda naye shambani kulima, na kwamba atajitahidi kutunza fedha anazopata ili kuelekeza nguvu kwenye biashara hiyo.

Mnufaika mwingine, Sane Mashishanga kutoka Ikwiriri wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, anasema yeye amepata ujuzi wa kutengeneza vikapu ambavyo amekuwa akiuza kila kimoja kwa Sh. 45,000.

"Binafsi sijauza sana kwani sina muda mrefu tangu nianze kutengeneza, ila nimefanikiwa kuuza vikapu viwili, ninaamini watu wengi watakapojua kuwa ninafanya kazi hii, watajitokeza kuniunga mkono,"anasema.

**UBUNIFU ULIVYO**

Akizungumzia hatua hiyo, mtaalam wa saikolojia wa Taasisi ya Tanzania Suicide Prevention Coalition (TSPC), ya jijini Dar es Salaam, Mayasa Kalinga anasema, MOI imekuja na ubunifu mzuri kwa wanawake hao na watoto.

"Unajua baadhi yao wanaathirika kisaikolojia na kukata tamaa hasa kutokana na kwamba huduma za matibabu ya watoto wenye ugonjwa huo ni kubwa halafu wengine wanakimbiwa na waume zao," anasema Mayasa.

Mama huyo anaeleza kwamba, kitendo cha MOI kuwapa mafunzo ya ujasiriamali, kinawasaidia kufanya biashara mbalimbali na kupata kipato cha kuwasaidia angalau kuwahudumia watoto wao.

"Ikumbukwe kuwa wengi wao hawana kipato cha kutosha halafu wanaachiwa kulea watoto wenye ulemavu huo bila msaada kutoka kwa waume zao, kisaikolojia ni lazima watakuwa na mwazo mengi vichwani," anasema Mayasa.

Kwa mujibu wa mama huyo, kitendo cha kuwapa mafunzo na mitaji, kinaweza kuwafanya wakawa na matumaini mapya, katika malezi ya watoto hao, huku wakijitahidi kuhakikisha wanajiingizia chochote kupitia ujuzi waliofundishwa.

BIASHARA

# Naibu Waziri atembelea wachimba dhahabu wadogo, wampatia neno

**Na Halima Ikunji,** Nzega



Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, akizungumza na maofisa wa kampuni ya Savanah Leaf.. **PICHA: HALIMA IKUNJI**

NI hivi karibuni Naibu Waziri wa Madini Dk. Steven Kiruswa, amesema serikali kwa sasa imedhamiria kuhakikisha inawanyanyua wachimbaji wadogo wa dhahabu, hata wafikie ngazi ya wachimbaji wa kati na wakubwa, ifikapo mwaka 2025.

Kauli hiyo inaanzia kwenye mkutano wa hadhara katika kijiji cha Igulubi, Mwamikola wilayani Nzega, wilayani Igunga kwenye Mgodi Namba Tano, wakati wa ziara ya siku mbili kukagua sekta madini mkoani Tabora.

Dk. Kiruswa anasema, serikali inawatambua wachimbaji madini nchini na ina wajibu wa kuwasaidia kuhakikisha wanafikia uchimbaji mkubwa.

Ufafanuzi hapo ni kwamba wanawathamini, kwani wanalipa kodi na kuisaidia jamii katika maeneo yanayowazunguka, lengo ni serikali kuwajengea uwezo na kuwapa dira waweze kupanda kutoka uchimbaji mdogo, hadi wa kati kuelekea uchimbaji mkubwa, mapato yaongezeke.

Dk. Kiruswa anasema katika ziara yake ya kukagua sekta, dhamira iliyoko ni kujua changamoto zinazowakabili wachimba madini, serikali izichukulie hatua, akisisitiza wachimba madini wanatakiwa kufuata sheria za uchimbaji na kuzingatia usalama na, maelekezo katika miduara yao, ili serikali ipate urahisi kuwasaidia .

Dk. Kiruswa, anasema serikali sasa inanuia kuwa na wachimbaji wadogo wanaochangia pato la taifa kwa asilimia nane kwa mwaka, pia kuwa na taratibu zote zilizowekwa za uchimbaji, ikiwemo za usalama wao.

Anawahimiza wachimbaji waliowekeza katika migodi ya Nzega na Igunga, waendelee kuisaidia jamii inayowazunguka kama walivyoelekezwa na serikali.

"Igeni mfano uliofanywa na kampuni ya Savanah Leaf ya wilayani Nzega kuleta vifaa vya kisasa vya kuchenjua dhahabu na vipimo vya utafiti wa miamba na kusaidia jamii iliyowazunguka katika suala la afya, maji na elimu," anafafanua.

Hapo naye, anawawahakikishia wachimba dhahabu, kwamba mfumo wa serikali haumpunji mchimbaji wa madini yeyote, kila mtu atapata haki yake kutokana na nguvu anazowekeza, kwa kazi anayoifanya.

Dk. Kiruswa anamuagiza Ofisa Madini Mkoa wa Tabora, Mayigi Makolobela, kuanzisha mchakato wa kuwa na kituo cha ununuzi wa madini ya dhahabu katika wilaya ya Igunga, ili kurahisisha biashara hiyo ambayo inaongoza kwa uzalishaji nchini.

Anaeleza kwamba, mzunguko wa fedha wa soko la madini umefikia shilingi bilioni 48, zinazotokana na kuuzwa na kununuliwa dhahabu katika soko kuu la mkoa wa Tabora.

Hapo ana maelezo kwamba, wafanyabiashara wa mkoa huo wanategemea soko la madini lililopo wilayani Nzega pekee, hivyo ni muhimu kuanzishwa soko wilayani Igunga, ambako ndiko kuna wazalishaji wakubwa.

Katibu Mkuu anasema kwamba, kutokana na mafanikio hayo, pia mwenendo mzuri wa makusanyo ya maduhuli serikalini, ni hali inayozidisha umuhimu wa kuanzisha kituo kipya cha ununuzi wa soko la dhahabu.

Naibu Waziri huyo anaupongeza mkoa wa Tabora kwa kuvuka lengo lililowekwa na serikali kwa makusanyo ya madini aina mbalimbali, kwani mwaka 2021/2022 katika lengo la shilingi bilioni 4.5 , mkoa ulikusanya shilingi bilioni 5.6, sawa na asilimia 126.

Anaeleza kwa mwaka wa fedha uliopo, mkoa umepewa lengo kukusanya shilingi bilioni 6.4 na mwezi uliopita, ukiwa ni wastani wa miezi mitatu zimeshakusanywa shilingi bilioni 1.5 sawa na asilimia 24.14 au robo ya malengo.

### NENO LA WACHENJUAJI

Mkurugenzi wa kampuni ya uchenjuaji madini ya dhahabu, Savanah Leaf, ya wilayani Nzega, Pilbaksh Ashiraf, ambaye ni mwekezaji mdogo, anaiomba serikali iwabadilishie njia ya umeme na kuwaunganishia unaogusa mgodi wa Resolute, ambao ni bora na inawaongezea tija ya uzalishaji.

Anasema, kampuni yao imechimba bwawa lililogharimu shilingi milioni 47 na kisima cha kisasa, kinachowasaidia wananchi 50 kupata huduma ya maji safi. Pia, anasema huduma walizoweza kuzitoa kwa jamii ni pamoja na kusafisha kisima cha kijiji cha zamani (mita 1.5) na kuchangia ofisi ya kijiji kila mwezi, kwa maendeleo yao wananchi waliowazunguka, tangu mwaka 2016 .

Anataja changamoto kubwa ni mzigo wa kuchenjua madini ya dhahabu, hivyo anamuomba Naibu Waziri wa Madini Dk. Steven Kiruswa, awasaidie kubadilishia njia ya umeme, kwani kwa sasa wanakwama katika maendeleo ya uzalishaji.

Mkurugenzi huyo anamuahidi Naibu Waziri, watatafiti miamba ya kuchoronga na kutumika kutafiti na kuingia ubia na wachimbaji wadogo wenye leseni zao.

Ramadhani Rashidi, akizungumza kwa niaba ya wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, anaishukuru serikali kuwasaidia kuondoa migogoro iliyokuwepo, wakisimamia sheria iliyowekwa.

Pia, ana ombi kwa naibu waziri wasimamizi wao, wakiwamo Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na GST, wahamasishwe kuwafikia wachimbaji wadogo mkoani Tabora .

Rashidi, anawakosoa wachimbaji wenzake ,mbele ya naibu waziri, akiwataka waache tamaa ya kuingia kwenye maduara ya mashimo yaliyozuiliwa na serikali, kwani ni hatari kwao na hata baadhi yao wanapoteza maisha.

Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Tabora, Baraka Mbassa, anawatahadharisha wachimbaji wenzake, kwamba suala la utoroshaji madini ni ukiukwaji wa sheria, kwani mkosaji huangukia mikononi mwa sheria kwa tuhuma za uhujumu uchumi.

### OFISA MADINI

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Tabora, Mayingi Makolobela, anasisitiza kwamba panapokuwepo mdau anayehitaji taarifa zinazohusu biashara ya madini, afike katika ofisi hiyo kupatiwa taratibu, ili kuepuka kufanya shughuli zao kinyume na taratibu zilizowekwa kisekta.

Hadi sasa, anasema wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wilaya za Nzega na Igunga, wameshajenga madarasa mawili katika Shule ya Sekondari ya Nanga na kukarabati nyumba za walimu kijiji cha Igulubi.

Pia, wilayani Kaliua, eneo la Nsungwa, wachimbaji wadogo wamejenga ofisi ya kijiji, kutokana na mapato ya madini.

Kwa mujibu wa Ofisa Madini huyo, katika miaka miwili sasa anataja mafanikio anayoyaorodhesha; ukarabati wa jengo la ofisi, kuvuka lengo la makusanyo, kununuliwa kwa samani, kompyuta na mizani na kikuu, kuthibiti utoroshaji dhahabu uliokuwepo awali.

Ofisa huyo wa mkoa anasema, kwa sasa wamepangiwa kukusanya shilingi bilioni 6.4, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 1.9 sawa na asilimia 42 kutokana na ongezeko hilo.

Pia anataja mipango kazi waliyo nayo ni kuimarisha vyanzo vya mapato kwa wilaya zote za mkoa wa Tabora, kuwaelimisha wachimbaji wadogo ,mbinu za kisasa kwa kazi yao, wakishirikiana na wawekezaji .

Aidha anasema kwa sasa wanaendelea kuthibiti utoroshaji madini katika maeneo yote ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ,kuendelea kuimarisha ukaguzi wa migodi na kutatua migogoro inayosababisha uzalishaji kupungua na kufuatilia madeni ya miradi ya Tanroads ambayo haijalipwa mrahaba na ada ya ukaguzi.

> "Igeni mfano uliofanywa na kampuni ya Savanah Leaf ya wilayani Nzega kuleta vifaa vya kisasa vya kuchenjua dhahabu na vipimo vya utafiti wa miamba na kusaidia jamii iliyowazunguka katika suala la afya, maji na elimu.

BIASHARA

KIJANA ELIENA MALISA ANAPOJIAJIRI...

# Msomi aliyeegesha kando taaluma akifanya makubwa ng'ambo ya bia

## • Ushoga na mama, leo ana mgahawa maalum kwa wahitaji maalum Dar

**Na Romana Mallya**

"ISHI kama mfalme, asubuhi unakula kama mfalme, mchana unakula kama mtoto wa mfalme, jioni unakula kama mtumishi" ni msemo ambao umemuibua katika biashara ya chakula, Eliena Malisa, ambaye licha ya kusomea sheria, ameamua kuingia jikoni kuwaandalia mlo wateja wake, mfukoni ikimjibu kwa kipato.

Eliena Malisa, akiwa katika mazingira ya bashasha kumkaribisha mgeni wake mwandishi wa habari wa Nipashe aliyefika katika mgahawa wake ambao kwa jicho la kwanza unaendeshwa kidigitali zaidi.

Muda wote oda kupitia simu hazikomi, huduma mahali hapo ni za kupokezana, mlo wa mchana unapatikana tangu alfajiri, lakini kubwa mwendeshaji ni msomi wa sheria, sasa anaonyesha makubwa katika fani mbili tofauti; masoko na upishi.

Kama Waingereza walivyo na usemi 'mtoto kama mama yake' ni aina ya unasaba wa kuiga ameupata kutoka kwa mzazi wake (mama), hata ikambadilisha sasa yu katika makubwa zaidi, lakini akinong'oneza sheria bado imebaki kwenye damu yake, kwani haikwepeki.

Anajitambulisha kumaliza Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro mwaka 2016, lakini baada ya kuhitimu taaluma hiyo ya sheria, akaamua kukifungia kabatini cheti chake na kufungua biashara ya chakula kutokana na uhitaji uliopo sokoni.

Tofauti na migahawa mingine, mwanamke huyo ameamua kuja tofauti kwa kupika vyakula vya mchana wakati wa asubuhi, tena kuanzia saa 12 asubuhi, huku eneo lake la biashara likitambulishwa kwa jina 'Lunch for Breakfast' eneo la Survey, jirani na Mlimani City mkoani Dar es Salaam.

Anasema jina hilo linatokana na utafiti alioufanya na akabaini uhitaji wa chakula cha mchana wakati wa asubuhi kwa baadhi ya watu, pindi wanapoamka hutaka kula mlo kamili kabla ya kwenda kazini au kwenye shughuli zao.

Mwanamke huyo anayeendesha mradi huo na kinamama wenzake anasema, alibaini watu wengi wanapenda pindi wanapoamka kula mlo kamili kabla ya kuanza shughuli zao za kila siku.

"Ninaposema 'ishi kama mfalme' maana yake mtu anaamka asubuhi anakula mlo wake kamili, mchana anakula kidogo na jioni anakula kidogo zaidi au atakula matunda yake, kisha analala. Hapo hata mfumo wa chakula unakaa vizuri," anasema.



Eliena Malisa, akiwa kazini kwenye biashara. **PICHA ZOTE: ROMANA MALLYA**

> **Biashara yangu niliifanya kwa mtaji mdogo wa Sh. 100,000 na fedha hii niliipata kwa kujiwekea akiba kidogo kidogo, sikuwa mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu.**

**SIMULIZI ALIKOANZIA**

Ilikuwaje akafikia hatua hiyo? Eliena anasema, pamoja na kwamba amesomea sheria, lakini biashara ni kitu anachokipenda na imekuwa ikimpa msukumo mkubwa wa kutafuta vitu vipya kila siku ili kuboresha alicho nacho.

Anasimulia kwamba, kabla ya kufikia biashara hiyo, wakati akiwa mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, akiwa mwaka wa kwanza katika masomo hayo ya miaka mitatu, akajikuta ametumbukia katika uuzaji wa viatu vya mitumba kwa wenzake.

Eliena anasema, akaanza biashara hiyo baada ya kubaini ni moja ya hitaji kubwa kwa wanafunzi wakati huo, akaunda ubunifu wa kufika sokoni na kuanza 'kusagura' viatu vya mtumba na kuuza kwa faida.

"Nilianza biashara ya viatu mwaka 2015 nilipoingia chuoni. Kabla ya kuanza biashara, nilianza kujivalisha mwenyewe, wanafunzi wenzangu wakawa wanavutiwa wakawa wananiagiza.

"Biashara yangu niliifanya kwa mtaji mdogo wa Sh. 100,000 na fedha hii niliipata kwa kujiwekea akiba kidogo kidogo, sikuwa mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu," anasimulia katika mazungumzo hayo yaliyotawaliwa na kuhudumia wateja wenzake kwenye mradi, ikiwamo kupitia oda za simu, hata analazimika kusaidiwa aliyo nao kwenye mradi huo.

Anaeleza kwamba katika miaka mitatu chuoni, akatumia fursa ya soko hilo kwa wanafunzi kufanya biashara na wateja wake wakiwa ni wanafunzi na watu wengine nje ya hapo.

Mama huyo kijana, anasema baada ya kumaliza masomo chuoni, ndipo wazo lingine la kufanya biashara ya chakula likamjia. Hapo akatumia tena usomi wake kwa kufanya utafiti na akabaini, baadhi ya watu wamekuwa wakitafuta mlo wa mchana wakati wa asubuhi na wanaukosa.

"Nikaona ni kitu cha tofauti na sehemu nyingi hakuna huduma hii na binafsi ni mdau wa kula mlo wa mchana wakati wa asubuhi, lakini kila nilipohitaji chakula hiki maeneo mbalimbali, nilikuwa sipati," anaeleza.



Mwanasheria Eliena Malisa (kulia), akionyesha ujuzi wake jikoni wakati akiandaa chakula ambacho amekuwa akiwapikia wateja wake asubuhi, pembeni ni mwenzake, Rahma Ally.

Anasema kutokana na hitaji hilo, ndipo alipoamua kufungua eneo lake la kuuza vyakula vya aina hiyo ili kukidhi mahitaji ndani ya jamii.

Eliena anasema baada ya nafsi ya kibiashara kuidhinisha, akaipa jina la 'Lunch for Breakfast' ambayo ameianzisha mwishoni mwa mwezi Agosti, mwaka huu akijinasibu kila siku zinavyoenda , wateja wake wamekuwa wakiongezeka.

Anasema biashara yake im-

# yake sheria, ashara na lishe



elenga wateja wa kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa sita mchana, ambao anawaandalia vyakula vya aina mbalimbali kama, wali maharage, nyama, maini, pilau, chipsi, mayai na aina nyinginezo za mlo tofauti.

Kwanini biashara ya chakula, anasema anaamini hiyo imetokana na maisha yake tangu utotoni? Ni ufafanuzi kwa Nipashe, kwamba mama yake alikuwa akijishughulisha na upikaji keki, hivyo muda mrefu alitumia kukaa naye, hata ikamsaidia kujifunza mapishi ya aina mbalimbali.

Hivyo, anaeleza utashi uliomhamishia kwenye biashara ya viatu, ambayo imemvusha kwa miaka mitatu, sasa imemuwezesha kufungua eneo la chakula ambalo wateja wake wapo wanaokwenda hapo na wengine akiwapelekea walipo, akifafanua soko linapanuka maradufu .

**TAALUMA YAKE**

Swali la Nipashe likamrejesha darasani, kwa maana ya cheti chake cha shahada ya sheria, kakihamishia kabatini? Hapo Eliena anarejea katika kilichompeleka Mzumbe hajatekeleza unasaba nao.

Anasema, dhamira ya kusaidia Watanzania wanaohitaji msaada wa kisheria haijafutika kichwani mwake, ingawa bado hajafika katika Shule ya Sheria, kusaka idhini ya kusimama mahakami kitaaluma.

"Mpango wa kurudi kwenye kile nilichokisomea bado upo, nikishaweza kusimamia kitu kimoja kikasimama, ninaweza kuendelea na taaluma yangu ya sheria, kwa sababu ni kitu ninachokipenda," anasimulia.

Anasema amejikita zaidi kwenye biashara kwa sababu ya mazoea na kitu ambacho tayari ameshakifanya kwa muda mrefu na alipohitimu, akajikuta ameegemea zaidi biashara na siyo kutafuta ajira ya alichosomea.

Anasema licha ya kusomea taaluma hiyo hajawahi kuifanyia kazi zaidi ya mafunzo kwa vitendo wakati alipokuwa chuoni.

Hata hivyo, anabainisha kuwa suala la kila Mtanzania kujua sheria ni jambo la umuhimu na halipingiki.

"Kujua sheria ni muhimu, ukiachana na somo kila mtu anatakiwa kuhakikisha anajua sheria ili imsaidie katika maisha ya kila siku. Sijawahi kuomba kazi kupitia taaluma yangu, lakini mtu akitaka ushauri wa kisheria ninautoa," anabainisha.

**USHAURI KWA WAHITIMU**

Mwanamke huyo anawageukia wahitimu wenzake na kuwaeleza kuwa wakijisikia kufanya jambo tofauti na taaluma yao wasisite wafanye.


"Ukianza kufikiria sana mtaji utakuaje, anza na ulichonacho, anza bila kujali makosa wakati ukiendelea yasahihishe makosa utakayokutana nayo katika biashara, uwe na uhusiano mzuri na wateja kwa sababu hao ndiyo wanaokwenda kukuletea wateja wapya," anasema.

Pia, anaeleza kuwa, wakati wakitaka kufanya kitu wasiogope kuomba ushauri kwa watu wengine ili kuweza kupata mawazo mapya.

"Siyo lazima ufanye biashara zipo kazi ambazo hazihitaji taaluma yako unaweza kuzifanya wakati unasubiri kutimiza ndoto yako, tusikae tu kwa kusubiri lazima kujichanganya," anasema.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Wanahabari tuache uchawa kwa wanasiasa






NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

SASA hivi Mtanzania mwenzangu ukitaka kujua nchi inakwendaje na iko wapi, usikose taarifa ya Kikosi Kazi cha Chifu Hangaya kilichotafiti masuala ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Mimi leo kwa heshima na unyenyekevu, nijikite kwenye hili linalotuhusu la uandishi wa habari, unapofika wakati wa uchaguzi, ambapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na vyombo vya habari vya umma, wagombea na vyama vya siasa huandaa mwongozo kwa vyombo vya umma, kwa mujibu wa kifungu cha 53 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Mwongozo unalenga kutoa fursa sawa kwa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa vyama vyote vya siasa, kuelezea Ilani, sera za vyama vyao na kutangaza habari za mikutano ya kampeni kwa kutumia vyombo vya habari vya umma.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO) ya mwaka 2015, masuala ya habari husimamiwa na sheria, lakini hakuna chombo kinachosimamia vyombo vya habari kwa ujumla na vyombo binafsi haviwajibiki kisheria kufuata Mwongozo huo.

Hali hiyo imezaa malalamiko kwa wanasiasa, vyama vya siasa (upinzani), watazamaji na waangalizi wa uchaguzi, kuwa baadhi ya vyombo huwa na upendeleo wa wazi, kwa kuchapisha au kufifisha habari za baadhi ya wagombea na vyama.

Kukua kwa teknolojia ya mawasiliano, kumesaidia wanasiasa kuanzisha akaunti za mawasiliano ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, Instagram, Telegram na mingine ambayo huitumia kufikia wafuasi wao moja kwa moja na kirahisi, bila kupitia kwa wanahabari wanaowalalamikia.

Ukuaji huo wa teknolojia, umekuja na changamoto zake, mathalani baadhi ya wanasiasa na wadau wamekuwa wakitumia mitandao kusambaza habari za kughushi, kutoa lugha za kuudhi, kejeli, matusi na upotoshaji kwa baadhi ya wagombea.

Hayo sasa, yakasababisha kutungwa kwa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2018. Hivi ndivyo tunavyolizwa sasa na sheria hizo zinazokanyaga uhuru wa habari nchini na kilio kinapazwa ili ziboreshwe.

Sasa basi, pamoja na hali hiyo, kilichobainika kwetu wanahabari ni cha kusikitisha, mathalan tunasemwa, kwamba tunakandamiza wapinzani kwa kuwanyima uhuru wa kutumia vyombo vyetu kutokana na vitisho kutoka serikalini; je ni kweli?

Tunatumiwa na wanasiasa kutoa matusi na kejeli kwa wanasiasa wengine badala ya kujadili hoja, lakini pia hatuko huru, kwani tunakuwa na upendeleo wa wazi kwa chama tawala, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi; mnasemaje hapo wananzengo?

Kingine, eti vyombo vya habari vya umma havitoi habari kwa usawa kwa vyama vyote vya siasa nchini; mpo? Halafu tunatuhumiwa kula mlungula mchana kweupe au kujipendekeza tukitarajia kuteuliwa tunapoandika au kutangaza habari katika kipindi cha uchaguzi; mnakataa hilo?

Kumbe watu wamegundua, kuwa sisi na wanasiasa hatuaminiani,kwani baadhi yetu hatutangazi kampeni za wagombea wote kwa usawa na eti ndiyo sababu, uhusiano kati ya vyombo vya habari, vyama vya siasa na wanasiasa huimarika wakati wa uchaguzi na kufifia baada ya uchaguzi; mnaionaje hii, lakini kaukweli kapo.

Hii sasa ni baba lao, kwamba baadhi ya wanahabari hujinasibisha na vyama vya siasa au kushiriki siasa, huku wakiendelea kufanya kazi ya uandishi wa habari, hali inayoondoa imani ya wananchi kwa vyombo vya habari; nani anabisha hapa, wakati wengine tumewakuta ndani ya magwanda kabisa!

Tunashauriwa kuunda chombo cha kusimamia maadili ya wanahabari na vyombo vya habari; ukiwapo pia utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria husika, ili vyombo vya habari vya umma vitoe fursa sawa, kwa kutangaza habari za wagombea na vyama vya siasa wakati wa uchaguzi bila upendeleo.

Lakini la msingi ni kuandaliwa kanuni zitakazoelekeza vyombo vya habari kuheshimu maadili ya taaluma ya uandishi wa habari, ikiwamo mwanahabari kuhakikisha anahakiki habari kabla ya kuitoa. Tukikosea hapa tumekwisha na tutaendelea kuitwa chawa wa wanasiasa. Alamsiki!

FEDHA

# Wenyeviti Halmashauri ya Magu hawajalipwa posho miaka mitatu

**Na Anthony Gervas,** MAGU

• Alalamika ugumu dai la Sh. 3000 kwa mwezi...

MFUMO wa serikali katika ngazi za wenyeviti wa vitongoji na mitaa, huwa wanalipwa posho na si mishahara au malipo rasmi katika mfumo wa kiserikali.

Katika Halmashauri ya Wilaya Magu, nako kuna mfumo wa ndani wa malipo ya posho kwa kada hiyo ya watumishi. Hata hivyo, sasa kuna madai hawajalipwa kwa miezi mitatu sasa, hata kugeuka changamoto kwa watendaji hao, baadhi waliokutana na Nipashe wakianika malalamiko yao.

Viongozi hao wanadai kwamba, mfumo uliopo wa malipo yao kutoka serikalini haujakaa vizuri, kwani wameachwa kutokuwa waajiriwa wa serikali.

Kimsingi, wenyeviti wa vitongoji na mitaa huchaguliwa na wananchi, kwa kupigiwa kura kwenye maeneo yao katika uchaguzi mdogo wa serikali za mitaa wanabaki sio waajiriwa.

Kinachofanyika ni halmashauri zao hukubaliana kuwalipa posho, ambazo ndio saa kwa Halmashauri ya Magu iko katika malalamiko, watendaji hao hawajalipwa.

Wanadai kwamba, wanafanya kazi kubwa masaa yote kuwatumikia wananchi, wakati mwingine hupokea maagizo makubwa kutoka serikalini ngazi za juu kitaifa yakiwataka kuyatekeleza.

**MWENYEKITI KITONGOJI**

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ng'wang'halanga 'A' katika kata ya Bujora, wilayani Magu, Ng'wenesho Malago, analalamika kinachowasibu ni kukaa madarakani miaka mitatu bila ya kupatiwa posho zao rasmi.

"Sisi wenyeviti wa vitongoji na mitaa huwa hatulipwi posho zetu, leo miaka mitatu tangu mimi niingie madarakani mwaka 2019 kama mwenyekiti wa kitongoji cha Ng'wang'halanga 'A' na hata wenzangu, hatujawahi kulipwa. "Posho tunazolipwa kwa mwezi ni shilingi 3,000 tu,ukiigawanya fedha hiyo maana yake tunafanya kazi na kulipwa kwa siku sh,100,lakini serikali wanashindwa kutulipa," analalamika.

Malago anasema, ni hali inayowakabili huku wakibeba wajibu mkubwa anaoainisha kwa mifano ya kutatua migogoro mbalimbali ya wananchi inayohusu ndoa, ardhi na mipaka ya mashamba.

Vilevile, anataja kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji, kuimarisha ulinzi na usalama wa mali za watu, kusimamia miradi ya maendeleo, pamoja na ulinzi dhidi ya uhalifu kama vile wa 'panya road' wanaibuka na kutoweka kwa vipindi tofauti mitaani.



Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ng'wang'halanga 'A' Ng'wenesho Malago, akizungumza na mwandishi wa Nipashe (hayupo pichani), hivi karibuni. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

> **"Posho tunazolipwa kwa mwezi ni shilingi 3,000 tu, ukiigawanya fedha hiyo maana yake tunafanya kazi na kulipwa kwa siku sh,100,lakini serikali wanashindwa kutulipa.**

Vilevile anataja kazi yao ya kusimamia usafi wa mazingira, kubuni na kuhamasisha ujenzi miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi, miradi ya elimu,afya, maji, barabara, masoko na utekelezaji shughuli zote za kiuchumi kwa jumla.

Mwenyekiti Malago, hapo anafafanua kwamba wamebebeshwa majukumu mazito katika utekelezaji wa maendeleo, hivyo ni vyema serikali yao ikaona namna ya kuwezesha kuwalipa, kama namna ya kuwapa nguvu, watekeleze majukumu yao kwa hamasa na tija zaidi.

**MAPENDEKEZO**

Mwenyekiti Malago anapendekeza, serikali iweke mfumo wa kuwalipa kiinua mgongo, wenyeviti hao pale wanapomaliza muda wao kipindi cha miaka mitano madarakani, kama ilivyo kwa madiwani na wabunge,kwa sababu majukumu wanayobeba kuitumikia jamii ni makubwa.

Hali kadhalika, anaiomba serikali ifikirie upya nyongeza ya posho zao iwalipe shilingi 30,000 kwa mwezi, ili angalau ziwasaidie kujikimu kimaisha, akisema amegundua kuwa majukumu yao ni mazito na yenye maslahi kitaifa.

Malago pia anatoa rai kwa wenyeviti wenzake na jeshi la polisi kushirikiana nao katika maeneo yao, kuhusu ulinzi na usalama, mfano katika vita dhidi ya 'panya road' na hawana mipaka, kwani hao wanatoka kwenye familia za wananchi wenyewe,

Mwenyekiti Malago anaikumbushia serikali kuwatazama katika suala zima kuwasaidia kupata bima ya afya, ili wanapougua iwapunguzie gharama za matibabu.

Anahimiza wazazi kuwalinda na kuwaonya watoto wao kuachana na vitendo viovu kama hivyo, ili kuepuka baadaye kuwa na taifa lenye mmomonyoko wa maadili.

Malago, analalamika kuwa serikali haiwapi semina wala elimu juu ya uongozi, pale wanapokuwa madarakani jambo linalochangia kutojua mipaka yao ya madaraka, hivyo wanajikuta wanakiuka waangukia lawama na makosa ya kisheria kazini.

Anatoa mfano katika hatua ya Sensa ya Watu na Makazi ya hivi karibuni,akidai serikali iliwashitukiza ghafla kutembea mitaani na makarani bila ya kuandaliwa kuwapatia elimu, akisema ilikuwa kazi ngumu walipokutana na wananchi wakihojiwa maswali walikuwa wakishindwa kuyajibu.

Malago anarejea dhana ya uelewa na uwajibikalji wao kwa jumla, kwamba katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi ya hivi karibuni, wao viongozi wa kuchaguliwa, bado wana mchango mkubwa kufanikisha mengi katika maeneo yao.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo katika mazungumzo yake na Nipashe, wamesaidia kwa kutembea kuwasaidia makarani wa Sensa,kutwa nzima wakiwa nao kwa muda wa siku nane, jambo linalotafsiri umuhimu wao katika umma na maendeleo kwa taifa.

Anarejea katika siku nane akashiriki suala la kutambua makazi, kuweka namba makazi na kuyaweka kwenye mtandao, pia kutambua barabara za mitaa.

Mwenyekiti huyo anakiri kwa kuishukuru serikali, baada ya kumalizika jukumu la Sensa, wakalipwa posho walizoahidiwa, shilingi 50,000 ambayo inabeba sura ya 'kifuta machozi kwa hali inayowakabili.

**DED MAGU**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, Fidelica Myovella, anapotakiwa kutolea ufafanuzi malalamiko hayo ya watendaji wa kuchaguliwa wenyeviti wa vitongoji na mitaa kutolipwa posho zao kwa miaka mingi, anakiri ukweli na kuna hatua zinaandaliwa kufanikisha malipo hayo.

Myovella anasema, halmashauri yake kupitia vikao vya Baraza la Madiwani, imeandaa bajeti ya fedha za kuwalipa wenyeviti wa mitaa,vitongoji na vijiji kwa miezi mitatu, ambayo ni Julai, Agosti na Septemba mwaka huu.

"Swali la kutolipwa miaka mitatu wenyeviti hao, siwezi kulijua wala kulijibu, kwa sababu kwanza sikuwepo hapa. Tumefanya maandalizi ya bajeti kuwalipa posho zao miezi mitatu, ambayo ni Julai, Agosti na Septemba mwaka huu, kulingana na ufinyu wa bajeti yetu,

"Shida ni ukomo wa bajeti katika makusanyo ya mapato, kila kitu kina taratibu zake unajua mimi mgeni hapa, sijui awali muda ule kulikuwa na makubaliano gani ya mkataba sisi na wao wachaguliwa,' anasema Myovella.

FEDHA

# Ijue Faida Fund; mtaa mpya wa uwekezaji kwa wasio nacho

**Na Beatrice Moses**



Kada ya wajasiriamali wanaotarajiwa kunufaika na mfuko mpya. **PICHA: MAKTABA**

KUNA mifuko kadhaa ya uwekezaji wa fedha, ambayo imeanzishwa nchini, baadhi inasimamiwa na taasisi za serikali na mingine kwenye sekta binafsi, ikitajwa kuwa lengo la jumla ni kuinua uchumi wa wenye kiu na maendeleo kwa ngazi tofauti.

Hivi karibuni Mfuko uitwao Faida Fund wenye lengo la kufungua fursa ya uwekezaji kiuchumi kwa wananchi wa kipato cha chini na kati ulitambulishwa kwa wadau wa sekta ya fedha kutoka benki mbalimbali nchini na madalali wa soko la fedha ili kubaini fursa zilizopo humo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investments (WHI) Dk Fred Msemwa, anasema Faida Fund ni fursa ya uwekezaji mkubwa wa pamoja wa fedha kwa kiwango kidogo cha kuanzia elfu 5 hadi 10,000 hatua ambayo inampa nafasi mwekezaji kuimiliki vipande ambavyo anaweza kuviuza au kuendelea kupokea faida kulingana na uwepo wa mfuko huo.

Katika mkutano huo uliofanyika jijini Dar es Salaam, Dk Msemwa, anasema uwekezaji katika vipande unalenga kupatikana mapato kupitia ukuaji wa mitaji na kutengeneza utamaduni wa kuwekeza katika masoko ya fedha na mitaji ambayo yana uhakika wa kipato kwa mwekezaji.

### MANUFAA YAKE

Dk. Msemwa anaeleza Faida Fund inatarajia kutoa malipo mazuri kwa wawekezaji kulingana na mwenendo wa mapato yatakayopatikana katika uwekezaji wa hati fungani za serikali na amana za muda wa kati katika mabenki.

"Faida fund imeweka mifumo ya teknohama ambayo ina lengo la kurahisha kuwekeza na kuuza sehemu ya vipande au vipande vyote bila kulazimika kuja katika ofisi za Faida Fund," anasema.

Anabainisha, pia wawekezaji wake wenye nia ya kununua nyumba zinazojengwa na WHI wanaweza kutumia fedha zao walizowekeza kwenye mfuko huo kununua au kulipa fedha za kianzio ili kununua nyumba.

Wawekezaji hao pia wanaweza kutumia vipande vyao kama dhamana wakati wa kuomba mkopo katika benki na hivyo kujiwezesha zaidi kiuchumi.

"Kiwango cha kuanzia kuwekeza ni shilingi elfu kumi na kuendelea na baada ya hapo unaweza kuwekeza shilingi elfu tano na kuendelea.

"Viwango hivi vina lengo la kuwashirikisha watanzania wengi zaidi ambao hapo awali hawakuweza kupata fursa ya kushiriki katika masoko ya fedha kutokana na kuwa na fedha kidogo kupitia uwekezaji wa pamoja," anasema,

Anasema pia mfuko huu umefungua fursa kwa mzazi kufanya uwekezaji kwa ajili ya mtoto mwenye umri wowote.

"Uwekezaji huo unaweza kufanyika kidogo kidogo kuanzia shilingi elfu 10 na kuendelea na baadaye shilingi elfu tano na kuendelea kwa muda mrefu ambapo baada ya muda uwekezaji huo unaweza kuwa ni fedha za kutosha kumuendeleza mtoto kielimu au katika ngazi za juu zaidi au kumuwezesha atakapotakiwa kuanza kujitegemea," anasema Dk Msemwa.

Anabainisha kuwa kwa kiasi kikubwa uwekezaji utafanyika kidigitali na hivyo kupunguza gharama za uwekezaji na kuleta urahisi na hivyo kuwanufaisha wawekezaji.

Dk. Msemwa anafafanua kuhusu Faida Fund ni uwekezaji wa pamoja unaotarajiwa kuanza kuuza vipande vya awali kuanzia Novemba 1 mwaka huu Mfuko huu umeanzishwa na (WHI), taasisi ya umma iliyo chini ya Ofisi ya Rais utumishi na Utawala Bora.

Anasema jukumu la WHI ni kusimamia uwekezaji na uendelezaji milki kwa kuwa tayari ina uzoefu wa uwekezaji wa nyumba kwa takribani miaka nane iliyopita na ilianza kazi zake na kwa kuanzisha mfuko wa nyumba ambapo kupitia huo imeweza kujenga nyumba 983 katika mikoa 19 Tanzania bara ikiwemo mkoa wa Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Singida, Morogoro, Arusha, Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga.

Awali WHI ilikuwa inauza nyumba zake kwa watumishi wa umma lakini ilipofika mwaka 2019, serikali ilitoa kibali kwa nyumba hizo kuuzwa kwa wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii pia na hivyo kumaanisha kuwa wanufaika wa nyumba hizo ni wafanyakazi walioko katika sekta ya umma na sekta binafsi pia.

Kwa kuwa miongoni mwa mafanikio ya kiuchumi katika ngazi ya kijamii ni pamoja na kuwa na makazi bora hivyo kuwezeshwa kumiliki nyumba ni hatua njema yenye mafanikio.

Pia, kuwezesha kumudu maisha kuwa bora ikiwamo kuwa na uhakika wa kupata mahitaji muhimu hivyo kupitia uwekezaji huo utawezesha wawekezaji kutimiza ndoto zao.

Kwa kuwa lengo la mfuko wa Faida Fund ni kuwawezesha wawekezaji kiuchumi kwa kukuza mtaji au fedha walizowekeza.

### USALAMA WA MFUKO

Dk Msemwa anaeleza kuwa muundo na usimamizi wa Mfuko wa Faida Fund una mifumo itakayohakikisha fedha za wawekezaji zitakuwa salama. Mosi, Faida Fund imeanzishwa kisheria na imeidhinishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko na Mitaji (CMSA) ambaye ndiye msimamizi wa sekta ya fedha.

> **"Faida fund imeweka mifumo ya teknohama ambayo ina lengo la kurahisha kuwekeza na kuuza sehemu ya vipande au vipande vyote bila kulazimika kuja katika ofisi za Faida Fund.**

Pili, Faida Fund utasimamiwa na Bodi ya Wadhamini ambayo inaundwa na Wakurugenzi Wakuu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF, PSSSF, NHIF na NHC, huku mwangalizi wa Mfuko huu ambaye ni benki ya CRDB fedha zilizowekezwa zitatunzwa.

"Kila mwaka, kila wawekezaji wa mfuko wawekezaji watakuwa na fursa ya kupata taarifa za maendeleo ya mfuko na mipango yake mbalimbali,"

Akizungumzia kuhusu usalama wa uwekezaji huo Mkuu wa Idara ya Mtaji na masoko wa benki ya CRDB Masumai Ahmed ambao ndiyo wasimamizi wa uwekezaji huo, kupitia mkutano huo aliwahakikishia wananchi Akiba Fund ni mahali salama kwa uwekezaji.

Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa WHI Pascal Masawe alisema kuwa malipo ya mfuko huo yanafanywa kwa mfumo wa serikali, mtu anaweza kujiunga kupitia simu hivyo siyo rahisi kufanyika udanganyifu wa aina yoyote.

Anasema kuwa hatua za uuzaji wa vipande utafanyika kila siku, mfuko utatuma taarifa ya malipo ya vipande ndani ya siku zote saba za wiki, mapato ya mfuko hayatakuwa na kodi ya mapato kwa wawekezaji.

UCHUMI

# Namna ilivyo Rais 'kaupiga mwingi' watumishi vyeti feki kuambulia



Kada ya wafanyakazi kwenye sherehe yao. Baadhi ndio wanufaika wa uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

HUENDA huko waliko, sasa ni kicheko kitupu baada ya kusikia taarifa kwamba, sasa watalipwa mafao yao. Hapa ni watumishi walioondolewa kazini katika taasisi mbalimbali za umma, kwa tuhuma za kuwa na vyeti feki.

Uamuzi uliochukuliwa na serikali dhidi ya watumishi hao, ninaweza kuuchukulia na msemo huu kwamba, 'jasho la mtu halipotei bure' kwani, watuhumiwa wa vyeti hivyo nao ni binadamu, wana familia zinawategemea.

Kwa ujumla ni kwamba wana watu wanaowategemea wakiwamo watoto na wazazi, haijulikani hadi sasa tangu walipotimuliwa bila kupewa chochote wanaishije, lakini Rais ameona kuna haja kuwakumbuka.

Ni uamuzi wenye mtazamo wa huruma, kuwezeshana watumie mafao hayo kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo biashara, ili waweze kujiingizia kipato cha kuendesha maisha yao.

Tangu Rais atoe maelekezo ya kuwalipa mafao watumishi hao, kumekuwapo na mtazamo na maoni tofauti katika mitandao ya kijamii, kutoka kwa baadhi ya Watanzania wakiwamo wanaolalamikia uamuzi huo.

Wapo wanaounga mkono uamuzi huo wengine wakilalamika kuwa walitumia fedha za umma bila kuwa na sifa au walikosesha ajira watu wenye vyeti halisi.

> "Serikali imejenga masoko mengi hasa maeneo ya mijini ikiwamo Dar es Salaam ambayo baadhi hayana wafanyabiashara, hivyo ni wakati wa kuchangamkia nafasi ili wapate meza za biashara.



Rais Samia Suluhu Hassan.

Yaani kila mmoja anasema lake.

Lakini kuna moja linasimama, 'wale nao ni binadamu' walitimiza wajibu katika maeneo yao ya kazi, kwani walitumia nguvu na akili zao kufanya kazi na si vyeti.

Kwa mantiki hiyo uamuzi aliofanya Rais ni sahihi, ikikumbukwa kuwa inawezekana hao wenye vyeti feki kwa upande wa elimu, ndio waliofundisha watu wengi ambao kwa sasa wana nafasi kubwa serikalini au kwenye mashirika ya umma na taasisi binafsi.

Hivyo, wale ambao wanahoji kuhusu uamuzi wa Rais Samia, ni vyema pia wakaeleza kwa ushahidi kuhusu udhaifu wa aliyefoji cheti kwamba kitaaluma ulikuwa upi, badala ya kulalamikia uamuzi wa kuwapaa mafao.

Pia, kuwapo kwa vyeti feki inaeleweka sio sahihi, bali ubinadamu nao una nafasi kuonyeshwa na Rais kwa kundi la wale wote waliotimuliwa baada kubainika kuwa na vyeti hivyo.

Ninaamini kupitia mafao, wote waliotimuliwa, kila mmoja kwa wakati wake akiyapokea anaweza kuanzisha mradi wowote wa biashara, ili kujiingizia kipato, hasa kwa kuzingatia kwamba, kwa sasa biashara ina nafasi kubwa.

Kwa sasa wengi wamekuwa wakijihusisha na biashara mbalimbali zikiwamo za mazao ya vyakula, mamalishe, matunda, mitumba na nyingine nyingi, hivyo si vibaya watumishi hao wa zamani nao wakajiingiza huko.

Serikali imejenga masoko mengi hasa maeneo ya mijini ikiwamo Dar es Salaam ambayo baadhi hayana wafanyabiashara, hivyo ni wakati wa kuchangamkia nafasi ili wapate meza za biashara.

Miongoni mwa masoko yenye nafasi ni lile la mawasiliano lenye uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 2,600 lakini kwa sasa wapo 964 tu baada ya wengine kuondoka na kwenda kwingine.

Viongozi wa soko hilo wameshawatangazia wale wanaotaka nafasi za meza au vizimba waende wapewe bure, hivyo si vibaya hata watumishi hao wa zamani waliopo Dar es Salaam wakaanza kujipanga kuchukua nafasi mapema.

Wanachukua nafasi huku wakiendelea na taratibu za kupata mafao yao, badala ya kusubiri kuchukua, hali ambayo inaweza kusababisha wakachelewa na kukuta nafasi zote katika soko hilo zimejaa.





# Serikali yaruhusu ujenzi shule shikizi kuwanusuru watoto

**Na Grace Mwakalinga,** ILEJE

SERIKALI imeruhusu ujenzi wa shule shikizi katika Kitongoji cha Nkanka kilichoko Kata ya Itumba wilayani Ileje, Mkoa wa Songwe ili kunusuru watoto waliokuwa wanatembea umbali wa kilometa 10 kufuata masomo Shule ya Msingi Rungwa.

Uamuzi wa kujengwa kwa shule hiyo umetokana na maamuzi ya kamati ya mawaziri nane wa kisekta inayoshughulikia migogoro ya ardhi kuagiza wakazi zaidi ya 300 wa kitongoji hicho, wanaodaiwa kuvamia Hifadhi ya Msitu wa Safu za Milima Ileje (Ileje Range) kuendelea kuishi eneo hilo bila kubughudhiwa na mtu yeyote.

Akitangaza hatua hiyo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde, alisema wizara hiyo itaanzisha shule shikizi kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wanaotoka umbali wa zaidi ya kilomita 10 kwa ajili ya kufuata masomo katika Shule ya Rungwa.

"Nafahamu adha wanayoipata watoto wetu kutembea umbali mrefu kutafuta masomo kwenye Shule ya Msingi Rungwa ambapo kwenda na kurudi hutumia kilomita 30," alisema Silinde.

Diwani wa Kata ya Itumba, Mohamed Mwala, alisema mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu umekuwa chanzo cha kuzorotesha maendeleo ya wakazi wake.

Alisema kabla ya uamuzi huo wananchi wa kitongoji hicho walikuwa wakiishi kwa hofu, kushindwa kufanya shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi, kilimo na biashara.

Mkazi wa kitongoji hicho, Agnes Nyondo alisema watoto wamepata shida kwa muda mrefu kwenda shule na kwamba licha ya kadhia hiyo pia walihatarisha usalama wao.

Elizabeth Kanyika alisema watoto wengi waliacha shule kutokana na umbali wa kufuata masomo, huku wengine wakipanda milima ya Ileje.



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, Geofrey Mwakihaba, akiwasilisha mada ya namna Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, inavyoweza kuondokana na tatizo la wananchi wake kujichukulia sheria mkononi, ikiwamo mauaji na vitendo vingine vya uhalifu, katika kikao cha viongozi wa dini na mila kujadili matatizo hayo, jana. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Mradi wa maji Mto Kiwira kugharimu bil. 300/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA), imeanza utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa maji kutoka Mto Kiwira uliopo wilayani Rungwe Mkoa wa Mbeya.

Mradi huo utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 125 kwa siku, utagharimu Sh. bilioni 300.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Edna Mwaigomole, alisema mradi huo utasaidia kukidhi mahitaji ya wananchi waishio jijini Mbeya na maeneo yanayozunguka mji huo.

Alisema mradi huo tayari umefikia hatua mbalimbali kama vile usanifu wa mradi na upembuzi yakinifu.

Mwaigomole alisema mradi huo utasaidia kufanikisha shughuli za kijamii na uzalishaji mali, viwanda vidogo na vikubwa ambavyo hutegemea maji kuendesha mitambo na mahitaji mengine.

"Uwezo wa mamlaka yetu sasa ni kuzalisha maji lita milioni 65 kwa siku huku mahitaji ya Jiji la Mbeya yakiwa ni lita milioni 90 kuna upungufu ikiwa ni lita milioni 25 alisema Mwaigomole.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma kwa Wateja, Neema Mangwala, alisema kuna tatizo kubwa ya uharibifu wa miundombinu ya maji hali inayosababisha maji kumwagika na maeneo mengine kukosa huduma hiyo.

Alisema wateja kutolipa ankara za maji imekuwa ni kikwazo kutekeleza miradi mingine ya maji. Mangwala alisema hadi sasa mamlaka hiyo inawadai wateja Sh. bilioni 1.9 na kwamba wanaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha deni hilo linalipwa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Bomba Mbili Kata ya Mwakibete, Rodrick Mwang'onda, alisema watakuwa mabalozi wazuri kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa ili kuondoka na hadha ya maji katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya.

Mkazi wa Mtaa wa Ghana, Rehema Braison, aliiomba mamlaka hiyo kuendelea kufanya usafi kwenye vyanzo mbalimbali vya maji ili wananchi wapate huduma ya majisafi na salama.

# TANESCO yaeleza sababu kukatika umeme

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Umeme nchini (TANESCO), Mkoa wa Mbeya, limesema tatizo la umeme kuzima linatokana na upungufu wa nishati hiyo katika vyanzo mbalimbali vya uzalishaji.

Kwa mujibu wa taarifa ya jana kutoka kwa Meneja wa TANESCO, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Mathias Solongo, kuzima kwa umeme kunatokana na kupungua kwa uzalishaji kwenye vyanzo vyake.

Alisema hali hiyo imesababishwa na mabadiliko ya tabia nchi na kuchangia uhaba wa mvua za kutosha kwenye kipindi cha masika na vuli.

"Athari za mabadiliko ya tabianchi yamechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa nishati ya umeme ambapo kwa nchi yetu tunategemea maji kuzalisha, adha hii inatokana na upungufu wa mvua za masika na vuli kuanzia mwaka 2021," alisema Mhandisi Solongo.

Vile vile, alisema katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati hiyo, shirika hilo linaendelea na jitihada za kuanzisha vyanzo vingine vya nishati kwa ajili kuwasaidia wananchi.

Vyanzo vilivyotajwa na shirika hilo kuongeza nguvu ya upatikanaji wa nishati ya umeme ni vya nguvu ya upepo, unaotokana na nishati ya jua jotoardhi na gesi ambayo itasambazwa maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wananchi.

"Kwa sasa tunalazimika kuzima umeme kwenye baadhi ya maeneo, tunaomba wananchi waendelee kuwa wavumilivu wakati tunashughulikia tatizo hilo na kulipatia ufumbuzi wa kudumu," alisema Mhandisi Solongo.

Hivi karibuni baadhi ya wamiliki wa viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti katika soko la Sido jijini Mbeya waliiomba serikali kutafuta ufumbuzi wa tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara wakidai kuwa hali hiyo inaathiri kazi zao na kuwasababishia hasara.





# Benjamin Mkapa ilivyookoa mabilioni matibabu kibingwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa imeokoa zaidi ya Sh. bilioni nne za matibabu ya wagonjwa wa figo, nyonga na magoti ambao wangetibiwa nje ya nchi.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema kwenye upandikizaji wa figo, wananchi 31 wamenufaika na huduma hiyo na kuokoa Sh. bilioni 2.3.

"Ukilinganisha gharama za utoaji wa huduma hapa nchini kwa Benjamin Mkapa zipo chini ambapo fedha inayotumika kuhudumia mgonjwa mmoja India hapa nchini inahudumia wagonjwa wanne hadi watano.

"Wastani gharama zinazotumika kupandikiza figo kwa mtu mmoja ni Sh. milioni 25 ambapo kwa India ni Sh. milioni 100," alisema.

Kuhusu uvunjaji wa mawe kwenye figo, alisema huduma hiyo imetolewa kwa wagonjwa 148 na kuokoa Sh. milioni 850.

"Wastani wa mgonjwa mmoja kuondoa mawe ni Sh. milioni 1.2 lakini nje ya nchi ni Sh. milioni saba, tumeokoa Sh. milioni 850," alisema.

Vilevile, alisema hospitali hiyo imeanzisha huduma za matibabu ya moyo na ina maabara maalum ya matibabu hayo bila kufungua kifua.

"Ni hospitali ya pili nchini kuwa na maabara hiyo ya utoaji huduma, na tangu kuanza kutoa huduma mwaka 2019, wananchi 715 wamehudumiwa kwa kufanyika uchunguzi ambapo kati yao wagonjwa 39 waliobainika kuwa na matatizo ya kuziba mishipa inayopeleka damu kwenye moyo, wamepata matibabu kwenye maabara hii," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wagonjwa wanane wamehudumiwa kwenye hospitali hiyo kwa kupandikiziwa betri kwenye moyo na watoto 12 waliozaliwa na matatizo ya moyo wamepata huduma kupitia maabara hiyo.

"Tunafanya upasuaji wa moyo wa watoto ambao wanahitaji kufunguliwa kifua, tumehudumia wagonjwa 10," alisema.

Kuhusu nyonga na magoti, alisema hospitali hiyo inafanya upasuaji kwa kuweka vipandikizi ambapo wagonjwa 56 wamefanyiwa na kuokoa Sh. bilioni 1.28.

"Wastani wa mgonjwa mmoja tunamtibu kwa Sh.milioni 12 ambapo nje ya nchi angetibiwa kwa Sh. milioni 35, tumeokoa kwa wagonjwa hawa Sh. bilioni 1.28 kama wangetibiwa nje ya nchi," alisema.

Pamoja na hayo, alisema hospitali hiyo imedhamiria ifikapo mwaka 2025 iwe ya pili nchini kwa utoaji wa huduma bora za kibingwa.

Alisema kwa mwaka 2022/23 hospitali hiyo imeanza ujenzi wa kituo cha mionzi cha matibabu ya saratani ambapo wamepokea Sh. bilioni 10.

"Pia huduma ya upandikizaji wa uboho tuliomba kuwezeshwa Sh. bilioni moja tumepewa na matibabu yataanza Januari 2023," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imewapatiwa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya kununua nyumba 40 za watumishi kutoka Shirika la Nyumba Tanzania (NHC).

Pia alisema wametoa mafunzo kwa watumishi 127 wa usingizi na ganzi ambao wamepelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio na utekelezaji wa shughuli za tume hiyo, kwa mwaka wa fedha 2022/2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Msajili Hazina ajivunia ukusanyaji wa mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Msajili wa Hazina imesema hadi kufikia Juni 30 mwaka huu, imekusanya mapato yasiyo ya kodi ambayo yanajumuisha gawio na michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi.

Pia imekusanya mapato mengine Sh. bilioni 852.98 sawa na asilimia 109.5 ya lengo.

Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Umma Ofisi ya Msajili wa Hazina, Lightness Mauki alibainisha hayo wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za taasisi hiyo kwa waandishi wa habari jijini Dodoma.

Alisema katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria, pamoja na mambo mengine, Msajili wa Hazina ana jukumu la kukusanya mapato yasiyo ya kodi ambayo yanajumuisha gawio, michango ya asilimia 15 ya pato ghafi na mapato mengineyo.

Mauki alisema ofisi imeendelea kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi ambapo mapato yamekuwa yakiimarika mwaka hadi mwaka.

"Kufikia tarehe 30 Juni 2022, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikuwa imekusanya Sh. bilioni 852.98 sawa na asilimia 109.5 ya lengo lililokuwa kukusanya Sh. bilioni 779.03 na asilimia 33.5 zaidi ya kiasi kilichokusanywa 30 Juni 2021 ambacho kilikuwa ni Sh. bilioni 638.87. Huu ni ufanisi mkubwa unaotia moyo na ambao haujawahi kufikiwa," alisema Mauki.

Aliongeza kuwa ufanisi huo umechangiwa na kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya uwekezaji wa mitaji ya umma, hatua za makusudi zilizochukuliwa na serikali katika kukuza mapato na kudhibiti matumizi pamoja na kuongezeka kwa shughuli za ufuatiliaji katika taasisi, mashirika ya umma na kampuni ambazo serikali inamiliki hisa chache.

Akizungumzia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero, alisema serikali ni mbia katika kiwanda hicho, ikimiliki asilimia 25 kupitia msajili.

"Kutokana na kuendelea kukua kwa mahitaji ya sukari nchini sambamba na ongezeko la malighafi kutoka kwa wakulima wadogo wanaolima kandokando ya Mto Kilombero, kumekuwa na uhitaji wa kupanua kiwanda cha sukari cha Kilombero, ili kutimiza mahitaji haya.

"Bodi ya wakurugenzi ya kiwanda baada ya kufanya uchambuzi wa kina iliwasilisha mapendekezo ya kupanua kiwanda kwa wanahisa, ambapo serikali kupitia Msajili wa Hazina pamoja na wanahisa wenza (Illovo Group), baada ya majadiliano waliafiki kutekeleza mradi mkubwa wa upanuzi wa kiwanda kwa gharama ya Sh. bilioni 571.6.

"Uwekezaji huo unatarajiwa kuzalisha sukari tani 144,000 ambazo zitaongeza uwezo wa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero kuzalisha sukari hadi kufikia tani 271,000 kutoka tani 127,000 za sasa," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea na juhudi za kusimamia utendaji wa kampuni ambazo ina umiliki wa hisa chache, ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano na wabia wenza na kusimamia kwa karibu matumizi yasiyo ya lazima ambapo ongezeko la gawio kwa wanahisa limeonekana.

"Mafanikio ya jitihada hizo yamejidhihirisha katika utendaji wa Benki ya NBC ambayo imeongeza faida kabla ya kodi kutoka Sh. bilioni saba mwaka 2020 hadi Sh. bilioni 60 mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia 757," alisema.

## Ndalichako ataka wadau kuipa ushirikiano OSHA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, ametoa wito kwa wadau wa sekta ya umma kushirikiana kikamilifu na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kuimarisha mifumo ya usalama na afya katika ofisi na miradi mbalimbali ya serikali.

Prof. Ndalichako alitoa rai hiyo juzi jijini hapo alipofungua mafunzo maalum ya usalama na afya yaliyoandaliwa na OSHA na kutolewa kwa maofisa ya wizara, mashirika ya umma, idara na taasisi za serikali.

Maofisa walioalikwa kushiriki mafunzo hayo kwa awamu ya kwanza ni pamoja na maofisa rasilimali watu na utawala, maofisa ununuzi na ugavi, maofisa sheria, wakaguzi wa ndani na maofisa mipango ambao kwa namna moja au nyingine wanahusika katika usimamizi wa ofisi za umma, mifumo mbalimbali ya kiutendaji pamoja na ustawi wa wafanyakazi.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Prof. Ndalichako, aliipongeza OSHA kwa kutekeleza maagizo ya ofisi yake, ikiwaagiza kufanya ukaguzi katika ofisi zote za serikali na kisha kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kuhusu uboreshaji wa mazingira ya kazi katika ofisi hizo na miradi mbalimbali ya ujenzi inayoendelea.

"Ni matarajio yangu kwamba baada ya mafunzo haya ya siku mbili mtapata uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi na mtaweza kwenda kuisimamia vizuri.

"Tunawaomba mkawe mabalozi wetu na mkatusaidie kuwaelekeza wafanyakazi wachukue tahadhari kwani mnaweza kuwapa vifaa vinavyotakiwa lakini wakavitumia tofauti na maelekezo ya kitaalamu.

"Niwapongeze OSHA kwa kutekeleza maagizo niliyowapatia mwezi Aprili lakini ningependa kuona mnawafikia wadau wengi zaidi na hata baadaye mnaweza kupanga kuwakutanisha makatibu wakuu kwa ajili ya kuwapa elimu hii ili kurahisisha utekelezaji wa masuala haya," aliagiza Prof. Ndalichako.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mrejesho wa kampeni ya ukaguzi na uchunguzi wa afya za wafanyakazi iliyoendeshwa na taasisi yake mwezi Aprili na kubaini shida mbalimbali za usalama na afya ikiwamo uelewa mdogo miongoni mwa wadau.

"Mafunzo haya ni sehemu ya mkakati wetu wa kushughulikia shida tulizozibaini katika kazi tuliyoendesha Aprili, ambapo tulibaini kuwapo ombwe la uelewa na hivyo tumeamua kuliondoa kupitia mafunzo haya kwa makundi mbalimbali ya watumishi ambao tutawafikia kwa nyakati tofauti," alisema Khadija.

Alieleza kuwa kupitia mafunzo hayo kutakuwa na uelewa wa pamoja miongoni mwa watendaji mbalimbali wa serikali na hivyo kuwezesha utoaji wa huduma kwa wananchi katika ofisi za umma pamoja miradi mbalimbali ya serikali kufanyika kwa kuzingatia kanuni za usalama na afya.

# Uwekezaji kidijitali NMB kutumika kukuza uchumi wa buluu Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KONGAMANO la Sita la Kitaifa la TEHAMA (TAIC 2022) limefunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, huku Benki ya NMB ikilitumia kuiahidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuwa itatumia nguvu ya uwekezaji wa kidijitali iliyofanya katika kuchangia kasi ya ukuaji wa uchumi wa buluu.

TAIC 2022 ni kongamano la siku tatu kuanzia Oktoba 26 hadi 28 lililoratibiwa na Tume ya TEHAMA (Tanzania ICT Commission) likiwa na kaulimbiu 'kutumia mabadiliko ya kidigitali katika uchumi wa buluu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi', likishirikisha zaidi ya watu 1,000, wakiwamo wadau 800 wa TEHAMA, waalikwa, kampuni washirika na wadhamini wa ndani na nje zaidi ya 200.

Akizungumza wakati akiwasilisha mada katika kongamano hilo, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa NMB, Benedicto Baragomwa, alisema ahadi yao hiyo ni mwendelezo wa ushirikiano wao na SMZ.

Alisema benki yake imekuwa mchangiaji mkuu wa ukuaji wa uchumi wa buluu Zanzibar kupitia makubaliano mbalimbali iliyosaini na kwamba visiwa hivyo ni wanufaika wa uwekezaji wao wa mabadiliko ya teknolojia.

Baragomwa alibainisha kuwa ushirikiano wao na Umoja wa Kampuni za Kutoa Huduma za Utalii Zanzibar (ZATO) uliozaa Kadi Maalum ya Malipo Kabla (NMB, ZATO Prepaid Card) na ule wa Wakala wa Serikali Mtandao (NMB e'Government Zanzibar), unaokusanya malipo ya taasisi za SMZ kupitia mifumo ya NMB, ni kielelezo cha mchango wao uliotukuka wa kukuza uchumi wa buluu.

"Kupitia NMB e'Government Zanzibar, benki imewezesha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Malipo Kidijitali 'One Stop Center' cha Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), ambako malipo mbalimbali hupitia 'control number' moja na hivyo kurahisisha makusanyo na kukuza pato la serikali inayochakata Sera ya Uchumi wa Buluu," alifafanua Baragomwa.

Alisisitiza kuwa uwekezaji mkubwa wa mabadiliko ya mifumo ya kidigitali uliofanywa na NMB tangu mwaka 1997, ndio siri ya asilimia 94 ya miamala ya benki hiyo hivi sasa kufanyika kidigitali nje ya matawi yao 228, wakichagizwa pia na mawakala zaidi ya 10,000, ATM zaidi ya 800 na huduma zinginezo, zikiwamo za Teleza Kidigitali, NMB Mkononi na Vituo vya Mauzo (PoS).

Baragomwa alieleza siri iliyowasukuma kushiriki kongamano hilo kuwa ni kuona umuhimu wa teknolojia katika uchumi (digital economy) ambako benki yake imefanya mengi kama taasisi kuwekeza kwenye ubunifu na kutoa masuluhisho mbalimbali.

"Kwa Zanzibar, katika 'blue economy' (uchumi wa buluu) tumefanya mengi kuharakisha ukuaji wa uchumi na kupunguza matumizi ya fedha taslimu kupitia hiyo 'one stop center' na PoS.

"Pia hivi karibuni pale uwanja wa ndege tumezindua ATM ya kubadili fedha za kigeni kama pauni, dola na euro kuwa shilingi za Kitanzania kwa saa 24," alisema Baragomwa.

Kongamano hilo lilihudhuriwa pia na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, ambaye aliitaja Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama kitovu cha ukuaji wa haraka wa uchumi wa nchi yoyote na kupongeza jitihada za wadau wa serikali katika maendeleo kwa kufanikisha kongamano hilo la kitaifa linalofungwa leo Oktoba 28.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhi tuzo kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa MIC Tanzania, Kamal Okba, katika ufunguzi wa minara 42 na vituo 11 vya TEHAMA Bwefuu, Mkoa Mjini Magharibi juzi, iliyojengwa kwa fedha za ruzuku za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), ambapo Tigo kushirikiana na UCSAF zimewezesha ujenzi wa minara ya mawasiliano katika maeneo ya kimkakati kote nchini ikiwamo Unguja na Pemba. Kushoto ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ kuimarisha uchakataji nafaka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) itaendelea kuhakikisha inaimarisha sekta ya uchakataji wa bidhaa za nafaka Zanzibar.

Aliyasema hayo jana katika mkutano wa 32 wa Jumuiya ya Kimataifa ya Uchakataji Nafaka (IAOM) uliofanyika Hoteli Verde Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali inatambua mchango wa sekta hiyo ya uchakataji wa bidhaa za nafaka nchini, akifafanua kuwa mabadiliko ya tabianchi yameathiri uzalishaji na uchakataji wa bidhaa za nafaka, hivyo kuwataka wadau wa mkutano huo kujadili suala hilo na kupata ufumbuzi wake.

Alisema mkutano huo utawasaidia wadau hao katika kubadilishana uzoefu, uelewa na teknolojia kwenye sekta ya uchakataji wa bidhaa za nafaka.

Rais Dk. Mwinyi aliwaalika wadau hao kuwekeza Zanzibar hususan katika eneo la uchumi wa buluu.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaabani, alisema Serikali ya Zanzibar inafanya jitihada kubwa kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwamo sekta ya uchakataji wa bidhaa za nafaka.

Alisema juhudi hizo za serikali ni fursa kwa wadau wa mkutano huo kuwekeza Zanzibar.

Mwenyekiti wa mkutano huo wa 32 wa IAOM, Muniri Bakheresa, alisema mkutano huo utatoa fursa kwa wadau hao kujadili teknolojia ambazo zinatumika kwenye shughuli za uchakataji wa bidhaa za nafaka.

Alisema ni muhimu wadau hao kujadili teknolojia kwa kuwa inasaidia kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa ambazo mlaji anazihitaji.

# Mkuu wa wilaya apongeza wanakijiji kuwekeza uvuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kusini, Rajab Yussuf Mkasaba, amesema amepongeza uamuzi wa wananchi wa Kijiji cha Kizimkazi Mkunguni kujitafutia maendeleo na kukuza kipato chao kupitia sekta ya uvuvi, akitaka waungwe mkono.

Aliyasema hayo juzi huko Kizimkazi wilayani humo wakati akizungumza na wananchi wa kijiji hicho katika hafla ya uzinduzi wa uvunaji wa pweza.

Alisema kusimamia ufugaji wa pweza kunahitaji ujasiri mkubwa na kuna baadhi ya watu wasio waaminifu huharibu kwa makusudi taratibu zinazowekwa na kuingia baharini kuiba pweza wanaofugwa.

Mkasaba alitumia fursa hiyo kuwapongeza wananchi wa kijiji hicho kwa ustahimilivu wao mkubwa kwa kipindi chote cha miezi mitatu kufanya kazi hiyo bila kujitokeza ukorofi wa aina yoyote.

Alisema ushirikiano huo ndio unaohitajika miongoni mwa jamii na ndio sababu kuu ya kuendeleza umoja na mshikamano na kudumisha amani na usalama katika jamii.


Mkasaba alisema panapojitokeza wananchi wakorofi na kutofuata matakwa ya makubaliano, wakati mwingine hupelekea kujitokea viashiria vya uvunjaji wa amani, jambo ambalo halipewi nafasi katika wilaya hiyo.

Kutokana na mafanikio hayo, Mkasaba aliwaeleza wananchi hao kwamba ofisi yake imeamua ufugaji wa pweza katika ukanda huo usimamiwe na wilaya kwa lengo la kufuata taratibu na miongozo inayotolewa na vijiji husika kupitia kamati zao juu ya ufugaji na uvunaji wa pweza.

Alieleza kuwa hatua hiyo itasaidia kuondoa migogoro inayotokea kati ya kijiji na kijiji katika kazi hiyo.

Diwani wa Muyuni, Mustafa Haji alisema ushirikiano mzuri kati ya wananchi na kamati ya uvuvi ya kijiji hicho ndio iliyosababisha kufanikisha kazi hiyo ya uvunaji wa pweza, wakiwavuna kwa wingi na wananchi kujiingizia kipato.

Wananchi wa kijiji hicho cha Kizimkazi Mkunguni waliahidi kuendelea kumuunga mkono mkuu wa wilaya huyo na kuendelea kufanya kazi za halali kwa lengo la kujiongezea kipato na kuondokana na hali ngumu ya kiuchumi.



# Musoma kupanda miti 100,000 kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Mathias Marwa,**
MUSOMA

KUTOKANA na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame katika maeneo mbalimbali nchini na kutishia hali ya upatikanaji wa chakula, malisho ya mifugo na maji, Jimbo la Musoma vijijini limeandaa mkakati wa kupanda miti 100,000.

Kupitia mkakati huo unaotarajia kurejesha ukijani katika Jimbo la Musoma, Mbunge wa jimbo hilo, Prof. Sospeter Muhongo, aliitaja miche itakayopandwa kuwa ni ya matunda, mbao za ujenzi, kuni, ufugaji wa nyuki na ya dawa za asili.

Miti hiyo inayopandwa kwa lengo la kurejesha uoto wa asili jimboni humo vilevile itawasaidia wananchi kupata matunda ambayo ni chakula mbao za kujenga nyumba, kufuga nyuki, na dawa za asili na kuwanufaisha kiafya, kibiashara, kimazingira na chakula.

Prof. Muhongo alisema miche hiyo itagawiwa bure kwa wananchi wa jimbo hilo na taasisi mbalimbali alizozitaja kuwa ni pamoja na shule na zahanati.

Aidha, upandaji huo unatarajiwa kuanza wakati wa mvua za vuli mwezi wa Novemba na Desemba mwaka huu ili kusaidia miche hiyo kustawi kwa haraka kupitia maji ya mvua.

Akitembelea wananchi na kukagua miradi ya maendeleo jimboni humo juzi, Prof. Muhongo alisema miche hiyo itasambazwa kwa walengwa hao kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la utunzaji wa mazingira VI-Agroforestry chini ya ufadhili wa Serikali ya Sweden.

Katika hatua nyingine jimbo hilo limeiomba Wizara ya Maliasili na Utalii kufufua kitalu cha miti cha serikali kilichoko katika kijiji cha Suguti ili kiwe endelevu na kusaidia kukabiliana na tatizo la ukame.



Mbunge wa Musoma Vijijini, mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (kushoto) na mtaalamu wa miti, Jacob Malima, wakiwa kwenye vitalu vya miche ya miti vya Kampuni ya VI Agroforest, mjini Musoma juzi, ambapo anatarajia kuchukua miche 100,000 ya miti ya matunda na mbao kwenda kupanda katika vijiji 68 vya jimboni kwake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Chanzo wanawake kupata uvimbe tumboni chatajwa

**Na Shaban Njia,**
BUKOMBE

WANAWAKE wenye umri wa kuanzia miaka 35 na kuendelea ambao hawajabahatika kupata watoto wakati wa umri huo, wapo hatarini kupata uvimbe tumboni.

Wameshauriwa kupata ujauzito chini ya miaka hiyo na kama inatokea kuna uhitaji mkubwa wa kuzaa katika umri huo wanatakiwa kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa madaktari waliopo katika maeneo yao.

Hayo yalibainishwa na Daktari Bingwa wa Rijiolojia kutoka Hospitali ya Rufani Kanda ya Bugando, Rajabu Kidenda, kuwa kinamama hawatakiwi kukaa muda mrefu bila ya kupata ujauzito kwa kuwa inaweza kuwaletea madhara makubwa hapo baadaye.

Alisema, hali hiyo inasababishwa na uwapo wa mabadiliko ya via vya uzazi juu yao katika kipindi cha kuanzia miaka 35 na kuendelea na ili kuondokana na hilo wanatakiwa kupata mtoto chini ya miaka hiyo.

Hata hivyo alisema, kwa sasa wanatoa huduma ya kipimo cha mionzi ya sauti ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa wanawake wenye ulazima wa kupata watoto katika umri mkubwa kutokana na sababu mbalimbali.

"Huduma hizi zinatolewa kupitia Hospitali ya Charles Kulwa Memorial iliyoko Bukombe mkoani Geita na kwa siku tunawezi kutoa huduma kwa wanawake 30 kwa kutumia mashine za mionzi ya sauti huku Jumapili na Jumatatu tumeitenga kwa ajili ya kutoa elimu," alisema.

Naye Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Charles Kulwa alisema, hospitali yake iko kilometa 45 kutoka mjini Bukombe na imekuwa msaada mkubwa kwa wananchi wanaokizunguka na wamekuwa wakifanyakazi kwa kushirikiana vema na serikali katika masuala yote yanayohusu afya.

Alisema, serikali kwa sasa imeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji hasa wa binafsi ikiwa ni pamoja na kuwaunga mkono katika jitihada za kuwahudumia wananchi hasa katika masuala ya kampeni za kifua kikuu na ukoma kwa kupewa vitendea kazi.

Kwa upande wake Zuwena Alfred alisema, hakuwa anayefahamu kuchelewa kupata mtoto kama inaweza ikamletea shida ya kupata uvimbe kwenye kizazi hivyo hivyo kuahidi kuzidi kuwashauri wengine wenye kujitahidi kupata watoto mapema kuepukana na magonjwa kama hayo.

## Taasisi za dini zaitwa mkakati kuzuia ebola

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Issessanda Kaniki, amewaomba viongozi wa taasisi za dini kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa kushirikiana na serikali kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya mlipuko wa virusi vya ebola ambao umeendelea kuwa tishio katika nchi jirani ya Uganda.

Amesisitiza kuwa kupitia viongozi hao, elimu ya kujikinga dhidi ya ugonjwa huo inaweza kuwafikia wananchi wengi wa Kanda ya Ziwa kutokana na ushawishi wa viongozi hao.

Dk. Kaniki alitoa kauli hiyo juzi jijini Mwanza wakati wa kuwajengea uwezo wa namna ya uelimishaji juu ya kujikinga na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya ebola kwa kuwahusisha viongozi wa dini kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa na mipakani.

Dk. Kaniki alisema licha ya ugonjwa huo kutoingia nchini, jitihada za haraka zinatakiwa kuchukuliwa na kila mtu kuhakikisha unadhibitiwa kabla haujafika na kuleta athari kubwa.

Alisema viongozi wa dini wana uhakika wa kukutana na watu wengi na wenye itikadi mbalimbali huku wakiwa na sifa ya kuaminika zaidi, hivyo kuwataka kutumia talanta na vipawa vyao kuwafikia waamini ili kudhibiti janga hilo.

Baadhi ya wadau wa afya likiwamo shirika lisilokuwa la kiserikali la Interface Partnership, walieleza dhamira yao ya kuwakutanisha viongozi wa taasisi za dini kuwa ni kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya maambukizi ya ebola.

Asina Shenduli, Mkurugenzi Mtendaji TIP, alisema kupitia viongozi wa dini wanaimani elimu hiyo itafika mbali na kufanikisha lengo la kudhibiti ebola kuingia nchini.

Mwenyekiti mwenza wa Kamati ya Dini Mbalimbali Mkoa wa Mwanza na Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Hassani Kabeke, aliahidi kupitia baraza hilo watashirikiana pega kwa bega na serikali na wadau wa afya kufikisha elimu ya kujikinga na ebola kwa waumini wao.

Aliwataka waamini wote nchini kuwa na imani huku wakifuata taratibu za wataalamu wa afya kuepusha usambaaji wa virusi hivyo vya ebola nchini.

# Polisi yaua watuhumiwa kupora fedha za VICOBA

**Na Romana Mallya**

WAKATI watuhumiwa wawili wa ujambazi wakiuawa baada ya kudaiwa kupora Sh. milioni 1.5 ya VIKOBA Chanika jijini Dar es Salaam, Jeshi la Polisi limesema litawashughulikia wahalifu wa kutumia silaha kama lilivyofanya kwa vijana wahalifu wa mitaani (panya road).

Itakumbuka kwamba Aprili mwaka huu, panya road waliibuka jijini na kujeruhi baadhi ya wananchi na kupora mali zao na hata kuua mwanafunzi na kulilazimu jeshi hilo kufanya operesheni kuwasaka.

Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alithibitisha kuuawa kwa watuhumiwa hao wa ujambuzi juzi alipozungumzia tukio la uporaji wa fedha za kikundi cha wanawake walizokusanya ili kuziwasilisha katika taasisi ya ASA iliyoko Chanika.

Alisema wakati wanawake hao wakifanya marejesho ya kikundi chao katika taasisi ya ASA wakiwa wamekusanya fedha taslimu Sh. milioni 1.5, wahalifu hao waliwavamia na kuwatishia kwa silaha kisha kuzipora na kukimbia.

Kamanda Muliro alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 5:30 asubuhi na wakati wanawake hao wakiwa wamekaa, wahalifu wawili wakiwa kwenye pikipiki namba MC714 CLL walifika eneo hilo.

Kamanda Muliro alisema baada ya tukio hilo, mmoja wa wanawake hao alipiga kelele kuomba msaada ndipo kikundi cha bodaboda ambacho ni sehemu ya ulinzi shirishi kilichoko eneo hilo, kilipowakimbiza watuhumiwa hao hadi maeneo ya Gongo la Mboto.

"Mmoja wa watuhumiwa hao alifyatua risasi lakini bodaboda wakaendelea kuwakimbiza na kuwazuia kwa mbele wakaanguka, wakati mmoja akijaribu kukimbia akadhibitiwa na mwingine aliyekuwa na bastola akakamatwa," alisema.

Aliendelea kusimulia kuwa watuhumiwa hao walishambuliwa na polisi walifika eneo la tukio waliipata bastola ambayo imebainika kutengenezwa kienyeji na ina uwezo wa kutumia risasi.

Pia alisema eneo hilo walikuta maganda matano ya risasi yaliyotumika ya bunduki aina ya shot gun.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao walifariki dunia kutokana na majeraha ya kushambuliwa.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Muliro alisema: "Salamu kwa wahalifu tumepambana na watu waliokuwa wanajiita panya road, wamepata ujumbe wa kutosha sasa hawa watu wanaojaribu kutumia silaha na wao watashughulikiwa.

"Tumejifunza namna wananchi wa Dar es Salaam ambavyo wanavyochukia uhalifu, hawataki kabisa uhalifu, pili tumejifunza namna wananchi wanavyotoa taarifa haraka na polisi kwa kushirikiana na wananchi, walijitoa kudhibiti wahalifu hawa waliopoteza maisha."

Kamanda Muliro alisema suala la ulinzi na usalama ni la kila mwananchi na hiyo imedhihirishwa kwa vitendo kupitia tukio hilo.

"Mhalifu akiwa na bunduki na risasi amesalimu, huwezi kupambana na nguvu ya umma ukiwa mhalifu, Jeshi la Polisi limeshuka chini, jeshi lipo na wananchi, wananchi wapo na jeshi. Hizi ni salamu kwa wahalifu," alisema.

Kamanda Muliro alisema mmoja wa wahalifu hao amekutwa na leseni yenye jina Kurwa Mwakabala na anakadiriwa kuwa na umri wa miaka 22 ambaye alikuwa dereva wa pikipiki hiyo.



Mafundi wakikarabati maeneo yaliyoharibika katika Barabara ya Bagamoyo hadi Msata, mkoani Pwani mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kaya 250 kupisha hifadhi ya Shamba la Sao Hill

**Na Munir Shemweta,** IRINGA

KAYA 255 za vijiji vitatu vya Igeleke, Usokami na Kibengu vilivyoko Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa zitaondolewa eneo la hifadhi ya Shamba la Sao Hill.

Uamuzi huo ulitangazwa juzi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, wakati Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta inayoshughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 ilipotembelea na kukutana na wananchi wa Kijiji cha Kibengu kilichoko wilayani Mufindi mkoani Iringa.

Dk. Mabula alisema uamuzi unaofanywa kuhusiana na eneo hilo, una nia njema kwa mustakabali wa taifa na vizazi vijavyo kwa kuwa kaya hizo zimekuwa zikifanya shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi ikiwamo kilimo cha mazao ya kudumu na mazao ya msimu na kuharibu mazingira.

Alitaja idadi ya kaya kwa kila kijiji kuwa ni pamoja na kaya nne za Kijiji cha Igeleke kinachohusisha vitongoji vya Kihesa, Mdodi, Lwombogole na Igangilonga.

Kaya zingine ni 97 za Kijiji cha Usokami zilizoko vitongoji vya Kidete, Msega, Mgwao, Ilamba, Nyamifwa na Uhwana pamoja na kaya 154 za Kijiji cha Kibengu ambazo zote zitatakiwa kuondoka.

"Hizo ni takwimu za kaya zinazokwenda kuathirika na sio kuhama eneo moja kwenda lingine lakini kwa utaratibu maalum na hakuna atakayekuja kusema ondokeni leo," alifafanua Dk. Mabula.

Aliongeza: "Mheshimiwa Rais Samia amesema hamtaondoka bure na uthamini utafanyika kwa yeyote aliyetimiza masharti na kwa kuwa kijiji kimeandikishwa maana yake mmekidhi vigezo vya kulipwa na kila mlichowekeza katika eneo husika hakuna atakayedhurika," alisema.

Baadhi ya mapendekezo ya wataalamu kuhusiana kaya zinazotakiwa kuondoka eneo la hifadhi ya msitu wa Sao Hill mkoani Iringa ni pamoja na kuwekwa ukomo kwa wananchi kuondoa miti ndani ya hifadhi sambamba na hifadhi kutoa notsi ya kisheria kwa wananchi kuondoa miti yao kabla ya tarehe ya ukomo.

Mkoa wa Iringa unahusisha vijiji/mitaa 15 yenye migogoro ya matumizi ya ardhi ambapo vijiji hivyo vimeainishwa katika sehemu kuu sita kulingana na aina ya mgogoro na uamuzi uliotolewa na Baraza la Mawaziri.

Manaibu mawaziri wa wizara za kisekta walipo katika ziara hiyo kila mmoja alielezea umuhimu wa sekta yake katika kulinda na kuimarisha rasilimali za nchi kupitia sekta ya ardhi.

Khamis Hamza Chilo mbali na kupongeza upandaji miti ya biashara wilayani Mufindi alishauri wananchi kupanda miti ya kudumu ili kurithisha vizazi vijavyo.


"Ninasema haya kwa sababu Tanzania kwa sasa inalia na kuathirika kwa mabadiliko ya tabianchi na tuchukue tahadhari na kujitahidi kwa kutunza mazingira na kupanda miti ili mwisho wa siku tusilete athari kwa viumbe hai," alisema Chillo.

Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alieleza umuhimu wa kuwa na ng'ombe wa maziwa na kushauri wananchi wa Mufindi kujitahidi kila mmoja kuwa na angalau ng'ombe wawili na kusisitiza kuwa wizara yake iko katika jitihada za kuimarisha shamba lake sehemu ya Sao Hill.

Davida Silinde, Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI alisema ofisi yake kuanzia sasa mchakato wa kusajili vijiji utafanyika kwa ushirikiano na wizara zingine za kisekta ili kuepuka migogoro ya ardhi inayojitokeza mara kwa mara.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



citi

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## Tanzu ya Citigroup, Kampuni iliyoshirikishwa nchini Marekani

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 17,910 | 15,496 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 163,186 | 63,908 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 156,612 | 197,778 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 215,453 | 394,996 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 225 | 140 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 32,686 | 23,517 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 23,801 | 29,149 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 30,315 | 100,275 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 315,428 | 356,717 |
| 12 | Mali Nyingine | 15,344 | 15,435 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6,913 | 6,951 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **977,873** | **1,204,362** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 4,144 | 312 |
| 18 | Amana za Wateja | 794,114 | 834,946 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 9 | 9 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,424 | 2,379 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 5,610 | 4,084 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 23,837 | 29,160 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 864 | 712 |
| 27 | Dhima Nyingine | 30,879 | 34,074 |
| 28 | Madeni | 11,660 | 198,240 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **873,540** | **1,103,915** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** | **104,333** | **100,447** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | - Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,660 | 9,660 |
| 32 | - Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | - Mapato Yaliyobakizwa | 82,441 | 82,441 |
| 34 | - Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 11,085 | 6,433 |
| 35 | - Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,146 | 1,913 |
| 36 | - Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **104,333** | **100,447** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 109,979 | 104,829 |
| 39 | Mikopo Chechefu | - | - |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,511 | 1,348 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| ( i ) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.7% | 8.3% |
| ( ii ) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.0% | 0.0% |
| ( iii ) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 39.5% | 42.7% |
| ( iv ) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 32.3% | 29.6% |
| ( v ) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70.3% | 78.8% |
| ( vi ) | Ongezeko la Amana | -4.6% | 11.2% |
| ( vii ) | Ongezeko la Mali | -23.2% | 17.5% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 9,659 | 7,937 | 25,486 | 23,152 |
| 2 | Gharama za Riba | (2,021) | (1,226) | (5,272) | (5,833) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba** | **7,638** | **6,711** | **20,214** | **17,319** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (163) | (86) | (302) | (319) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **6,241** | **3,656** | **16,489** | **10,276** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 4,339 | 2,357 | 9,963 | 6,470 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,922 | 1,300 | 4,782 | 3,807 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | (20) | (1) | 1,744 | (1) |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,835)** | **(5,984)** | **(20,365)** | **(17,457)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,907) | (2,227) | (8,998) | (6,714) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (3,929) | (3,757) | (11,367) | (10,743) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **6,880** | **4,297** | **16,035** | **9,819** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (2,227) | (1,210) | (4,950) | (2,942) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **4,652** | **3,088** | **11,085** | **6,878** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | |
| | Mapato ambayo hayajakamilika | (1,095) | 1,306 | (1,249) | 1,224 |
| | Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | 329 | (392) | 375 | (367) |
| | Mapato mengine baada ya kodi ya mapato | (767) | 914 | (874) | 857 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **3,886** | **4,002** | **10,211** | **7,735** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 55 | 47 | 55 | 47 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 465,239 | 308,755 | 1,108,526 | 687,761 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| ( i ) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.9% | 1.4% | 1.4% | 0.9% |
| ( ii ) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 18.0% | 12.3% | 14.5% | 9.3% |
| ( iii ) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 49.3% | 57.7% | 55.5% | 63.3% |
| ( iv ) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.5% | 4.4% | 4.6% | 3.2% |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Imesainiwa na: Geofrey Mchangila (Ofisa Mtendaji Mkuu) — Date : 27 October 2022

Imesainiwa na: Iddi Msonga (Mkuu wa Fedha) — Date : 27 October 2022

Imesainiwa na: Godwin Rutashobya (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) — Date : 27 October 2022

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Imesainiwa na: Andulile Mwakalyeye — Date : 27 October 2022

Imesainiwa na: Wilson Chola — Date : 27 October 2022

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 6,880 | 4,440 | 16,035 | 4,297 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| -Hasara Katika Mali | 525 | 491 | 1,500 | 536 |
| -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 41,288 | (54,515) | (24,929) | (8,595) |
| -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 20 | - | 56 | 1 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (37,000) | 93,719 | (120,930) | (116,074) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (8,135) | 8,859 | 14,844 | (7,809) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (3,326) | (18,216) | (31,802) | 7,349 |
| -Kodi Iliyolipwa | (886) | (886) | (2,658) | (605) |
| -Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(634)** | **33,891** | **(147,884)** | **(120,900)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (582) | (274) | (856) | (298) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 40,071 | (2,235) | 26,448 | 2,254 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **39,489** | **(2,509)** | **25,592** | **1,956** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (186,580) | 105,160 | (80,540) | 156,553 |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(186,580)** | **105,160** | **(80,540)** | **156,553** |
| | **(147,726)** | **136,542** | **(202,832)** | **37,609** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(147,726)** | **136,542** | **(202,832)** | **37,609** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 574,814 | 438,272 | 629,921 | 364,029 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 427,089 | 574,814 | 427,089 | 401,638 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | - | **89,401** | **605** | - | **2,021** | **101,686** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 11,085 | - | - | - | **11,085** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (874) | **(874)** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | - | - | (7,564) | - | - | - | **(7,564)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 605 | (605) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | - | **93,527** | - | - | **1,146** | **104,333** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | - | **85,916** | **1,582** | - | **1,759** | **98,917** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 6,878 | - | - | - | **6,878** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 857 | **857** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | - | - | (5,057) | - | - | - | **(5,057)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 694 | (694) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | - | **88,431** | **888** | - | **2,616** | **101,595** |

## CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

### CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

| 1.0 | **Current Accounts** | **CHARGE/FEE-LCY** | **CHARGE/FEE-FCY** |
|---|---|---|---|
| | (a) Required minimum opening balance | Waived | Waived |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 20,000 | USD $20 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 4,000 | US$ 5.00 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | N/A | N/A |
| | (e) ATM mini statement | N/A | N/A |
| | (f) Interim statement per page | TZS 7,000 | US$ 5.00 |
| | (g) Periodic scheduled statement | Waived | Waived |
| | (h) Cheque book | TZS 35,000 (100 leaves) | US$ 35 (100 leaves) |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 52,000 | US$ 50 |
| | (j) Special clearance | TZS 60,000 | US$ 60 |
| | (k) Counter cheque | TZS 2,500 per leaf | US$ 2 per leaf |
| | (l) Stop Payment | TZS 30,000 | US$ 30 |
| | (m) Standing order | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| | (n) Balance enquiry | Waived | Waived |
| | (o) New ATM card issuance | N/A | N/A |
| | (p) ATM card renewal or replacement | N/A | N/A |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 5.29-8.10.08% | 4.57%-10.49% |
| | (r) Unarranged overdraft | 15% | 10% |
| | (s) Interbank transfer | Waived | Waived |
| | (t) Bill payments through ATM | N/A | N/A |
| | (u) Deposit fee | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 |
| | (v) Other (please specify) | N/A | N/A |
| | (w) BRELA Search fees. Per search | TZS 30,000 | US$ 15 |
| | (x) Foreign Loan Registration fees (DRN) | US$ 700 | US$ 700 |
| 2.0 | **Savings Accounts** | | |
| | (a) Required minimum opening balance | NA | NA |
| | (b) Monthly service fee | NA | NA |
| | (c) Interim statement | NA | NA |
| | (d) Account clossure | NA | NA |
| 3.0 | **Electronic Banking** | | |
| | (a) Internet banking monthly fee | Waived | Waived |
| | (b) Internet transfers | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.0 and Max US$ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| | (c) SMS banking | N/A | N/A |
| | (d) Other | Managers Cheques: TZS 4,000 | Managers Cheques: US$ 5.00 |

| 4.0 | **Foreign Exchange Transactions** | **CHARGE/FEE-LCY** | **CHARGE/FEE-FCY** |
|---|---|---|---|
| | (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | NA | NA |
| | (b) Purchase of foreign cheque | NA | NA |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | NA | NA |
| | (d) Telegraphic transfer | | |
| | -Inward Telegraphic Transfers [FTIN] | US$ 30 | US$ 30 |
| | -Outward International TT / Electronic [ROCT] | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 |
| | (e) Telex/SWIFT | NA | NA |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current | NA | NA |
| 5.0 | **Personal Loans** | | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| | (i) Personal loans | NA | NA |
| | (ii) Overdrafts | NA | NA |
| | (iii) Mortgage finance | NA | NA |
| | (iv) Asset finance | NA | NA |
| | (b) Unpaid loan instalment | NA | NA |
| | (c) Early repayment | NA | NA |
| | (d) Valuation fees | NA | NA |
| | (e) Other | NA | NA |

**Additional Disclossures**

| 1 | **Deposit Rates** | **LCY** | **FCY** |
|---|---|---|---|
| | -Current Account Deposits | 0%-3% | 0%-0.25% |
| | -Time Deposits | | |
| | (a) 1 - Months | 1.48% -1.68% | 2.73%-3.04% |
| | (b) 3 - Months | 2.7% - 3.00% | 3.21%-3.56% |
| | (c) 6 - Months | 3.78% - 4.08% | 3.53%-3.92% |
| | (d) 9 - Months | 4.18% -4.49% | 3.62%-4.03% |
| | (e) 12 - Months | 4.61% -4.91% | 3.72%-4.13% |
| 2 | **Lending Rate** | **LCY** | **FCY** |
| | Base lending rate | 9.58%-10.58% | 6.16%-7.16% |
| | Short term ( up to one year ) | 9.58%-10.58% | 6.16%-7.16% |
| | Medium term ( 2 to 3 years ) | 10.08%-11.08% | 6.66%-7.66% |
| | Long term ( 3 - 5 years ) | 10.58%-11.58% | 7.16%-8.16% |
| | Term loans ( over 5 years ) | 10.06%-11.06% | 7.66%-8.66% |

| 6.0 | **Trade Finance** | **CHARGE/FEE** |
|---|---|---|
| | **Documentary Collections** | |
| | Imports | Handling: $130, Acceptance $65, Telex: 0.325% minimum $98 and maximum $650 |
| | Exports | All in fee: $100 ($50 courier and $50 handling) per set of documents |
| | **Imports Letters of Credits** | |
| | Opening fees | LC issuance - 0.5% per quarter Min. $325 |
| | Handling fees | Handling: $130 |
| | Amendment Fees | Simple amendment $100, extension 0.5% per quarter if it extends to other quarter (s) |
| | Confirmation fees | Confirmation 0.39% per quarter Min. EUR 390 per quarter |
| | Risk margin on Acceptance | 0.25% per Quarter or part thereof |
| | Other Bank LC re-issuance | 0.1% per Quarter, min. $200 |
| | Bills Availization (Pour Aval) | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | **Exports Letters of Credits** | |
| | Handling fees | $500 |
| | Courier | $100 |
| | Confirmation fees | 0.25% per Quarter or part thereof |
| | Negotiation fees | 0.1% Min. $1000 |
| | **Liquidity financing** | |
| | Suppliers finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| | Accounts Receivable Finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| | **Guarantees and Standby Letters of Credits** | |
| | SBLC | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Bid Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Performance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Maintanance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Advance Payment Guarantee | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Amendments fees on Guarantees | Simple amendments $100 and 0.5% per Quarter or part thereof, if it extends into next quarter(s) |
| | Custom Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Warehouse Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Transit Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Facility fees | 1.5% per annum |

We the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information

| | **Name** | **Designation** | | **Date** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Iddi Msonga | CFO | ........................................................... | Date : 27th Oct 2022 |
| 2 | Michael Mungure | TTS Head | ........................................................... | Date : 27th Oct 2022 |
| 3 | Magdalena Neema Martin | Ag. Head of Treasury | ........................................................... | Date : 27th Oct 2022 |

217119502

# MASTAA WALIAMUA MECHI - MKWASA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Boniface Mkwasa, amesema uzoefu wa wachezaji Juma Mahadhi na Saido Ntibazonkiza ndiyo uliosababisha timu yake kufungwa 2-1 juzi dhidi ya Geita Gold na si vinginevyo.

**Alisema kama isingekuwa uzoefu wa wachezaji hao wana uhakika nafasi zilizo patikana zisingeweza kuwa mabao.**

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hizo uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Ruvu Shooting ikiwa wenyeji, Mkwasa alisema wamepoteza mechi hiyo kutokana na uzoefu wa wachezaji waliofunga mabao hayo, lakini akikiri kulikuwa na uzembe kidogo kwa wachezaji wake.

"Tumefungwa na wachezaji wazoefu, kama isingekuwa uzoefu wao, kina Mahadhi na Saido kwa wachezaji wengine yale wangeweza kukosa, lakini kulikuwa na hali ya kujisahau kwa mabeki wangu, kwenye mpira ukifanya makosa mwenzako anayatumia, walitufunga tukapambana tikasawazisha, baadaye wakatufunga tena bao la pili. Kwa haya yaliyotokea tutakwenda kujipanga ili kurekebisha makosa," alisema Mkwasa.

Naye Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, alisema mechi ilikuwa ngumu kutokana na Ruvu Shooting kuwa na timu nzuri na kocha mzuri pia.

"Haikuwa mechi rahisi, Ruvu Shooting wana timu bora na walisajili timu nzuri, namheshimu kaka yangu Mkwasa na uwezo wake kwenye kufundisha timu, tuliweka mikakati ya ushindi na tumetimiza malengo, unajua wachezaji wetu wa Kitanzania wakati mwingine wana makosa fulani ambayo ni lazima kila muda uongee nao, lakini tunashukuru tumepata pointi tatu. Minziro na Mkwasa wote waliwahi kuichezea Yanga kwa pamoja miaka ya 1980. Mkwasa yeye alianza soka katikati ya miaka ya 1970, Minziro akaja kukutana naye mwanzoni miaka ya 1980 hadi katikati.

Mahadhi na Ntibazonkiza ambao wote wamewahi kuichezea Yanga, waliifungia Geita Gold, huku Abalkassim Sulaiman akiifungia Ruvu Shooting.

Kwa matokeo hayo, Geita Gold inafikisha pointi 13 ikiwa kwenye nafasi ya saba na Ruvu Shooting ikibaki na pointi 10 kwenye nafasi ya 10.



Baadhi ya mabinti wanaopata mafunzo ya ujuzi wa fani mbalimbali katika kituo cha Reach the Goal, Mwanambaya Mkuranga mkoani Pwani, wakiimba katika ufunguzi wa kituo hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Ruvu yajipa mechi tatu kuikabili Simba*

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya kupoteza mchezo wao dhidi ya Geita Gold, Timu ya Ruvu Shooting imejipa mechi tatu kama kipimo ili kuikabili Simba Novemba 19, mwaka huu.

Ruvu ilijikuta ikipoteza mchezo wake wa juzi dhidi ya Geita Gold kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mchezo uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, amesema kuwa wanacheza mechi zao kwa mafungu hivyo baada ya kupoteza mchezo huo, watatumia michezo mitatu iliyo mbele yao kama kipimo cha kuivaa Simba.

"Ukiangalia mabeki wetu walikosa umakini kazi inayotakiwa kufanywa na kocha wetu Boniface Mkwasa ni kuweza kujitathmini kuona wapi tulikosea na kujipanga upya ili tuendelee kuwa bora na kupata matokeo mazuri.

"Kwa sasa tunajipanga kwa ajili ya michezo yetu mitatu ijayo, tunacheza mechi zetu kwa mafungu, mchezo huu umeisha, hii michezo mitatu ijayo ndiyo tunakwenda kuipa uzito mkubwa ambayo itaonyesha Ruvu Shooting ina uwezo gani ambayo ni Mbeya City, Tanzania Prisons na Azam FC.

"Hii michezo mitatu inatupeleka kwenye kipimo cha mchezo wetu dhidi ya Simba, mwalimu sasa ana kazi kubwa ya kuona afanye nini katika hii michezo ili tupate matokeo chanya tuweze kufanya vizuri katika mchezo wetu wa nne dhidi ya Simba," alisema Bwire.

## Ntibazonkiza atuma salamu Yanga Sc

**Na Shufaa Lyimo**

KIUNGO wa Klabu ya Geita Gold, Said Ntibazonkiza, amesema ushindani waliouonyesha katika mchezo wao dhidi ya Ruvu Shooting atauendeleza dhidi ya timu yake ya zamani Yanga Oktoba 29, mwaka huu.

Akizungumza jijini jana, alisema anaifahamu Yanga vizuri hivyo hana hofu akikutana nayo.

"Yanga ni timu ya kawaida ninafahamu sehemu za kuwakaba wasiweze kuifumania nyavu yetu," alisema Ntibazonkiza.

Alisema anauheshimu mchezo huo kwani unatarajiwa kuwa mgumu na wa ushindani.

Alisema lengo ni kupata pointi tatu katika mchezo huo na kudai watakuwa na faida kwa kuwa watakuwa nyumbani.

Alisema Ligi Kuu msimu huu ina ushindani kila timu imejipanga vizuri ili isishuke daraja.

Aliomba mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono ikiwamo kujitokeza kwa wingi uwanjani siku hiyo.

## Kocha JKU ashangaa kufungwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Timu JKU, Sheha Mohamed, amesema anaendelea kutafakari kwanini timu hiyo inapoteza michezo yake.

JKU imetupwa nafasi ya 11 ikiwa na alama 10 kati ya michezo tisa iliyocheza ikiwa imeshinda mara tatu sare moja na imefungwa mitano mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili, kocha Mohamed alisema timu yake inacheza vizuri lakini bado anashindwa kujua tatizo linalofanya hadi wakafungwa michezo mitano mfululizo.

Alisema katika michezo yote waliyocheza haoni kosa kwa wachezaji wake pengine ndio yanapelekea kupoteza mchezo licha ya kuwepo kwa makosa ya kawaida.

Aidha, alisema kuwa wanahitaji kupambana ili kuhakikisha wanashinda michezo inayofuata na kuweka timu katika nafasi nzuri kabla ya kuelekea dirisha dogo.

"Kwangu naona kama upepo mbaya umeipitia timu, nashindwa kuelewa wapi tunakosea mpaka tunapoteza mchezo, wachezaji wangu wanacheza vizuri katika viwango vyao na hakuna mchezaji aliyeshuka kiwango, lakini bado tunashindwa kupata alama tatu kwa michezo mitano mfululizo, kufungwa kwetu ni goli moja tu," alisema.

Timu ya JKU itatupa karata yake uwanjani katika mchezo wake wa 10 wa Ligi Kuu Zanzibar Jumatatu ya Oktoba 31 dhidi ya Maafande wenzao wa Mafunzo.

## ZISIKUPITE

### NAPOLI HAWAMTAKI RONALDO

KLABU ya Napoli imekuwa ikihusishwa na mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, lakini mkurugenzi wa klabu hiyo ya Italia, Cristiano Giuntoli amefutilia mbali uwezekano wa kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno. (***DAZN, via Talksport***)

### GUIMARAES AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL ndio klabu ya hivi karibuni zaidi kuhusishwa na kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Chelsea na Real Madrid wanaomtaka pia, kama Newcastle United watashindwa kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kusaini mkataba mpya. (***TNT Sports***)

### DUMFRIES ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inamfuatilia mlinzi wa Inter Milan na Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 26, wakati wakijaribu kuongeza upana zaidi kwenye nafasi yao ya beki wa kulia ambayo imepwaya baada ya kuumia kwa mchezaji wa kimataifa wa England, Reece James mwenye umri wa miaka 22. (***90 Min***).

### SKRINIAR HAUZWI

RAIS wa Inter Milan, Steven Zhang amesema mlinzi wa Slovakia, Milan Skriniar ambaye inaaminika anasakwa na Paris St-Germain, hauzwi na "ana imani" mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 atabakia katika klabu hiyo ya Serie A. (***Sky Sport Italia, via Football Italia***)

### GIL, TANGANGA KURUHUSIWA

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kuwaruhusu winga wa Hispania, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 21 na mlinzi wa England, Japhet Tanganga mwenye miaka 23 kuondoka Januari, huku pia wakimtoa kwa mkopo beki wa kulia wa England, Djed Spence mwenye umri wa miaka 22. (Times)

### ILING JR KUPEWA MKATABA

KLABU ya Juventus inataka kumpa winga, Samuel Iling-Junior mwenye umri wa miaka 19 mkataba mpya, huku mazungumzo kati ya pande hizo mbili yakiwa yameanza. (***Calciomercato***)

### EDU KUONGEZEWA MKATABA

KLABU ya Arsenal imefanya mazungumzo ya awali kuhusu mkataba mpya na mkurugenzi wa ufundi Edu ambaye amekuwa akihusishwa na majukumu kama hayo katika klabu nyingine Ulaya. (***Evening Standard***)

### PODENCE AWINDWA WOLVES

KLABU ya Everton wanavutiwa na mshambuliaji wa Ureno, Daniel Podence mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake na Wolves utaendelea hadi msimu wa joto wa 2024. (***Football Insider***)

### FOREST KUTUMIA PAUNI MIL 100

KLABU ya Nottingham Forest inapanga kutumia kati ya pauni milioni 50 hadi 100 kwenye dirisha la uhamisho la Januari ili kuimarisha timu yao kwenye Ligi Kuu ya England. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LAPORTA: AIBU BARCA KUTOLEWA MAKUNDI

### ●●● Akataa kuwalaumu wachezaji, asema bado wana mradi mchanga na...

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amekiri kuondolewa kwa timu yake kwenye hatua ya makundi katika Ligi ya Mabingwa Ulaya ni aibu, lakini alikuwa na falsafa kuhusu "mradi wao mchanga" chini ya Xavi.

The Blaugrana waliondolewa rasmi na kutupwa kwenye Ligi ya Europa baada ya ushindi wa Inter wa 4-0 dhidi ya Viktoria Plzen mapema Jumatano, huku wao wakichezea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Bayern Munich.

Barcelona wametolewa kwa msimu wa pili mfululizo kwenye hatua ya makundi, ikiwa ni takribani miezi 12 tangu kuteuliwa kwa Xavi kuchukua nafasi ya Ronald Koeman.

Washindi hao mara tano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya walifanya usajili mkubwa katika msimu wa kwanza wa Xavi, wakiwaleta Robert Lewandowski, Jules Kounde, Andreas Christensen, Hector Bellerin, Franck Kessie, Marcos Alonso na Raphinha.

Kushindwa kwa Barca kufika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa kutakuwa na athari za kifedha kwa klabu, lakini Laporta ana falsafa yake.

**"Ni aibu, lakini huwezi kuwalaumu wachezaji au kocha kwa lolote," alisema Laporta akiiambia Barca TV.**

"Lazima tuangalie mbele, kwa sababu tumebakiza LaLiga na mashindano mengine.

"Huu ni mradi mchanga ambao tangu mwanzo tulijua tutakuwa na heka heka. Ligi inabaki na tunapaswa kuonesha kuwa tunaendelea."

The Blaugrana wanashika nafasi ya pili kwenye LaLiga baada ya kuanza vyema kampeni hii wakiwa na pointi 28 katika michezo 11, pointi tatu nyuma ya Real Madrid, ambao ushindi wao wa El Clasico mapema mwezi huu uliwaweka kileleni.

"LaLiga ni muhimu sana na tunakaribia," alisema Laporta. "Ujumbe ni kuangalia mbele. Hili tayari limetokea."

Kipigo cha Barca cha 3-0 nyumbani kwa mabingwa hao wa Ujerumani kilikuwa kipigo cha sita mfululizo dhidi ya Bayern, ikiwa ni pamoja na kipigo cha 8-2 cha robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2020.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,044,3

MECHI KALI

MALLORCA
VERSUS
ESPANYOL

1 | 2.22
X | 3.06
2 | 3.41

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom | m-pesa
BREAKING
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# OBLAK AOMBA RADHI MASHABIKI ATLETICO

**MADRID,** Hispania

GOLIKIPA Jan Oblak anaamini kuwa mashabiki wa Atletico Madrid "wanastahili zaidi" baada ya Los Rojiblancos hao kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Atletico walitolewa hatua ya makundi kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka mitano baada ya sare ya 2-2 na Bayern Leverkusen kwenye Uwanja wa Civitas Metropolitano, ambapo mkwaju wa penalti wa dakika za lala salama wa Yannick Carrasco uliokolewa na Lukas Hradecky.

Baada ya Porto kuicharaza Club Brugge mabao 4-0 ilimaanisha ushindi pekee dhidi ya Leverkusen ungetosha kudumisha matumaini yao ya kusonga mbele kutoka kundi B.

"(Ni) njia ya ukatili sana (ya kuondolewa). Ni soka," alisema golikipa huyo akiiambia Movistar+.

"Tumefanya kila kitu kushinda, lakini michezo iliyopita imetuadhibu, hatujapata bahati kidogo inayohitajika.

"Tunaweza tu kushukuru kutoka chini ya mioyo yetu kwa sapoti ya mashabiki. Wanastahili zaidi. Timu inasikitika sana.

"Ni kosa la timu nzima. Na si mechi hii tu, bali hata zile zilizopita. Ni aibu kwamba hatuwezi kuendelea kwenye Ligi ya Mabingwa."



## Conte awa mbogo maamuzi VAR

**LONDON,** England

KOCHA Antonio Conte aliishutumu VAR kwa "kutengeneza matatizo makubwa " baada ya bao la Harry Kane la dakika ya 95 kukataliwa katika sare ya 1-1 na Sporting CP, akidai klabu nyingine kubwa huwa na wakati mzuri zaidi kuliko Spurs.

Tottenham walidhani walikuwa wametinga hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya huku kukiwa na mchezo mmoja uliobakia, wakati Kane alipofunga bao dakika ya mwisho baada ya Rodrigo Bentancur kusawazisha lile la Marcus Edwards.

Hata hivyo, Kane alionekana ameotea baada ya ukaguzi wa dakika tatu wa VAR, na kuwaacha wenyeji wakiwa na hasira.

Conte alioneshwa kadi nyekundu na mwamuzi, Danny Makkelie wakati benchi la Tottenham likilipuka kwa kupinga uamuzi huo, na aliendelea kuelezea hasira yake katika mahojiano yake baada ya mechi.

"Kuhusu mwisho, nadhani mpira ulikuwa mbele ya Kane na lile ni bao. Sielewi VAR, mstari ambao waliweka," alisema Conte akiiambia BT Sport.

303,118/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/10/22 | 17:00 | Hull City vs Blackburn | 2.59 | 3.19 | 2.74 |
| 02. 29/10/22 | 17:00 | Wigan vs Watford | 2.93 | 3.28 | 2.39 |
| 03. 29/10/22 | 17:00 | Preston vs Middlesbrough | 2.68 | 3.13 | 2.68 |
| 04. 29/10/22 | 17:00 | Huddersfield vs Millwall | 2.99 | 3.24 | 2.37 |
| 05. 29/10/22 | 17:00 | Brighton vs Chelsea | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 06. 29/10/22 | 19:30 | Fulham vs Everton | 2.29 | 3.42 | 2.97 |
| 07. 29/10/22 | 19:30 | Eintracht Frankfurt vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.52 | 2.25 |
| 08. 29/10/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.53 | 3.53 | 2.58 |
| 09. 30/10/22 | 15:00 | AJ Auxerre vs AC Ajaccio | 2.45 | 3.07 | 2.97 |
| 10. 30/10/22 | 15:30 | Hannover vs Karlsruher SC | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 11. 30/10/22 | 15:30 | Sandhausen vs Eintracht Braunschweig | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 12. 30/10/22 | 15:30 | Paderborn vs Hamburger SV | 2.28 | 3.73 | 2.79 |
| 13. 30/10/22 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 14. 30/10/22 | 17:00 | Brest vs Reims | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 15. 30/10/22 | 18:30 | Boavista vs Vizela | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 16. 30/10/22 | 19:00 | Sandefjord vs Ham-Kam | 2.58 | 3.37 | 2.63 |
| 17. 30/10/22 | 19:05 | Lorient vs Nice | 2.57 | 3.26 | 2.67 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 28/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 3439 | Blacks Power FC vs Dove All Stars | 7.00 | 4.80 | 1.39 |
| 16:00 | 5341 | Hapoel Ramat Gan vs Hapoel Acre | 2.75 | 2.75 | 2.95 |
| 16:30 | 5574 | Ajax Cape Town vs Uthongathi | 2.63 | 2.78 | 2.78 |
| 17:00 | 1248 | FC Metalist 1925 vs Zorya Lugansk | 4.00 | 3.70 | 1.72 |
| 17:00 | 1917 | Kerala Blasters FC vs Mumbai City FC | 2.62 | 3.30 | 2.41 |
| 17:00 | 4587 | Glentoran Belfast vs Larne | 2.27 | 3.11 | 2.96 |
| 17:00 | 5002 | Gazovik Orenburg vs Fakel | 1.91 | 3.62 | 3.57 |
| 18:00 | 1568 | Chindia Targoviste vs Botosani | 2.10 | 3.08 | 3.57 |
| 18:30 | 3518 | Domzale vs ND Gorica | 1.80 | 3.50 | 3.88 |
| 18:30 | 4170 | Zlate Moravce vs MSK Zilina | 2.68 | 3.32 | 2.35 |
| 19:00 | 1158 | Miedz Legnica vs Pogon Szczecin | 3.46 | 3.31 | 1.97 |
| 19:00 | 2322 | HNK Sibenik vs Vsnk Varazdin | 2.78 | 3.12 | 2.39 |
| 19:00 | 5294 | Akritas Chlorakas vs AEL Limassol | 3.94 | 3.39 | 1.92 |
| 19:30 | 3003 | Magdeburg vs Heidenheim | 2.68 | 3.57 | 2.35 |
| 19:30 | 3381 | Greuther Furth vs Arminia Bielefeld | 2.04 | 3.53 | 3.28 |
| 20:00 | 1349 | FC Helsingor vs Vendsyssel FF | 2.04 | 3.45 | 3.11 |
| 20:00 | 2024 | Fatih Karagumruk vs Galatasaray | 3.58 | 3.68 | 1.91 |
| 20:00 | 3424 | Altinordu vs Yeni Malatyaspor | 1.89 | 3.45 | 3.55 |
| 20:00 | 5949 | Nordsjalland vs Horsens | 1.62 | 3.93 | 4.88 |
| 20:30 | 4698 | Yverdon-Sport FC vs Lausanne-Sport | 2.67 | 3.44 | 2.30 |
| 20:30 | 4975 | Neuchatel Xamax vs FC Thun | 2.68 | 3.55 | 2.25 |
| 21:00 | 1875 | U Craiova SA vs Farul Constanta | 3.02 | 3.02 | 2.39 |
| 21:00 | 2913 | Helmond Sport vs ADO Den Haag | 2.77 | 3.51 | 2.28 |
| 21:00 | 3091 | Telstar vs Dordrecht | 1.75 | 3.60 | 4.25 |
| 21:00 | 3383 | VVV Venlo vs Jong AZ Alkmaar | 2.08 | 3.49 | 3.14 |
| 21:00 | 4238 | Den Bosch vs NAC Breda | 2.77 | 3.51 | 2.28 |
| 21:00 | 4271 | PEC Zwolle vs Maastricht | 1.29 | 5.36 | 8.14 |
| 21:00 | 4339 | FC Eindhoven vs Jong PSV | 1.88 | 3.45 | 3.79 |
| 21:00 | 5318 | Roda Kerkrade vs Jong Utrecht | 1.47 | 4.34 | 5.72 |
| 21:00 | 5891 | Almere City vs Heracles Almelo | 2.72 | 3.56 | 2.29 |
| 21:00 | 5907 | De Graafschap vs FC Oss | 1.51 | 4.25 | 5.33 |
| 21:15 | 1493 | FC Stade LS Ouchy vs FC Aarau | 2.21 | 3.56 | 2.73 |
| 21:15 | 3989 | FC Wil vs FC Schaffhausen | 1.98 | 3.65 | 3.12 |
| 21:30 | 3110 | Werder Bremen vs Hertha BSC | 2.03 | 3.67 | 3.17 |
| 21:30 | 3160 | Gornik Zabrze vs Widzew Lodz | 2.24 | 3.16 | 2.96 |
| 21:45 | 1616 | Queens Park vs Dundee FC | 3.15 | 3.44 | 2.10 |
| 21:45 | 3391 | Morton vs Inverness | 2.30 | 3.15 | 3.00 |
| 21:45 | 3564 | Racing Genk vs Mechelen | 1.38 | 4.98 | 6.78 |
| 21:45 | 3714 | Shelbourne vs Drogheda Utd | 1.92 | 3.31 | 3.61 |
| 21:45 | 4624 | Glenavon vs Ballymena Utd | 1.89 | 3.55 | 3.45 |
| 21:45 | 4653 | Dundalk FC vs Bohemians FC | 1.72 | 3.65 | 4.08 |
| 21:45 | 4677 | Gap Connahs Quay vs Newtown AFC | 1.54 | 3.85 | 5.26 |
| 21:45 | 5317 | Sligo Rovers vs St Patricks | 3.45 | 3.30 | 1.97 |
| 22:00 | 2189 | Finn Harps vs UCD Dublin | 1.75 | 3.60 | 3.99 |
| 22:00 | 3114 | Mallorca vs Espanyol | 2.22 | 3.06 | 3.41 |
| 22:00 | 4334 | Tenerife vs Zaragoza | 2.13 | 2.92 | 3.72 |
| 22:00 | 4880 | Birmingham vs QPR | 2.42 | 3.18 | 2.83 |
| 22:00 | 4927 | Lens vs Toulouse | 1.55 | 4.19 | 5.18 |
| 22:00 | 5845 | Aberystwyth Town vs Flint Town United | 2.63 | 3.46 | 2.32 |
| 22:15 | 5394 | Pacos Ferreira vs Maritimo | 2.23 | 3.19 | 3.19 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MKULIMA WA MPUNGA ASHINDA MIL 31 ZA MULTIBET

**Na Mwandishi Wetu**

MKULIMA wa mpunga, anayefanyia shughuli zake za kilimo Wilaya ya Mbarali, Fred Seth Nkyami ameshinda Sh, 31,107,991 ya Multibet bonus ya Sportpesa aliyoshinda kupitia mikeka mitatu tofauti.

**Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za Sportpesa jijini Dar-Es-Salaam, amesema alianza kucheza mwishoni mwa mwaka 2019, baada ya kutoridhishwa na wigo wa kiwango cha kuweka na kushinda katika kampuni nyingine.**

"Nilianza kucheza na Sportpesa miaka mitatu iliyopita. Mimi ni mmoja wa wakongwe wa mchezo huu. Nilianza kucheza na kampuni nyingine jina sitaitaja kwa sasa, lakini baada ya kutoridhishwa na chaguzi chache za masoko na pia kiwango cha fedha cha kuweka na cha kushinda niliamua kuhamia Sportpesa," alisema.

Kwa mujibu wa maelezo yake Fred makampuni mengine wameweka wigo mdogo sana wa kuweka kiwango cha fedha, tofauti na matamanio yake, huku pia kiwango cha juu cha ushindi na malipo vikiwa navyo haviridhishi.

"Hili jambo halipo Sportpesa. Mimi nilikuwa naona kupitia vyombo vya habari mbali mbali kama magazeti, mitandao ya kijamii na televisheni namna washindi wa Sportpesa walikuwa wanalipwa.

Siku za nyuma tulizoea kuona washindi wa Jackpot na Jackpot bonus na sasa pia tunaona kuna washindi wa multibet wanatangazwa pia.

Akielezea namna alivyoshinda multibet bonus yake. Fred amesema kwanza alicheza mikeka mitatu tofauti ya mechi 50. Pili alicheza mikeka yake yote kwa mfumo wa dabo chansi kwa sababu alihisi huo ndio mfumo mzuri kwake.

"Kuna aina ya odds ambazo mimi huwa nazilenga na odds hizo huwa naweka kwa dabo chansi ya aina mbili. Ya kwanza timu ya nyumbani ishinde au itoe suluhu na dabo chansi ya pili huwa naweka timu ya ugenini ishinde au itoe suluhu".

Fred anawashauri Watanzania wajitahidi kucheza na kujaribu bahati zao na waamini kwamba lolote linawezekana kwa uwezo ambao Mungu amempa kila mja wake na pili lazima uweke jitihada kidogo kama kuchambua na kufuatilia timu zinazocheza na pia kuangalia mwenendo wa odds.

Kuhusu atafanyia nini fedha hiyo aliyoshinda ya Multibet ya Sportpesa, Fred amesema atawekeza kama mtaji kwenye shughuli zake za kilimo cha mpunga anachofanya.

Akizungumzia ushindi wa Fred, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya alimpongeza Fred kwa ushindi wake na kumtaka aendelee kucheza ili ashinde zaidi.




Mshindi wa Multibet bonus, Fred Seth Nkyami kutoka Mbarali, Mbeya akishikilia mfano wa hundi ya shilingi 31,107,991 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 50 kwenye mechi za wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba Queens kamili Morocco michuano CAF

INATOKA UKURASA 32

"Simba iko vizuri na imepata ushirikiano kutoka kwa wenyeji, tunajua tumekuja kupambana na akili na nguvu zetu tumezielekeza kufikia malengo ya kufanya vyema, tunajua mashindano haya ni makubwa na timu zote zilizofuzu ni nzuri," Chicco alisema.

Simba Queens imepangwa katika Kundi A na itafungua pazia la mashindano haya Jumapili kwa kuwavaa wenyeji ASFAR Queens kuanzia saa 2: 00 usiku kwa saa za hapa sawa na saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Fainali hizi zinazosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zinafanyika kwa mara ya pili ambapo mwaka jana zilichezwa Misri na Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Afrika Kusini, Mamelodi Sundowns ilifanikiwa kutwaa ubingwa.

## *Nabi aandaa silaha kuwavaa Watunisia*

INATOKA UKURASA 32

hawakuwa mchezoni kwa kushindwa kufuata maelekezo aliyowapa.

Alisema kama kocha hana wakumtupia lawama sababu licha ya kuushika mchezo katika kipindi cha kwanza lakini walishindwa kutumia madhaifu ya wapinzani wao kupata ushindi.

"Hatukucheza vizuri kuanzia nyuma hadi nafasi ya ushambuliaji tulifanya makosa mengi wachezaji walikuwa wazito katika kutimiza majukumu kwahiyo kiujumla siwezi kuainisha ni wapi palikuwa na mapungufu bali ni timu nzima hatukucheza vizuri," alisema Hitimana.

Michezo
Ijumaa Oktoba 28, 2022
Nipashe



'Barca kutolewa makundi ni aibu' UKURASA 29

KITU NA BOX...



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto' (katikati), akipiga shuti lililozaa goli huku akizongwa na wachezaji wa timu ya KMC FC, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nabi aandaa silaha kuwavaa Watunisia

## Asema amewapa mapumziko maalumu wachezaji nyota, autaja ushindi wa KMC...

**Na Saada Akida**

BAADA ya Yanga kuendelea na rekodi ya kutopoteza mechi 44 za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi ameanza kuandaa silaha zake kuelekea mchezo wa kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

**Juzi Yanga ilifanikiwa kuendelea kufanya vizuri na kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMC na kuipandisha kileleni mwa msimamo wa ligi wakifikisha pointi 17.**

Wakati wakijivunia rekodi hiyo, Nabi ameanza mikakati ya kujipanga na mechi ya Kimataifa watakayoanza nyumbani Novemba 2 mwaka huu katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na marudiano ugenini Novemba 9.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Nabi alisema pamoja na ushindi walioupata, mchezo ulikuwa mgumu kwa sababu ya ubora waliokuwa nao wapinzani, pamoja na uchovu na mabadiliko aliyoyafanya kwenye kikosi kilichangia kucheza chini ya kiwango.

Alisema kulingana na ugumu wa mechi iliyopo mbele yake analazimika kuwapa mapumziko baadhi ya wachezaji wake kuwa fiti kwa ajili ya mchezo wa kimataifa.

"Niwapongeze wachezaji wangu, kupambana na kupata pointi tatu, hatukucheza vizuri wachezaji wengi niliowatumia hawakuwa na utimamu wa mwili sababu hawachezi mara kwa mara, lakini walipambana kipindi cha pili na tukapata bao.

"Nilisema mchezo utakuwa mgumu sababu KMC ni timu inayoimarika kila msimu matokeo yao dhidi ya timu za Simba, Azam FC yanathibitisha ubora waliokuwa nao kitu cha msingi kwetu ilikuwa ni pointi tatu," aliongeza.

"Katika mechi ya leo (juzi) hakuonekana Fiston Mayele na Djuma Shabaan nimewapumzisha kwa sababu kuna mechi ngumu mbele yetu ambayo tunahitaji kushinda na kusonga mbele," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema ameangalia mechi mbili za Club Africain wakicheza ugenini na nyumbani wanakuwaje na watapambana kupata matokeo mazuri kwenye uwanja wa Mkapa.

"Mpinzani wetu mgumu, kwa hiyo lazima tujipange kwa nguvu zote kuhakikisha tunapata matokeo mazuri nyumbani," alisema.

Alisema anafahamu soka la Tunisia jambo ambalo ni faida kubwa kwake kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo wa nyumbani kabla kwenda nchini humo kwa ajili ya marudiano.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Thiery Hitimana alisema timu yake ilistahili kuadhibiwa kutokana na wachezaji wake

INAENDELEA UK. 31

# Simba Queens kamili Morocco michuano CAF

**Na Somoe Ng'itu,** RABAT

KIKOSI cha Simba Queens kimetua salama jijini Rabat nchini Morocco tayari kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Jumapili jijini hapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanasubiri kuanza kupeperusha vyema bendera ya klabu na Tanzania.

Makanya alisema kikosi kilitarajia kuanza rasmi mazoezi jana usiku na wanashukuru hali ya hewa kwa sasa jijini hapa ni nzuri na inafanana na Dar es Salaam.

"Tunamshukuru Mungu tumefika salama hapa Rabat, safari yetu ilikuwa nzuri na wenyeji wetu kutoka Chama cha Soka Morocco walitupokea vizuri, hakuna changamoto yoyote tuliyokutana nayo, tunaamini kila kitu kitaenda vizuri, " alisema Makanya.

Meneja huyo aliongeza anafurahi kuona kila mchezaji aliyesafiri hapa ana shauku kubwa ya kutimiza kile ambacho mashabiki, wanachama na viongozi wa Simba wanachokisubiri.

Naye Ofisa Habari wa Simba, Ally Shatry 'Chicco' aliliambia gazeti hili kwa upande wa utawala maandalizi yote kuelekea mashindano haya yamekamilika na tumejipanga vizuri.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >